SUPA JACKPOT
TZS. 1,056,554,107
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.co.tz
PIGA *150*87#



UKURASA 4

## RIPOTI MAALUM
Ugonjwa usio na tiba tishio kwa wenyeji wa migodini



MIAKA 61 YA UHURU

IJUMAA DESEMBA 9, 2022

Nipashe

NYERERE MWINYI MKAPA KIKWETE MAGUFULI

MRISHO MAKWAYA NA NYUMBA YAKE ...

**Ngome 'kivita' TANU ilikoasisiwa kwa siri, mahali Nyerere alikopata salamu na kuanza safari ya UNO**

• Makamanda wake; Kassanga Tumbo, Tewa, Maswanya...

Na Neema Hussein, Mpanda

LEO hii ni mzee tena hasa kwa umri, mwenye heshima na jina kubwa kwa maana ya kitaifa, akibeba maana ya uhuru wa nchi Tanganyika kwa hoja na vielelezo.

Huyo ni Mzee Selemani Makwaya, ambaye tarehe za kuwania uhuru alikuwa bwana mdogo, ila baba yake

Mzee Mrisho Makwaya, ndiye alikuwa ameiva katika harakati hizo, akiwa swahiba wa nahodha wa nyendo za kuwania uhuru nchini, Hayati Mwalimu Julius Nyerere.

Mzee Selemani anadokeza kuwa na bahati ya kuambiwa mengi kutoka kwa baba yake aliyefariki mwaka 2016, mbia wa kabla na baada ya kupatikana uhuru wa Tanganyika,

...

hapo mgodini, basi walimchukua wakampeleka humo mgodini wakampa hiyo tenda ya viatu," anasimulia.

Anaendelea: "Urafiki wao Mrisho Migila Postamasta na Nyerere, wakaanzisha klabu, kumbe ndio chama chenyewe ambacho ni TANU. Sasa wakafungua na grosariy hapo wakawa wanauza na bia, Nyerere akiwa ni Katibu.

"Basi harakati za Nyerere zikaendelea kupamba moto huko Tabora katika kukutana kwao, Mwalimu Nyerere akaanza kumwambia huyo Postamasta 'bwana sasa hii nchi ya Tanganyika vipi huko Shinyanga wapo makaburu, Mpanda?' wapo makaburu (akajibiwa), hizo ndio sehemu za kupeleka chama maana ndio ngome kubwa makaburu wanachukua mali na kuondoka nazo."

Anasema, wakakubaliana kwamba, ndiko maeneo panapaswa kuwekezwa harakati zao za kudai uhuru, hasa penye mikusanyiko ya wayui kama machimboni...

UKURASA 13

# Nipashe

Ijumaaa Desemba 9, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581154

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US

# PANGA LAJA

## SAMIA kufyeka walioshindwa kwenda na kasi yake, JK asema uongo unaigawa CCM...

*Endelea Ukurasa wa 2*




Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akisalimiana na Makamu Mwenyekiti wa CCM Zanzibar mstaafu, Dk. Ali Mohamed Shein, wakati wa Mkutano Mkuu wa 10 wa CCM, jijini Dodoma jana. Kushoto ni Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Abdulrahman Kinana. **PICHA: IKULU**

UKURASA WA 3

### SHULE 7,000 ZAHITAJI UKARABATI MKUBWA

SHULE za msingi 7,000 kati ya 17,000 nchini zilizofanyiwa tathmini na serikali, zimebainika kuhitaji ukarabati mkubwa kutokana na uchakavu wa miundombinu uliopo.

UKURASA WA 5

### MAKAMBA ARIDHISHWA MRADI UCHAKATAJI

WAZIRI wa Nishati, January Makamba, amesema ameridhishwa na maandalizi ya uwekezaji wa mradi wa kuchakata na kusindika gesi asilia (LNG...

UKURASA WA 5

### MFANYABIASHARA KIZIMBANI MASHTAKA DAWA ZA KULEVYA

MFANYABIASHARA maarufu Mohamed Abdallah 'Chonji' na wenzake wanne wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini...

## Prof. Assad kuteta na mwanasheria hukumu kuvuliwa cheo cha CAG

UKURASA 3



## Wakili ajitoa kesi ya Makonda

UKURASA 3

MICHEZO AZAM FC YAINGIA 'VITANI' NA YANGA UK. 32

KATUNI UK. 6



Mkurugenzi wa Kitengo cha Haki za Binadamu Wizara ya Katiba na Sheria, Sarakikya Nkasori (wa pili kulia), akikabidhi cheti na tuzo ya Mwanaharakati Kijana wa Haki za Binadamu kwa Daktari wa Hospitali ya Aga Khan, Zainab Artan, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Haki za Binadamu, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Samia asema panga linakuja

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MWENYEKITI wa Taifa wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais Samia Suluhu Hassan, amesema baada ya kukamilisha kupanga safu katika chama, anatarajia kuifumua serikali.

Samia alisema hayo jana wakati akifunga Mkutano Mkuu wa 10 wa CCM jana katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete jijini hapa huku akibainisha kwamba anataka kufanya hivyo kutokana na baadhi ya viongozi hawaendani na kasi yake.

"Tumepanga safu nzuri naomba baraka zenu nikapange serikali kwa namna ambayo nitaona timu hii inaweza kwenda kutekeleza yale mliyoyasema hapa kwa vizuri. Yaliyoelezwa hapa ni utekelezaji wa miaka miwili lakini katika safari yangu ya miaka miwili.

"Nahisi kabisa nina watu ambao mwendo wao hauendani na kasi yangu. Tuna safari ya miaka mitatu mbele kabla hatujaenda kuwajibishwa kwa wananchi. Kwa hiyo miaka mitatu iliyobaki nataka serikali zote mbili zifanye kazi. Tutakapokwenda kwa wananchi twende tukasimame, tuwe na ya kuwaambia.

"Tunapokwenda kwa wananchi ni wananchi wenyewe ndio wanaosema serikali iliyofanya kwao na si utamaduni wa nyuma wa serikali kuwaambia. Wakati mwingine wanashangaa hiki kimefanyika wapi," alisema.

Sambamba na hayo, Samia alisema kuna vijinongwa ndani ya chama vinaendelezwa na kwamba kwa mwana CCM ambaye anakijua chama na mwelekeo wa CCM hawezi kufanya mambo hayo.

"Kwa wana CCM waliotokana na Chama Cha Mapinduzi, hawawezi kufanya nongwa kuharibu chama chao. Lakini kuna wana CCM walioshika nyadhifa tofauti tofauti wakapitia CCM hawa wanaweza kutuharibia chama. Ninatoa wito kwa wanachama kuzingatia ukweli huo na tushirikiane," alisema.

Samia aliagiza watendaji wa Zanzibar na Tanzania Bara kushirikiana kuijenga Tanzania kwa kuheshimiana na kuzingatia mipaka ya madaraka yao.

Ma- RC, ma-DC KIKAANGONI

Katika kile kinachoonyesha kuwaweka kikaangoni wakuu wa mikoa na wilaya, Samia alisema viongozi hao wahojiwe utekelezaji wa ilani na kama chama kwenye eneo hilo kitasema hakimuelewi, atakwenda na upepo.

"Tuwatumikie wananchi kwanza na ndio watakavyokuheshimu. Heshima ya kweli haitokani na mabavu wala vitisho. Utawala bora kila mmoja ajipime kwenye eneo lake, turudishe imani kwa wananchi," alisema huku akibainisha kuwa serikali ya CCM itajiepusha na ulevi wa madaraka na matumizi ya mabavu.

"Jukumu letu ni kuhakikisha CCM hailali usingizi wala kulewa madaraka. Lazima iheshimu imani ya wananchi walioichagua kwa kuwa viongozi ni watumishi. Mimi ni kiongozi mtumishi nipo hapa kuwatumikia Watanzania na si kujitumikia, asiyekubaliana na hali hiyo ajue nafasi yake ni ndogo," alisema.

Mwenyekiti huyo pia alisema amegundua kuna kulegalega usimamizi wa haki za raia kwenye taasisi na ameunda timu itakayofanya mapitio haki za raia kwenye taasisi ili kuleta mapendekezo.

"Huko nyuma wananchi walikuwa wanakimbilia CCM kuwasilisha kero zao, turudishe imani kwa wananchi. Tutasimamia haki zao zilizosimamiwa zilizoahidiwa kikatiba na si vyema kunyanyaswa au kudhulumiwa na mamlaka za dola," alisema.

**KUJIIMARISHA KIUCHUMI**

Alisema wasibaki na CCM ya vibanda vya biashara bali watengeneze miradi mikubwa kwa kuwa uwezo wa kiuchumi unanunua uwezo wa kisiasa.

"Mfumo wa ukaguzi unakwenda kuimarika, chama tukaimarishe uwezo wa jumuiya zetu na si jumuiya ombaomba, zitakwenda kwa matajiri tupeni mtapandikiziwa watu," alisema.

**HAKUNA KILICHOSIMAMA**

"Mmeona kwa vielelezo hakuna kilichosimama, msichukue maneno ya pembeni nyie ndio wenye serikali mara bwawa limesita, pengine mwezi huu tunaenda kuanza zoezi la kuweka maji kuzalisha umeme,"alisema.

Pia alisema mambo mazuri ambayo hayamo kwenye ilani pia yatatekelezwa kama ilivyo Royal Tour. Alisisitiza umuhimu wa kishirikisha sekta binafsi huku akisisitiza kuwa serikali itaweka mazingira mazuri ili sekta binafsi ishiriki katika maendeleo ya uchumi.

Kuhusu kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti, alisema amepokea kwa moyo mkunjufu kazi aliyokabidhiwa ya kuendelea kukiongoza chama kwa miaka mitano ijayo. Aidha, alisema CCM ndio baba lao kwenye kuimarisha demokrasia nchini na hakuna chama cha siasa ambacho ni mfano wa demokrasia nchini zaidi ya CCM.

"Uchaguzi wa chama na jumuiya zake uliofanyika umedhihirisha tuna hazina kubwa ya viongozi, Mwaka huu ulikuwa na wagombea wengi sana kwa hakika uchaguzi huu umekuwa kielelezo cha ukomavu wa demokrasia na imethibitisha CCM si mali ya mtu ni mali ya wanachama," alisema.

Hata hivyo, aliwataka kuzika tofauti zao na kuwa mtindo mpya wa kuzikabili na mazingira yaliyopo sasa kwa kuwa kila zama zina vikwazo vyake ni vyema kuzifanya kazi.

Aliwataka kuimarisha umoja na mshikamano na wasikubali mikiki ya uchaguzi iwe chanzo cha mfarakano na kuanzisha nyufa ndani ya CCM.

"Wakati wa uchaguzi makundi ni mengi tutatofautiana lakini tukimaliza tusikubali kujenga nyufa ndani ya chama chetu, uchaguzi ukiisha lazima makundi yaishe,tuendelee kuimarisha chama na kujenga taifa," alisema.

## JK: Uongo unaigawa CCM

**Na Waandishi Wetu**

RAIS mstaafu, Jakaya Kikwete amesema tabia ya uongo ndio inayokigawa Chama Cha Mapinduzi (CCM) bila sababu na kuwatengenezea viongozi msongo wa mawazo badala ya kukusanya nguvu kukijenga.

Kikwete ambaye ni mwenyekiti mstaafu wa chama hicho alitoa kauli hiyo jana jijini hapa kwenye Mkutano Mkuu wa 10 wa CCM.

Alisema: "Mimi sina kura ila ni mzee maarufu ndani ya chama, kwanza ninaeleza imani hiyo na mimi ninaamini hivyo, Rais usisikilize porojo za watu kwamba kuna kijana gani atagombea na mzee gani atagombea, ni upuuzi mtupu.

"Sio kwamba nasema nawazuia lakini simwoni mwanaCCM mwaka 2025 atakayechukua fomu labda mambo yaharibike sana kati ya sasa na wakati huo, lakini siamini hivyo, si mila yetu lakini niseme ukweli tu hapa Tanzania leo kuna mwasiasa maarufu kumshinda Samia? Hayupo ndani ya chama hiki, hayupo nje ya chama hiki.

"Kwa hiyo, usibabaishwe na maneno wanaosema sijui waziri gani kaenda wapi kukusanya fedha, hao waganga njaa, tuliyapata sana maneno ya aina kama hayo kwa bwana fulani hivi alikuwa anajiita mwanaharakati huru, uongo mtupu.

"Nami nawaomba ndugu zangu achaneni na uongo, yaani katika kuelekea uchaguzi huu ukisema kwenye mitandao maneno ya ovyo ovyo lakini yote ni ya kutunga tu, fulani yuko hivi, fulani anaungwa mkono na mzee huyu, upuuzi mtupu.

"Tuache hii tabia, tabia hii inakigawa chama chetu bila sababu, mnawatengenezea viongozi wetu stresses (msongo wa mawazo) zisizo na msingi wowote kabisa, badala ya kukusanya nguzu zao kujenga chama na kutimiza majukumu yao ya kikatiba ya kuongoza taifa letu, wanaanza kuhangaikia upuuzi wenu, this is not fair (huu si uungwana)," alisema.

Alipendekeza mwanaCCM anayefanya hivyo, aitwe kwenye kamati ya maadili ili kuthibitisha tuhuma anazozielekeza dhidi ya viongozi na wanachama wengine.

"Chama chetu kikubwa sana, hakistahili kuvumilia upuuzi huu, mkiuvumilia chama hiki kitagawanyika kwa maslahi ya watu wapuuzi, kwa maslahi ya watu waongo wanaokaa kwenye mitandao," alisema Kikwete na kutahadharisha kuwa maneno ya aina hiyo yatakuwa mengi kuanzia sasa kueleka mwaka 2025.

"Wapo watakaosema 'haki ya Mungu wanakutana', kumbe kakutana yeye na mjinga mwenzake, tutawatia jakamoyo viongozi wetu bila sababu na dawa yake ni kukomesha uongo, sitaki kutoa mifano yaliyotusibu katika maisha yangu au tuliyopita katika mazingira hayo lakini katika kipindi changu sikutoa nafasi ya upuuzi," alisema.

Kuhusu uchaguzi wa Mwenyekiti, Kikwete alisema kupoteza kura moja au mbili, tatu kunathibitisha uchaguzi ulikuwa wa dhati kwa kuwa wakati mwingine asilimia 100 zinaleta shaka.

Katibu Mkuu mstaafu wa CCM, Yusuf Makamba aliwashambulia wanaCCM wanaomezea mate nafasi ya urais mwaka 2025, akisisitiza wajumbe wa Mkutano Mkuu kuweka maazimio kuwa Rais Samia Suluhu Hassan ndiye atakuwa mgombea pekee kwenye nafasi hiyo.

Mzee Makamba alisababisha washiriki wengi katika mkutano huo kuangua vicheko alipowahoji wanaokasirishwa na kauli ya 'mama anaupiga mwingi', akieleza kuwa hiyo ni nahau.

# Shule 7,000 zahitaji ukarabati mkubwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SHULE za msingi 7,000 kati ya 17,000 nchini zilizofanyiwa tathmini na serikali, zimebainika kuhitaji ukarabati mkubwa kutokana na uchakavu wa miundombinu uliopo.

Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Charles Msonde alibainisha hayo jana jijini hapa alipofunga mkutano wa mwaka wa tathmini ya maendeleo ya sekta ya elimu uliojumuisha wadau wa elimu na washirika wa maendeleo.

Alisema tathmini imeshafanyika katika shule zote zaidi ya 17,000 nchini, ikihusisha hali ya uchakavu wa shule kwa lengo kufahamu shule zote zinazohitaji kubomolewa na kujengwa upya, ukarabati mdogo na mkubwa.

"Kati ya hizo shule 17,000, shule 7,000 zinahitaji ukarabati mkubwa. Pia tumefanya tathmini kuangalia msongamano kwenye shule zetu na tumebaini kuna shule ambazo zina msongamano mkubwa sana wa wanafunzi," alisema.

Dk. Msonde pia alisema serikali imepanga katika mwaka 2022/23 kujenga shule mpya na madarasa zaidi ya 9,000 na kwa miaka ijayo wataendelea na mradi wa ujenzi wa shule mpya na ukarabati wa shule zilizopo.

Kuhusu msongamano, Dk. Msonde alisema kwa shule ambayo ina wanafunzi zaidi ya 1,500, itajengwa shule mpya ili wanafunzi wachepushwe ili kuweka mazingira mazuri ya kusomea.

"Katika mafanikio ya serikali ya kuendesha elimu bila ada kumekuwa na ongezeko kubwa la wanafunzi, kuna madarasa yamejaa sana, yapo madarasa yana wanafunzi 100, mengine 200 hadi 500 kwa darasa moja.

"Serikali inatambua miundombinu imekuwa dhaifu sana katika shule za msingi nchini na hapa wadau wa maendeleo wa elimu wametembelea katika baadhi ya shule hizo na walijionea shule za msingi kongwe nyingi zimechakaa na hali ya uchakavu ni kubwa," alisema.

Hata hivyo, bila kutaja idadi ya shule na mahali ziliko, Naibu Katibu huyo alisema wanafunzi wengine inabidi wakae nje kwa kuwa madarasa hayawezi kuwatosha.

Aliweka wazi mkakati wa serikali kupitia mradi wa Kuinua Ubora wa Elimu ya Awali na Msingi (BOOST) ulioanza kutekelezwa mwaka 2021/22 ukitarajiwa kufika ukomo 2025/26, kuwa utahakikisha unaondosha kero hizo.

"Mradi wa BOOST unatekelezwa kwa gharama ya Sh. bilioni 1.15 ikiwa ni mkopo nafuu wa Benki ya Dunia (WB)," alisema.

Vilevile, alisema serikali kupitia mradi wa kuboresha elimu ya sekondari (SEQUIP) ina mpango wa kujenga shule za sekondari 1,026 ambapo katika mwaka wa fedha uliopita, serikali ilijenga shule 232 na pia imetoa Sh. bilioni tatu ili kujenga shule za bweni za wasichana za mkoa kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita ambapo shule 10 zimeanza kujengwa.

Alisema kwa mwaka huu wa fedha serikali imepanga kujenga shule za sekondari 184 ikiwa ni shule moja katika kila halmashauri.

Mratibu wa Mtandao wa Elimu wa Tanzania (TENMET), Ochola Wayoga alishauri serikali kuongeza bajeti ya elimu hadi kufikia asilimia 20 ya bajeti yote ya serikali ili kusaidia mageuzi ya elimu yanayofanyika hivi sasa ikiwamo kuboresha ubora wa walimu.

Awali Naibu Katibu wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. James Mdoe aliwahakikisha wadau kuwa serikali imeweka milango wazi ya kupokea maoni ya kina katika kuboresha mapitio ya sera na mitaala.

Machi 31, 2017 Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesababu za Serikali (CAG) alitoa ripoti ya ukaguzi maalum kuhusu hali ya miundombinu na samani za shule za msingi nchini, akibainisha kuwa hali ni mbaya kwa shule zinazomilikiwa na serikali na kushauri hatua za haraka zichukuliwe kurekebisha dosari zilizobainika.

Hata hivyo, CAG katika ripoti yake ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo yake kuhusu ukaguzi maalum alioufanya mwaka 2017 iliyowasilishwa bungeni Aprili 12 mwaka huu, anaweka wazi kwamba serikali haijafanyia kazi hoja yake kuhusu uboreshaji wa miundombinu na samani za shule za msingi nchini.

# Assad kuteta na mwanasheria hukumu kuvuliwa cheo CAG

**Na Romana Mallya**



ALIYEKUWA Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad amesema kwa sasa hana cha kuzungumzia kuhusu hukumu iliyotolewa na Mahakama Kuu Masjala Kuu hadi pale atakapoongea na mwanasheria wake wiki hii.

Jumatatu mahakama hiyo ilitamka kwamba kuondolewa kwa Prof. Assad katika nafasi ya CAG kulifanyika kinyume cha Katiba.

Uamuzi huo ulitolewa jana mbele ya jopo la majaji watatu Jaji Juliana Masabo, Jaji Edwin Kakolaki na Jaji Dk. Benhaji Masoud kutokana na shauri la kikatiba lililofunguliwa Kiongozi wa Chama cha ACT Wazalendo, Zitto Kabwe kupinga kuondolewa kwa Prof. Assad madarakani.

Zitto aliwasilisha maombi dhidi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, CAG wa sasa, Charles Kichere na Prof. Assad aliyeondolewa madarakani Novemba 3, 2019.

Jana alipotafutwa na Nipashe kwa njia ya simu kuhusu hukumu hiyo, Prof. Assad alijibu kwa kifupi, akitamka: "Kwa sasa sina la kusema mpaka niongee na mwanasheria wangu. Nitaongea nao weekend (mwishoni mwa juma) hii, wiki ijayo labda nitakuwa na cha kusema".

Ikirejewa historia ya utendaji ya CAG Assad, aliwahi kuwa Profesa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kabla ya kuteuliwa kuwa 'bosi' wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) akiwa na umri wa miaka 58, ikiwa ni miaka saba kabla ya umri unaotajwa kikatiba wa kustaafu kwa CAG.

Desemba Mosi, 2014, Ikulu ilitangaza kuwa Rais wa wakati huo, Jakaya Kikwete alikuwa amemteua Prof. Assad kuwa CAG na uteuzi wake ulikuwa umeanza tangu Novemba 5 mwaka huo.

Prof. Assad alichukua nafasi ya mtangulizi wake, Ludovick Utouh aliyestaafu kwa mujibu wa Katiba.

Prof. Assad ni msomi, mwenye weledi, ujuzi na uzoefu mkubwa wa uhasibu na udhibiti wa fedha ambaye ana Shahada ya Uzamivu wa Uhasibu (PhD in Accounting) kutoka Chuo Kikuu cha Southampton, Uingereza mwaka 2001 na Shahada ya Uzamivu katika Udhibiti wa Fedha (MA in Financial Accounting) kutoka Chuo Kikuu cha Dublin City, Jamhuri ya Ireland, 1991.

# Wakili ajitoa kwenye kesi ya Paul Makonda

**Na Grace Gurisha**

WAKILI Kung'e Wabeha amejitoa kumwakilisha mahakamani mfanyabiashara Patrick Kamwelwe aliyemfungulia kesi ya madai ya gari aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda kwa madai kuwa ameshindwa kupata maelekezo sahihi kutoka kwa mteja wake.

Vilevile, Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu imekubali kusikiliza kesi hiyo upande mmoja wa Makonda na William Malecela baada ya Kamwelwe kushindwa kuwasilisha mahakamani hapo kiapo kinzani kwa wakati.

Wakili Wabeha alidai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Richard Kabate baada ya Wakili wa Makonda, Gift Joshua kuiomba mahakama itoe amri stahiki kwa sababu hawajapata kiapo kinzani (majibu ya hoja zao) kutoka kwa Kamwelwe.

Baada ya Joshua kudai hayo, Wakili Wabeha alidai kuwa Novemba 3 mwaka huu, walipata maombi hayo mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Ramadhani Rugemalira na walipewa siku 14 wajibu.

"Lakini tumeshindwa kwa sababu tumekosa maelekezo sahihi kutoka kwa mteja wetu na tumekuwa tukiwasiliana naye, lakini hatujapata majibu kwa wakati, kwa hiyo kutokana na hilo ninaomba kujitoa," alidai Wabeha.

Wakili Joshua alidai kwa sababu maelekezo ni muhimu, hawapingi hilo na kwa kuwa muda wa kuleta majibu kinzani umeisha, wanaomba maombi yaliyoletwa na Kamwelwe yasikilizwe upande mmoja kutokana na muda wa kujibu kiapo hicho kuisha. Hakimu Kabate baada ya kusikiliza hoja hizo, alikubali Wabeha kujitoa na pia amekubali kesi hiyo ya madai isikilizwe upande mmoja kama alivyoomba mjibu maombi.

Hata hivyo, Makonda na Malecela kupitia Wakili wao, Joshua, waliwasilisha maombi mahakamani Kamwelwe aweke dhamana ya kesi yake ili ikitokea wameshinda iwe rahisi kulipwa gharama za uendeshaji wa kesi hiyo kirahisi.

Maombi hayo hutolewa ikitokea mdai si raia wa Tanzania au hana mali isiyohamishika nchini.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Januari 31 mwakani mahakama itakaposikiliza madai ya msingi ya upande mmoja, pia itasikiliza maombi ya kutaka Kamwelwe aweke dhamana ya kesi hiyo na pia itaangalia kama mdai amepata wakili.

Kamwelwe anayeishi jijini New York, Marekani, amefungua kesi ya madai namba 234/2022 dhidi ya Makonda na Malecela, maarufu kama Le Mutuz, akiwataka wamlipe fidia ya Sh. milioni 247.2 kwa madai kuwa wamemdhulumu gari lake aina ya Range Rover Sport.

Kamwelwe anaiomba mahakama imwamuru Makonda na Malecela kumlipa kiasi hicho cha fedha kama fidia anayodai kuwa imetokana na hatua ya wadaiwa hao kumdhulumu gari lake jeusi aina ya Toyota Rand Rover/Range Rover Ronge Sport lenye namba 20153.

Mdai huyo (Kamwelwe) katika hati yake ya madai, anataka Makonda na Malecela walimpe dola za Marekani 11,250 kama gharama ya kodi ya kuliingiza gari hilo, dola za Marekani 50,000 kama fidia ya kulichukua gari hilo pamoja na dola 45,000 ambayo ni thamani ya gari hilo.

Kamwelwe pia anadai Makonda ameendelea kulitumia gari hilo hata baada ya kuondolewa madarakani licha ya kwamba si mali yake halali.

Katika hati yake ya madai, Kamwelwe anadai mwaka 2017 alifuatwa na William Malecela, maarufu Le Mutuz, na kumweleza kuwa Makonda anaomba amwazime gari aina ya Range Rover.


Victoria FINANCE

Victoria Finance Plc
5th Floor, Sky Tower Building-Kijitonyama
New Bagamoyo Road
P.O.Box 12102, Dar es Salaam - Tanzania

Telephone +255 22 277 4577
Fax: +255 22 277 4559
Email: info@victoriafinance.co.tz
Website: www.victoriafinance.co.tz

**TANGAZO LA MINADA YA HADHARA**

VICTORIA FINANCE PLC INAPENDA KUUTANGAZIA UMMA WA WATANZANIA YA KWAMBA KWA IDHINI ITAKAYOTOA KWA KAMPUNI TOFAUTI ZA UDALALI INATARAJIA KUUZA KWA MNADA WA HADHARA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU KAMA IFUATAVYO;

| NA | JINA LA MWENYE DHAMANA | DHAMANA | AINA NA SEHEMU YA DHAMANA | DALALI | TAREHE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MWAMINI MISSOKI | NYUMBA | HATI MILIKI – SINZA | KISAONI AUCTION MART TANZANIA LTD | 23-12-2022 |
| 2 | CHRISTOPHER UHAGILE | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO- IHANGA | HOLLYNESS AND RESPISHERS CO LTD | 23-12-2022 |
| 3 | FRANSISCA FRANCE LEMNG'E | NYUMBA | HATI MILIKI – MALAMBA MAWILI | JODAC PROFESSIONALS LTD | 23-12-2022 |
| 4 | PROPERTY MARKET CONSULT LTD | GARI | FAW T 589 BDL | JODAC PROFESSIONALS LTD | 23-12-2022 |

Minada yote itafanyika mahali husika katika muda na siku ambayo itatangazwa kupitia katika vipeperushi na magari ya matangazo kutokana na idhini itayotoka kutoka katika ofisi za wakuu wa wilaya wanaohusika.

**MASHARTI YA MNADA;**

- Asilimia 25% ya bei iliyofikia italipwa papo hapo na asilimia 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne. (14). Kwa kushindwa kufanya hivyo itapelekea mnada kurudiwa tena na pesa zilizolipwa kutokurudishwa.
- Gharama za kumuhamisha mmiliki na kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.
- Dhamana itauzwa Kama ilivyo.

# Silicosis: ugonjwa wa mfumo wa hewa usiotibika unawaoumiza wachimbaji

## •Ishara ya kutisha imetawala Mirerani

Na Mary Mosha, aliyekuwa MIRERANI

NI majira ya saa nane mchana, kwenye eneo tengefu la migodi ya Mirerani, maarufu Geti la Magufuli, wilayani Simanjiro mkoani Manyara, anaonekana kijana Nelson Laizer akiwa amelala pembeni mwa kifusi cha mchanga huku akiwa na dalili zote za kuwa mgonjwa.

Ni eneo lenye ukubwa wa takribani kilomita za mraba 24 lenye sifa ya kuwa na vumbi litokanalo na shughuli za uchimbaji madini.

"Ukiona mwanamume analia, ujue kazidiwa! Nimechimba kwa miaka 15 bila mafanikio, badala yake nimeambulia ugonjwa huu. Ninachokisubiri kwa sasa ni siku yangu ya kufa maana ugonjwa huu hauna tiba," analalamika Laizer huku akitiririkwa machozi.

Mchimbaji huyo anaiambia Nipashe kuwa ni miongoni mwa wachimbaji madini ya Tanzanite walioathiriwa na ugonjwa wa mapafu, ambao kitabibu unaitwa 'silicosis', ukisababishwa na vumbi wakati wa uchimbaji madini.

Hata hivyo, wakati Nipashe inaendelea na mahojiano na Laizer (40) mwezi uliopita, kijana huyo alipoteza fahamu. Wachimbaji wenzake walimbeba na kumpeleka eneo maalum la mapokezi kuliko na usafiri wa kumwezesha kupelekwa hospitalini.

Mchimbaji Sabastian Mgosi (37) anaendeleza mazungumzo ya Nipashe na Laizer, akijitambulisha ni miongoni mwa wachimbaji kwenye Kitalu B, akiwa na uzoefu wa miaka 23 mgodini.

Mgosi anasema wachimbaji wengi wanapata maradhi ya mapafu, hasa kifua kikuu (TB) na silicosis kutokana na vumbi wakati wa kuchoronga miamba migodini.

"Vijana tulio wengi hapa ni wa umri wa kati ya miaka 14 na 45, tunatatufa maisha kwa kuchimba madini ya Tanzanite lakini tunakabiliwa na matatizo mengi.

"Hatuna vifaa vya kujikinga na vumbi, migodi kutonyunyuziwa maji wakati wa kuchoronga miamba, idadi kubwa ya watu hapa mgodini na ukosefu wa hewa safi. Haya kwa kiwango kikubwa ndiyo kiini cha magonjwa tunayokabiliana nayo hapa migodini," analalamika.

Hassan Mushi (33) anayejitambulisha kuwa na uzoefu wa miaka 17 migodini Mirerani, anasema maisha ya wachimbaji yapo hatarani licha ya sekta hiyo kuingiza pato kubwa kwa taifa.



Baadhi ya wachimbaji wadogo wa Tanzanite kwenye migodi ya Mirerani. **PICHA: MAKTABA**

"Wapo wachimbaji wenzetu wana magonjwa yanayotisha, wanapumulia mashine kwa zaidi ya miaka mitatu sasa," Mushi anabainisha.

**HATARI ILIPO**

Mchimbaji Mushi anaeleza uzoefu wake karibu miongo miwili mgodini kwamba ili ubaini eneo lina madini, utaanza kuona sabuni kisha unaona mikanda iliyosimama kwenye hiyo miamba na baadaye utaona mistari yenye rangi nyeusi ikikuelekeza madini yalipo.

"Kisha utaona karandamu, haya ni madini yenye rangi ya bluu ila hayana thamani. Ukishayavuka utakumbana na krista ambayo ni madini ya kutengeneza penseli, kisha utakutana na miamba iliyojipanga kama sabuni ambayo inakuelekeza kwenye kuipata Tanzanite.

"Ni katika hatua hii ndipo wachimbaji huchimba kwa fujo bila tahadhari wakitegemea kupata Tanzanite. Wachimbaji wanapoanza kuona madini ya penseli na sabuni huwa hawakumbuki kuvaa barakoa hata kama wamepewa.

"Wamiliki nao husahau kumwaga maji kabla ya kuanza kuchimba ili kuondoa vumbi, kila mmoja huwa anawaza kuibua mali," anafafanua Mushi.

**HOSPITALINI**

Mkurugenzi wa Hospitali Maalum ya Magonjwa Ambukizi, maarufu Kibong'oto, Dk. Leonard Subi anafafanua kuwa ugonjwa wa silcosis unampata mchimbaji kwa kuvuta vumbi ambalo hutoka wakati wa ulipuaji wa miamba ardhini.

Dk. Subi anatoa ufafanuzi zaidi wa kitabibu, akitamka: "Vumbi hilo linalotokana na madini ya silca, husababisha matatizo ya silicosis. Vumbi likiingia kwenye mapafu, huathiri uingizwaji wa hewa safi ya Oksijeni kwenye mapafu kwani linapoingia hukaa sehemu na kuwa kovu.

"Kukishakuwa na kovu hilo, uvutaji wa hewa huwa wa shida kwa mchimbaji, hivyo mtu anapopatwa hulazimika kuongezwa hewa safi ya Oksijeni.

"Ugonjwa wa silicosis hauna tiba ya moja kwa moja na mgonjwa anaweza kukaa mwezi mmoja hadi miaka mitatu wakati anaendelea kupata hewa tiba (Oksijeni) pamoja na dawa za maumivu.

"Inategemeana na jinsi mgonjwa alivyoathirika. Mgonjwa anaweza kutumia mtungi mmoja kwa saa 24, ingawa wakati mwingine anaweza kupewa nyakati za usiku au mchana tu au pale tu anapozidiwa."

Mkurugenzi huyo anabainisha kuwa kwa sasa Hospitali ya Kibong'oto inatumia mitungi 20 hadi 24 kwa siku kutoa huduma kwa wagonjwa wa silicosis.

Anasema kuwa kutokana na wachimbaji hao kuwa na hali mbaya kiuchumi, serikali inawapatia wagonjwa mahitaji yote, ikiwamo chakula.

"Ikumbuke kuwa hawa ni vijana wenye umri wa kati ya miaka 15 na 45, ni watafutaji wa maisha, bado tunapaswa kuwasaidia.

"Tumekuwa tukipita kwenye migodi kuwakumbusha wachimbaji na waajiri kuchukua tahadhari zote, kuhakikisha kiwango cha kuwapo silca kwenye vumbi kinachokubalika kimataifa cha miligramu 0.05 kinazingatiwa.

"Hata hivyo, utafiti ambao umefanywa kwenye migodi 22 ya Mirerani, umeonyesha kiwango cha silca kwenye vumbi linalovutwa na wachimbaji kilikuwa ni miligramu 1.227, kiwango ambacho ni zaidi ya mara 25 ya kiwango kinachokubalika kimataifa cha miligramu 0.05," anabainisha.

Katika kudadisi maendeleo ya kiafya ya kijana Laizer hospitalini huko, Dk. Subi anatoa ufafanuzi kwa Nipashe kwamba serikali inagharamia matibabu yake na wagonjwa wengine wa aina hiyo, akibainisha kuwa wengi wao wametelekezwa na ndugu zao.

**WAMILIKI MIGODI**

Sadiki Mnene, mmoja wa wamiliki wa migodi aliyewahi kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji Madini Mirerani na mchimbaji tangu mwaka 1985, anakiri mmoja wa wafanyakazi kuugua silcosis na kwamba wanaougua TB ni wengi.

"Hao wanaougua kifua kikuu hawahesabiki. Suluhisho ni kujikinga kwa kuvaa barakoa na kunyunyuzia maji kwenye migodi wakati wa kuchoronga ili kupunguza vumbi. Pia kunahitajika mtambo mkubwa wa kukusanya vumbi. Mimi mwenyewe huwa ninaingia huko, nikikukuta hujavaa barakoa na hujajikinga sikuvumilii," anasema.

Anasema ugonjwa wa silicosis unaambukizwa wakati wa kuchoronga na kutoboa miamba kwa kutumia kifaa wanachokiita 'diga' (Rock Drill), akibainisha kuwa kinapofanya kazi, hutoka vipande vidogo vya madini yanayoitwa silca ambavyo vinafanana na vipande vidogo vya bati.

"Vipande hivi hunata kwenye mapafu na kutokana na wingi wake, hufanya mapafu kusinyaa na mapafu yanaposinyaa, mtu anapata matatizo ya kupata hewa safi na kushindwa kupumua.

"Tunahamasisha wasimamizi na wamiliki wa migodi kutumia mashine za kuchoronga zinazotumia maji na si zinazotimua vumbi. Pia tunahamasishana kutumia mashine za kunyonya vumbi kwenye migodi kabla na baada ya kulipua baruti.

"Wachimbaji tunawahimiza kuvaa barakoa wanapozama kwenye migodi ili ziwasaidie wasivute vumbi," anasema Mnene akiwa na angalizo kuwa licha ya jitihada zao hizo, kuna wachimbaji vijana hupuuza na kuingia migodini bila kinga.

Mnene anashauri serikali ifanye ukaguzi wa mara kwa mara kwenye migodi ikiwa ni pamoja na kupima afya za wachimbaji na kuchukua hatua stahiki kwa wasiofuata sheria.

Moses Nkya, mmiliki wa mgodi, anakiri gharama za matibabu kwa waathirika wa shughuli za uchimbaji migodoni zinapaswa kubebwa na mmiliki wa mgodi ingawa wakati mwingine hushindikana kutokana na hali ya maisha na ubinafsi.

"Ikumbukwe ugonjwa huu (silicosis) hauna dawa. Unapaswa kumhudumia mgonjwa huyo mpaka kifo chake. Changamoto ni kwamba unaweza kuchimba kwa miaka 10 hadi 15 na usipate kitu. Hivyo, ni ngumu kuwapa msaada wachimbaji kiasi kwamba baadhi huwakimbia wachimbaji wao wanapoathirika.

"Hakuna mmiliki anayemchukia mchimbaji. Tunafanya kulingana na kile tulichozalisha, kama haujazalisha utamtibu kwa kutumia nini? Serikali isitunyooshee kidole badala yake tusaidiane.

"Tumesikia inakuja bima ya afya kwa wote, hii itatusaidia kupunguza lawama kwa wamiliki. Ni vyema kuwapo utaratibu maalum wa kupata bima ili kuleta matokeo chanya kwa wachimbaji wenyewe na familia zao," anashauri Nkya.

**MAKAMU WA RAIS**

Hivi karibuni Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango alizuru mkoani Manyara na kuiagiza Wizara ya Madini kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Afya kufuatilia uzingatiwaji wa sheria na kanuni za afya na usalama mahali pa kazi migodini.

Dk. Mpango aliagiza kuchukuliwa hatua za haraka kudhibiti tatizo la silcosis linalowakumba wachimbaji wa Mirerani.

Alibainisha kuwapo wastani wa wagonjwa 25 kwenye Hospitali ya Kibong'oto, wengi wao wakiwa ni vijana wenye umri wa kati ya miaka 20 na 40 ambao wameathiriwa na vumbi la migodini.

"Wagonjwa hawa wanatumia takriban mitungi 30 ya hewa tiba ya Oksijeni kwa siku na kuigharimu serikali zaidi ya Sh. 500 milioni kwa mwaka kwa Hospitali ya Kibong'oto peke yake, huku baadhi ya wagonjwa wakiwa wamelazwa kwa zaidi ya miaka miwili wakipumulia mashine.

"Vumbi ni kichocheo kikubwa cha maambukizi ya ugonjwa wa kifua kikuu ambao ni tishio kwa taifa. Utafiti uliofanywa kwa wachimbaji 330 katika migodi ya Mirerani mwaka 2021, unaonesha wachimbaji 99 sawa na asilimia 30 walikuwa wameathirika na ugonjwa wa silicosis huku wachimbaji wengine 20 sawa na asilimia 6.1 wakiwa na kifua kikuu. Hii ni mara 24 zaidi ya wastani wa kitaifa," alibainisha Dk. Mpango.

Eneo la migodi ya Mirerani linakadiriwa kuwa na wachimbaji wadogo zaidi ya 800 kwenye machimbo yapatayo 400 wakati wilaya nzima ya Simanjiro ina migodi 2,000.

HABARI KITAIFA

# Makamba aridhishwa maandalizi mradi wa kuchakata gesi Lindi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nishati, January Makamba, amesema ameridhishwa na maandalizi ya uwekezaji wa mradi wa kuchakata na kusindika gesi asilia (LNG), kwa makubaliano kufikiwa katika mambo yote ya msingi.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma, iliyotolewa na Wizara ya Nishati, Makamba amekutana na kufanya mazungumzo na Makamu wa Rais wa Kampuni ya Mafuta na Gesi ya Equinor ya Norway, Nina Koch, ambao walizungumzia maandalizi ya uwekezaji wa mradi wa kuchakata na kusindika gesi asilia (LNG).

Taarifa hiyo ilisema kwa sasa timu za majadiliano za upande wa serikali na wawekezaji zipo katika hatua ya uandishi (drafting) ya mikataba ya mwisho (final agreements) baada ya makubaliano kufikiwa katika mambo yote ya msingi mwezi Novemba mwaka jana.

Aidha, Waziri Makamba alieleza kuridhishwa na hatua iliyofikiwa na kusisitiza kuwa anatarajia kuona mradi huu ukitekelezwa kwa wakati kama ilivyopangwa, ili kuhakikisha utatekelezwa kwa ufanisi mkubwa.

Koch alisisitiza kuwa Equinor ipo tayari kutoa ushirikiano katika uanzishaji wa Ofisi Maalum ya Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi asilia (LNG Project Office) ambayo itasimamia na kuratibu shughuli za mradi katika kipindi cha ujenzi na uendeshaji.

Aliongeza kuwa mradi huu ni muhimu na umepokelewa kwa mtazamo chanya nchini Norway: "Kwa uzoefu wangu miradi kama hii, sio rahisi kukubalika moja kwa moja na pande zote yaani kampuni na uongozi wa nchi. Lakini kwa mradi huu, uongozi wa kisiasa na wananchi wote wa Norway wanauunga mkono."

Katika ziara yake nchini, Koch alitembelea eneo utakapojengwa mradi huo wa kuchakata na kusindika gesi asilia (LNG) mkoani Lindi, pia aliipongeza serikali kwa kuchagua eneo la mradi karibu na kiwanja cha ndege, jambo ambalo litarahisisha usafiri wa wafanyakazi na vifaa mbalimbali wakati wa ujenzi na uendeshaji wa mradi.

Pia Koch alitembelea Chuo cha VETA Lindi ambacho kampuni zinazotarajiwa kuwekeza katika mradi wa LNG, zimekuwa zikitoa ufadhili wa vifaa vya kujifunzia na kumwekeza waziri huyo kuwa lengo la Kampuni ya Equinor ni kuendelea na kuvifadhili vyuo mbalimbali hasa vya mikoa ya Lindi na Mtwara ili kuwajengea uwezo kwa Watanzania waweze kushiriki kikamilifu katika ujenzi na uendeshaji wa mradi wa huo wenye thamani ya zaidi ya Sh. trilioni 70. Katika kikao hicho Waziri Makamba aliambatana na Kamishna wa Mafuta na Gesi wa Wizara ya Nishati, Mike Mjinja pamoja na Charles Sangweni Mkurugenzi Mkuu wa PURA.

Koch aliongozana na Nizar Damree, Mkuu wa Kitengo cha Mkondo wa Juu Kimataifa, Unni Fjær Makamu wa Rais na Mkurugenzi Mkuu wa Equnor Tanzania pamoja na Genevieve Kasanga, Ofisa Mawasiliano Equinor Tanzania.

# Mfanyabiashara kizimbani mashtaka dawa za kulevya

**Na Grace Gurisha**

MFANYABIASHARA maarufu Mohamed Abdallah 'Chonji' na wenzake wanne wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam kwa tuhuma za kusafirisha dawa za kulevya aina ya heroine na Cocaine gramu 6,203.85.

Mbali na Chonji, washtakiwa wengine ni Mkazi wa Kimara, Abdul Chumbi, Rehani Umande ambaye ni mkazi wa Magomeni Kondoa, Tanala Mwakosagule anayeishi Magomeni Makanya na Maliki Maunda, mkazi wa Magomeni Kagera mkoani Dar es Salaam.

Akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali Yusuph Aboud akisaidiana na Tumaini Mafulu, alidai jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Mary Mario kuwa washtakiwa wanatuhumiwa kwa makosa mawili ya kusafirisha dawa za kulevya.

Aboud alidai kuwa Oktoba 21, 2014 eneo la Magomeni Makanya, Kinondoni mkoani Dar es Salaam washtakiwa walikutwa wakisafirisha gramu 5309.57 za dawa za kulevya aina ya Heroine Hydrochloridec zenye thamani ya Sh. 265,478,500.

Katika shtaka la pili, ilidaiwa kuwa katika tarehe na eneo hilo, washtakiwa hao walikutwa wakisafirisha gramu 894.28 za dawa za kulevya aina Cocaine Hydrochloride zenye thamani ya Sh. 62,599,6000.

Baada ya kusomwa mashtaka hayo, hakimu aliwataka washtakiwa kutokujibu chochote kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo. Upande wa mashtaka ulidai upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na kesi iliahirishwa hadi Desemba 21, 2022 kwa ajili ya kutajwa ambapo upande wa mashtaka upo katika hatua ya kuwasilisha jalada la kesi hiyo Mahakama Kuu.


## NOTISI/TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,YONO AUCTION MART &CO.LTD ,YARDLEY RECOVERIES AUCTION LTD, SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya Benki ya AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| UBUNGO | SAIDI AKILIMALI KALILWA | NYUMBA | SAIDI AKILIMALI KALILWA | MWASONGA KIGAMBONI | 23/12/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KARIAKOO | ABOUBAKER O. HASSAN AND OR SAINECHA | KIWANJA HATI NAMBA 113599 KITALU 'G' TEGETA NA KIWANJA HATI NAMBA 105871 KITALU '12' KIBADA | ABOUBAKER O. HASSAN | TEGETA NA KIBADA | 23/12/2022 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | JAMILA KONDO GEMA | NYUMBA | JAMILA KONDO GEMA | KIPAWA-KIPUNGUNI | 16/12/2022 (MARUDIO) SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | HNP AND GENERAL SUPPLY LIMITED | NYUMBA | HELLY PETER NYONI | KIGAMBONI DEGE | 23/12/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MAIN | ESTER JEREMIA FOKAS | NYUMBA | ESTER JEREMIA FOKAS | YANGEYANGE MSONGOLA | 27/12/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MAIN | BETHUEL NAFTAL | NYUMBA | BETHUEL NAFTAL | HONDOGO KIBAMBA | 23/12/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | ATHUMANI HASSANI HEMEDI | NYUMBA | ATHUMANI HASSANI HEMEDI | ULONGONI 'B' | 27/12/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | MLIMO COMPANY LIMITED | NYUMBA | TIMOTH ANISETH KATWELA | KIMARA SARANGA | 23/12/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | GERALD LATYANDUMI KIMARO | NYUMBA | GERALD LATYANDUMI KIMARO | KIMARA | 23/12/2022 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | EMANUEL DANIEL SORORWA | NYUMBA | FRANK THOMAS KIVUYO | KITONGOJI CHA ILKIUSHIN KATA YA OLTURUMET ARUSHA | 23/12/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | ISIMBULA MAULID RAJAB | KIWANJA | ISIMBULA MAULID RAJAB | MURIET ARUSHA | 27/12/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | ELSON YALEDI ENOSI | NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NA.730 KITALU 'E' HATI NA.66242 | ELSON YALEDI ENOSI | BUHONGWA-MWANZA | 23/12/2022 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | NOZAWA G DAVID T/A BUSWELU SATELITE CABLE NETWORK | NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NA.306 KITALU 'C' HATI NA.91380 | KATONGOLE DASTAN KAKINDA | EAST BUSWELU-MWANZA | 23/12/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | GRACE ADONIAS MTEGO | NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NA.22 KITALU 'N' HATI NA.4870 | BLASIUS SWAI KAGINA | BUNDA | 27/12/2022 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | FAUSTIN JOSEPH MWACHA | NYUMBA | FAUSTIN JOSEPH MWACHA | GOBA MATOSA | 20/12/2022 (MARUDIO) SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | GODLISTEN ELINASAA KILEO | NYUMBA | GODLISTEN ELINASAA KILEO | MONGOLA NDEGE | 23/12/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | FESTO OBEDI SANGA | NYUMBA | FESTO OBEDI SANGA | MAPUTO-MBWENI | 27/12/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja, au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie namba **0762260787/0718038313/0712667989/0655715138/0754376493/0679441960**
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.

217187102

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hongera kusherehekea miaka 61 ya Uhuru

**LEO** ni siku muhimu sana wakati Tanganyika kabla ya kuungana na Zanzibar na kuwa Tanzania ikisherehekea miaka 61 ya Uhuru.

Miaka 61 ya Uhuru kuna mambo mengi yamefanyika na kumekuwapo na mabadiliko makubwa.

Kumekuwa na maendeleo makubwa katika sekta ya miundombinu ya barabara mpaka majengo. Kwa waliofanikiwa kuwapo tangu nchi haijapata Uhuru, wana mengi ya kueleza kwa sababu walishuhudia nchi ilipotoka mpaka ilipofikia na inakoendelea.

Tukizungumzia miundombinu ya barabara, kila mtu anaona jinsi nchi sasa ilivyounganishwa kutoka mkoa mmoja kwenda mwingine.

Hapo mwanzo kwenda baadhi ya mikoa watu walikuwa wakisafiri kwa siku mbili hadi tatu kufika mkoa mwingine kutokana na hali mbaya ya barabara.

Lakini kwa sasa, mtu anaweza kusafiri kwa gari ndogo kutoka mkoa mmoja kwenda mwingine na kufika siku hiyo hiyo na akitaka anaweza kugeuza na kurudi mkoani kwake.

Haya ni mafanikio makubwa ya kujivunia wakati wa kuadhimisha miaka 61 ya Uhuru. Kwa upande wa majengo, tumeshuhudia shule nyingi kuanzia za msingi, sekondari hadi vyuo zikiongezeka na idadi ya Watanzania wenye elimu ikizidi kuongezeka.

Majengo ya hospitali, vituo vya afya na zahanati pia yameongezeka kila mkoa na kufanya idadi ya Watanzania wanaokwenda kupata huduma ya afya kwenye vituo hivyo iongezeke na kuokoa vifo vilivyokuwa vikitokana na watu kushindwa kupata huduma hiyo kwa kukosekana hospitali na vituo vya afya.

Watanzania wengi wameondokana na ujinga kwa sababu sasa wanapata elimu kupitia shule nyingi zilizoongezeka na kutoa fursa kwa watu wengi kujiandikisha shuleni na vile vile kujua umuhimu wa kupata huduma sahihi ya tiba kwa kwenda hospitali au kwenye vituo vya afya.

Haya ni mafaniko makubwa ya kujivunia na Watanzania hawana budi kujivunia hapa walipofikia.

Kwa sasa huduma ya nishati ya umeme imesambaa katika vijiji vingi tofauti na miaka ya nyuma hali iliyoleta maendeleo makubwa ya watu kujitengenezea ajira zikiwamo za kufungua mashine za kusaga na kukoboa, viwanda vidogo vya uzalishaji kama ukamuaji mafuta ya kula, saluni za wanawake na wanaume na pia baadhi wamefungua sehemu za kusaidia wananchi wenzao kuchaji simu, ambao hawajawa na uwezo wa kuunganisha nishati hiyo.


Hayati Rais John Magufuli, yeye alikuja na staili ya kufuta sherehe za Uhuru kwa kuagiza fedha ambazo zingetumika kwenye sherehe hiyo, zipelekwe kwa ujenzi wa shughuli za maendeleo ambapo Barabara kutoka makutano ya Mwenge hadi Morocco, jijini Dar es Salaam, ilijengwa na kubadili kabisa sura ya barabara hiyo.

Na katika maadhimisho ya mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan, ameagiza sherehe hizo za miaka 61 ya Uhuru kufutwa na fedha hizo Sh. milioni 960 zielekezwe kwenye ujenzi wa mabweni katika shule nane za wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Uamuzi huo ni hatua kubwa ya kuleta maendeleo hasa katika sekta ya elimu kutokana na adha wanazopata wanafunzi hao kutokana na kukosekana kwa mabweni yatakayowasaidia kuishi shuleni na kuepuka adha ya kutembea umbali mrefu na kukutana na vikwazo vya kuwakosesha elimu.

Hatua ya Rais Samia ni ya kupongezwa na bila shaka nchi itashuhudia maendeleo makubwa zaidi katika kuhakikisha kila mwananchi anafaidika na maendeleo hayo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Halfani Chusi

## Muungwana Lazima Nilonge

# Hili wazo la Ndumbaro liungwe mkono

**HILI** likifanikiwa kwa asilimia 100, ukatili wa kijinsia utakuwa umepata suluhu. Ni siku chache zilizopita, Waziri wa Katiba na Sheria, Dk Damas Ndumbaro, alitoa rai kwa wanasheria nchini kuunga mkono juhudi za serikali kupambana na unyanyasaji kijinsia na ukatili dhidi ya watoto.

Ndumbaro alitoa rai hiyo, akiwa mkoani Dar es Salaam katika Maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia kwa wanawake na Watoto. Maadhimisho hayo yalihudhuriwa na wadau mbalimbali, wakiwamo wanafunzi kutoka Chuo cha Sheria, wasanii pamoja na wawakilishi kutoka asasi za kiraia.

Hayo ni maono yanayobeba sura ya kuunga mkono juhudi za Rais Dk Samia, katika kuhakikisha suala la ukatili Tanzania linakuwa historia.

Nilimsikia kiongozi huyo akisema, ili kuishinda vita dhidi ya ukatili uliokithiri, wanasheria, serikali na wadau wa maendeleo hawana budi kuungana na kuwa kitu kimoja.

"Tuna siku 16 za kupinga ukatili, ukiziangalia unaona ni chache sana, lakini ukizitumia vizuri ni nyingi sana katika kutoa elimu na kusaidia jamii, kujiepusha na vitendo vya ukatili wa kijinsia," anasema.

Safari hii ilianza mwaka 1991 kule nchini Marekani, ambako wanawake wa viongozi wakubwa waliungana mpaka kufikia hii leo jumla ya nchi 187 zimeungana na kati yake, Tanzania ni miongoni," anasema Dk. Ndumbaro na kuongeza kuwa

Hivi karibuni, mlishuhudia Waziri wa Fedha na Mipango Dk. Mwigulu Nchemba alikwenda nchini Ujerumani, kutia saini mkataba na serikali. Kati ya mambo yaliyopo katika mkataba huo ni mradi wa ushirikiano katika kupinga ukatili wa kijinsia.

Alisema mradi huo uliotiwa saini na Wajerumani, utajikita zaidi kupinga, kutatua vikwazo na kutoa mafunzo kwa wadau wa maendeleo juu ya athari za ukatili wa kijinsia, kwa watoto na wanawake.

Lengo la mradi huo, ndio agenda ya hizi Siku 16 za kupinga ukatili, tunataka kutekeleza kwa miaka mitatu ijayo tutatoa mafunzo kwa wataalamu, asasi, polisi, TAKUKURU na mhimili wa mahakama, ili waweze kulitambua kwa kina tuweze kuwa kitu kimoja katika kupambana na janga hili.

Elimu itajikita zaidi katika kutambua viashiria vya ukatili wa kijinsia, kwa sababu wapo wengine wanafanya ukatili lakini hawajui, lakini kwa sasa hadi wanaume wanafanyiwa hayo na ndio maana tafiti zinasema wanaume wanakufa mapema kuliko wanawake, kwa sababu wapo wanaume wanaonyanyaswa na kukatiliwa.

Akasema, kwa sasa wana mpango wa kuanziasha usajili wa kimtandao, ikikagua hali ya unyanyasaji na kuweka kwenye mfumo na hiyo itakuwa inaangalia wanapoenda kuomba ajira na kama waliwahi kufanya ukatili.

Pia, mtu akienda benki kuomba mkopo, anaangaliwa akikutwa na hatia hapewi mkopo hii ndio maana halisi ya kutumia teknolojia kupambana na ukatili.

Wajibu namba moja wa serikali sasa ni kuhakikisha sera, kanuni na miongozo inakuwa rafiki na jumuishi ili kuhakikisha tunaondoa kadhia hii.

Naibu Waziri Maendeleo ya Jamii Jinsia Wanawake na Makundi Maalumu, Mwanaidi Khamisi, anasema katika kupambana na ukatili huo, anaungana na mtangulizi wake Dk. Ndumbaro, akiongea kwa niaba ya waziri mwenye dhamana hiyo na Dk. Dorothy Gwajima.

"Kaulimbiu ya mwaka huu inasema kila uhai una thamani tokomeza mauaji na ukatili dhidi ya watoto kwa hiyo serikali inaendelea na kampeni ya kupinga ukatili kupitia Shujaa wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii SUMAUJATA, tangu ilipozinduliwa watu wengi wamejiunga na kampeni hii kushirikiana na serikali katika kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Wizara hii inaendelea kufanya mambo mengi katika kutokomeza vitendo vya ukatili ikiwamo kutekeleza mpango kazi wa kitaifa wa kutokomeza ukatili kwa wanawake na watototo.

Hali kadhalika, kuna suala la kuongeza madawati ya jinsia kwenye vituo vya polisi, kuanzishwa vituo vya mkono kwa mkono vinavyotoa huduma na kuanzisha madawati 22 katika vyuo vya elimu ya juu.

**Simu: 0787879707.**

# JICA yaahidi kusaidia miradi ya maendeleo

**Na Mary Geofrey**

SHIRIKA la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA), limeadhimisha miaka 60 ya ushirikiano wake na serikali kwa kuahidi kuendelea kusaidia kutekeleza miradi mbalimbali ya kijamii na kiuchumi.

Mwakilishi Mkuu wa JICA nchini, Naofumi Yamamura, alitoa ahadi hiyo juzi Jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi katika semina na ziara ya kutembelea baadhi ya miradi waliyoifadhili.

Baadhi ya miradi hiyo ni kituo cha kupooza umeme kilichoko katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) na mradi wa daraja la juu TAZARA la Mfugale.

Alisema uhusiano baina ya nchi hizo ulianza 1962 baada ya uhuru wa Tanganyika na wataendelea kushiriki na kufadhili miradi mingine Tanzania Bara na Visiwani Zanzibar.

"Kwa manufaa ya nchi hizi mbili na Watanzania 22,064 wamenufaika na programu za mafunzo zilizodhaminiwa na serikali ya Japan huku Wajapan 1,679 wakiwa wameshiriki programu hizo za mafunzo na kunufaika na mambo mengi kutoka Tanzania ikiwamo utamaduni na lugha ya Kiswahili," alisema.

Aidha, alisema ushirikiano huo ulidumu kwa miaka 60 na kutekeleza miradi mbalimbali Tanzania ukiwamo mradi wa ujenzi wa daraja la Salender 1980 ambao utaendelea kudumu kwa manufaa ya Watanzania.

Mwakilishi Mwandamizi wa (JICA,) Watanabe Hideki, alisema kwa miaka 60 JICA imeendelea kukua na kutekeleza miradi mbalimbali ya kijamii na kiuchumi kwa kushirikiana na serikali.

Pia alisema Japan imeendelea kunufaika na mengi kutoka Tanzania ikiwamo kilimo cha kahawa Kilimanjaro, korosho na bidhaa za kilimo ambazo zinakubalika katika soko la Japan.

Alitaja miradi mingine ya kijamii inayoendelea kufadhili kuwa ni ujenzi wa soko la samaki 'Malindi Fish Market' Zanzibar, ujenzi wa daraja la juu Gerezani, Dar es Salaam, ujenzi wa barabara mpya ya Bagamoyo na mradi mpya wa kuhimiza ujasiriamali na uvumbuzi kupitia Japan Project 'NINJA.

Alisema mingine ni mradi wa kuhimiza usawa wa kijinsia 'Ladies First' mradi utakaoshirikisha sekta binafsi pamoja na mafunzo kupitia elimu na kubadilishana teknolojia.

Mhandisi Mwandamizi wa Idara ya Usafirishaji Umeme wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) wa Mradi wa Kituo cha Kupooza Umeme MNH, Gwamaka Thobias alisema kituo hicho kilichozinduliwa mwaka 2017 kwa ufadhili wa JIC kimesaidia katika uendeshaji wa hospitali hiyo kutokana na uhakika wa nishati ya umeme kwa muda wote.

Katika mradi wa daraja la juu la Mfugale ambalo ni la kwanza kujengwa Tanzania, Mhandisi kutoka TANROADS Elisony Mweladzi, alisema mradi huo uliojengwa kwa ufadhili wa JICA na kukamilika 2018 umeongeza ufanisi wa hali ya juu katika usafiri hasa wa abiria wanaotoka mjini na kuelekea Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere na maeneo ya Gongo la Mboto.



Mkuu wa Masoko na Mawasiliano wa Benki ya Absa Tanzania, Aron Luhanga (wa tatu kushoto), akikabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 15 kwa Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la EngendeHealth, Dk. Moke Magoma, jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kusaidia miradi ya huduma za kiafya kwa wanawake, vijana, watoto na wenye ulemavu. Wengine ni Meneja Mahusiano wa Absa, Neema Athanas (kushoto), Mkurugenzi wa Wateja wa Makampuni, Hugo Chilufya (wa pili kushoto) na Mratibu Huduma ya Afya ya Uzazi na Mtoto Mkoa wa Dar es Salaam, Agnes Mgaya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ukeketaji tatizo mwaka unaogawanyika kwa mbili

**Na Salome Kitomari**

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Hope For Girls and Women, limesema watoto wa kike mkoani Mara wanateseka, kutokana na jamii hiyo kuendelea kukumbatia mila ya ukeketaji licha ya jitihada zinazofanyika.

Akizungumza hivi karibuni kwenye mdahalo wa nini kifanyike kumaliza ukeketaji mkoani humo, baada ya kuonyesha filamu maalum ya watoto wa kike wanavyokimbilia nyumba salama inayomilikiwa na shirika hilo, Mwanzilishi wake, Rhobi Samwelly, alisema hali si ya kuridhisha hasa kila mwaka unaogawanyika.

Filamu hiyo ilirekodiwa Desemba, 2018 ikionyesha watoto na wasichana wanavyopokewa kwenye nyumba salama wakikimbia ukeketaji, wanavyokamata wazazi, watoto wanavyokataliwa na familia zao mara baada ya muda wa kukeketa kwisha.

Filamu hiyo inayojulikana kwa jina la 'In the Name of My Daughter' (kwa jina la binti yangu), imefadhiliwa na Ubalozi wa Ufaransa nchini katika maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia kwa kauli mbiu ya "Kila Uhai Una Thamani'.

Katika filamu hiyo ndani ya siku saba, walipokewa zaidi ya watoto 210 waliokimbia nyumbani kwao, huku 70 wakilazimika kukaa kwenye nyumba hiyo baada ya wazazi kuwakataa kwa sababu walikataa kufanikisha mila hiyo kufanyika.

"Mkoani Mara bado familia hazijabadilisha mtazamo, zinashikilia mila mbaya. Viongozi wa kimila ni tatizo kubwa kwa kuwa ndio wanaotangaza msimu wa ukeketaji. Wanaalika wazazi wakajiandikishe ili wajue idadi, baadaye wanachagua mangariba ambao wanapeleka vifaa vikabarikwe na viongozi hao.

"Pia wanasiasa wanachagiza mila hii wanaogopa kukemea kwa sababu ni wapiga kura, hawathubutu kuwasema viongozi wa kimila," alisema.

Akielezea changamoto za nyumba hizo, alisema kuna wakati wasichana wanaongezeka hadi 271 huku bajeti ya chakula na mahitaji ikiwa ni ile ile.

"Unapopokea wasichana kama hawa wana mahitaji ya shule, mavazi chakula na huduma nyingine, bajeti ya nyumba unakuta ni ya watoto 150 ila unapokea 271. Muda wa ukeketaji unapokwisha ukiwarudisha kwa wazazi wao wanawakataa inabidi urudi nao uendelee kuwalea, wapo waliokataliwa kabisa nimeishi nao tangu shule za msingi na sasa wako sekondari," alisema.

Ofisa Uhamasishaji wa Hope for Girls and Women, Emmanuel Goodluck, alisema bado kuna tatizo la uelewa hasa kwa vijana ambao wakimuona mtoto wa kike wanaona ng'ombe kwamba akikeketwa na kuolewa naye atapata mali za kwenda kuoa. "Tunanyooshea vidole na jamii yetu, wanachukia tunachofanya (kuwaokoa wasichana), tunaishi kwa tahadhari sana maana chuki ni kubwa, kuna wakati tunaenda walikoandaa sherehe, wanatulaumu kwamba wamepata hasara,"alisema.

"Kwa kabila letu hata akiolewa mtu wa kabila jingine ni lazima wamkekete wakati wa kujifungua vinginevyo kuna haki nyingine atakosa. Binti aliyekeketwa analipiwa ng'ombe 12 na ambaye hajakeketwa ng'ombe saba," aliongeza.


Amina Ramadhani, mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, alikimbia ukeketaji na kwenda nyumba salama ambako ameishi hadi kumaliza elimu ya sekondari baada ya familia yake kumkataa.

"Inauma sana nilikimbilia nyumba salama nikiwa na miaka 12 nisikeketwe baada ya muda (Desemba) wa ukeketaji kwisha nilirudishwa mara kadhaa lakini familia ilikataa kabisa, niliishi nyumba salama nikasoma elimu ya msingi, sekondari na sasa nipo chuo kikuu nasomea sheria nifikie lengo langu,"alifafanua.

Askari wa Idara ya Upelelezi katika Dawati la Jinsia na Watoto, Sijali Nyambuche, alisema wanashirikiana na wanaharakati kukabili wazazi wanaotaka kukeketa watoto wao ambao hukamatwa na siku ya kurudishiwa watoto wanasaini nyaraka maalum na kuna ufuatiliaji kila baada ya miezi mitatu.

Askari huyo ambaye kwenye filamu hiyo alionekana kuwa mstari wa mbele kwenda kwenye nyumba zinazopanga kukeketa watoto wao na wengine waliokeketwa, pia wamefanikiwa kuwafikisha mahakamani na baadhi walihukumiwa miaka tofauti tofauti jela.

## KABWELA



# TSC yataka uboreshaji wa mitaala usafirishaji

**Na Prosper Makene**

BARAZA la Usafirishaji (TSC) limekishauri Chuo cha Usafirishaji nchini (NIT) kuendelea kuboresha mitaala ya mafunzo vyuoni kwa kushirikiana na wadau wa sekta hiyo ili kuendana na soko la ajira za wataalamu wa sekta hiyo.

Akizungumza jana katika kampasi kuu ya chuo hicho mkoani Dar es Salaam wakati wa ufunguzi wa Tamasha la Kwanza la Taaluma lililoandaliwa kwa lengo la kuwajengea uwezo wanafunzi katika kukabiliana na hali ya soko la ajira nchini, Katibu Mtendaji wa TSC, Sallu Johnson alisema:

"Malengo ya kujifunza masuala ya kazi yanasaidia kutimiza malengo ya uanzishwaji wa chuo hicho kwa kuboresha taaluma za wanafunzi na kuakisi dira ya maendeleo ya nchi ya kujenga mifumo imara ya sekta ya usafirishaji.

"Fursa ya kujifunza kwa vitendo inasaidia wanafunzi kuelewa namna ya kufanya kazi zao vizuri na lengo la kujenga kizazi chenye weledi.

"Ninaamini kuwa tukio hilo litakuwa chachu ya ushirikiano baina ya chuo na wadau wa sekta ya usafirishaji na kufikia soko la ajira kwa kuboresha mitaala ya mafunzo chuoni na ushirikiano wa wadau."

Alitoa rai kwa wawakilishi kutoka sekta za umma na binafsi kuendelea na ushirikiano huo kwa sababu jukumu la kujenga wanataaluma waliobobea sio la chuo pekee.

"Tamasha hili la taaluma linaendana na juhudi ya kuunganisha taasisi za elimu na wadau walipo kwenye soko la ajira, wanafunzi watapata fursa ya kujifunza na kuelewa mabadiliko yaliyopo kwenye soko la ajira duniani na sekta binafsi imepewa nafasi kubwa ya kuchangia maendeleo, hivyo wanafunzi wana jukumu la kuongeza uelewa huku wakiwa na mkakati wa kutosha kukabiliana na soko la ajira," alisema.

Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Zacharia Mganilwa alisema tamasha hilo limewakutanisha wadau wa sekta za usafirishaji na wanafunzi wa chuo hicho ikiwa ni sehemu ya kujifunza kwa vitendo pamoja na kupata uelewa wa soko hali ya soko la ajira nchini.

Prof. Mganilwa alisema kumekuwa na nafasi kati ya wanavyofundisha chuoni na vilivyomo kwenye soko la ajira.

Alisema katika kutengeneza daraja hilo wameona haja ya kuwa na tamasha hilo ili walimu na wanafunzi wapate fursa ya kujifunza kutoka kwa waajiri ili kuboresha taaluma zao na kuwajengea uwezo wa kutambua soko la ajira lilivyo.

"Chuo kimebadilika sana kwani tuna programu nyingi, shahada za kwanza 15, diploma 25 na jumla ya wanafunzi 14,000," alisema Prof. Mganilwa.

Pia alisema chuo kinajivunia kutumiza ndoto za waasisi wake za kuboresha sekta ya usafirishaji wa majini, reli, anga na kebo na wapo wanafunzi wa kutosha katika kozi zote.

Alisema tamasha hilo ni sehemu ya mikakati yao ya kuunga mkono juhudi za serikali katika uboreshaji miundombinu ya usafirishaji ikiwamo ujenzi wa reli, ujenzi wa bandari na ujenzi wa meli kwa kuwaandaa wataalamu wazawa waliobobea katika sekta hiyo.



Baadhi ya wahitimu wa mafunzo tarajali kutoka GGML, wakiwa na vyeti vya kuhitimisha mafunzo waliyoyapata kwenye kampuni hiyo katika kipindi cha 2021/2022. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Taasisi yakabidhi vifaa vya kuboresha huduma za afya

**Na Getrude Mbango**

TAASISI ya huduma za Afya Aga Khan-Tanzania (AKHS) imekabidhi mashine nne za kutibu mabadiliko ya awali ya mlango wa kizazi (Cryotherapy machines) zenye gharama ya Sh. milioni 26 kwa Mkoa wa Dar es Salaam ili kusaidia kuboresha utoaji huduma za afya.

Pia imekabidhi mashine 10 za tiba ya kemikali ya saratani (Infusion pumps) zinazogharimu Sh. million 21.5 kwa Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI).

Akizungumza wakati wa hafla ya kukabidhi vifaa hivyo mkoani Dar es Salaam juzi, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Huduma za Afya Aga Khan Tanzania, Sisawo Konteh alisema: "Mradi mtambuka wa saratani una malengo makuu manne na mojawapo ni kuboresha miundombinu katika vituo vya afya vya serikali.

"Mpaka sasa mradi umeweza kufadhili mashine ya kisasa kabisa ya ultrasound katika Taasisi ya Saratani Ocean Road pamoja na mashine ya mionzi ya kuchunguza saratani ya matiti (Mammogram machine) katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando."

Dk. Rashid Mfaume, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam alisema: "Sekretarieti ya TCCP ilifanya kazi nzuri sana kufanya katika vituo 50 vya mradi wa Dar es Salaam ikiwamo kutoa mafunzo ya uchunguzi wa awali wa saratani ya mlango wa kizazi na matiti, ukusanyaji wa takwimu za saratai na tiba shufaa (palliative care).

Alisema baada ya mafunzo hayo, TCCP ilifanya usimamizi shirikishi kuangalia kama huduma walizofundisha zinafanyika na kugundua kuwa baadhi ya vituo vilikuwa na nia ya kuanzisha huduma hizo isipokuwa palikuwa na ukosefu wa vifaa vya kutibu mabadiliko ya awali ya mlango wa kizazi na wakaamua kutoa msaada wa mashine hizo kwenye vituo vichache mkoani Dar es Salaam na Mwanza.

Mkurugenzi wa Tiba wa ORCI, Dk. Mark Mseti aliipongeza timu ya mradi huo kwa kazi kubwa na kujitolea, akisema: "Mradi Mtambuka wa Saratani Tanzania umeweza kufadhili ORCI mashine ya kisasa kabisa ya ultrasound na leo hii unatoa mashine 10 za tiba ya kemikali ya saratani ambazo zitasaidia sana katika ufanisi wa tiba hizo.

"Mradi Mtambuka wa Saratani upo mbioni kufadhili taasisi kwa mashine ya kutibu saratani za koo na nyinginezo (Intraluminal brachytherapy), mashine ambayo itakuwa ya kwanza Afrika ya Mashariki".

Mradi Mtambuka wa Saratani Tanzania (TCCP) unatekelezwa katika mikoa miwili lengwa ambayo ni Dar es Salaam na Mwanza.

Mradi una malengo makuu manne ambayo ni pamoja na kuboresha na kupanua miundombinu iliyopo ya saratani ili kutoa huduma ya kina zaidi ya saratani kupitia uimarishaji wa mifumo ya afya.

Mengine ni kujenga uwezo wa wafanyakazi katika taasisi shiriki ili kutoa huduma bora ya saratani kwa wataalamu waliopata mafunzo na kuwafundisha na kuwabakisha wataalamu wa ndani kupitia programu zilizoidhinishwa.

Lengo lingine ni kuimarisha taratibu za utunzaji wa saratani katika jamii kwa kutoa huduma za afya kwa gharama nafuu na za kina ikiwa ni pamoja na uchunguzi wa awali wa kinga na utambuzi wa mapema, kuendeleza na kudumisha uhusiano na taasisi shiriki katika ajenda na mipango ya pamoja ya utafiti.

## Wahitimu wasifu mkakati wa mgodi

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Geita Gold Mining Limited (GGML) imewaaga wahitimu 26 wa mafunzo tarajali waliokuwa wakifanya mafunzo katika kampuni hiyo kwa mwaka 2021/22.

GGML hutekeleza programu ya mafunzo tarajali kila mwaka kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu inayohusika na ajira, vijana na watu wenye ulemavu pamoja na Mfuko wa Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) na Chama cha Waajiri (ATE). Uongozi wa mgodi huo umesema hiyo ni moja ya mkakati wao kunufaisha jamii ya Tanzania kutokana na shughuli za uchimbaji dhahabu.

Akizungumza katika hafla ya kuwaaga wahitimu hao juzi mkoani Geita, Meneja Mwandamizi anayesimamia Kitengo cha Afya, Usalama, Mazingira na Mafunzo kutoka GGML, Dk. Kiva Mvungi aliwapongeza wahitimu hao kwa kufikia hatua hiyo muhimu katika fani walizozisomea.

"Tunawapongeza kwa kupata fursa hii. Kampuni yetu imekuwa ikitoa nafasi hizi kila mwaka na wahitimu wengi wa vyuo vikuu wamekuwa wakituma maombi yao.

"Kwa ambao mlichangamkia fursa za ajira zilipotangazwa, tunawapongeza kwa kuwa wafanyakazi wa kudumu wa kampuni hii. Kwa ambao hamjapata ajira, endeleeni kutuma maombi yenu kila GGML inapotoa nafasi za kazi.

"Kukamilisha programu hii ni mwanzo wa kuonyesha ukomavu wenu mnapoitwa katika udahili wa kazi. Asimilia kubwa ya vijana waliopitia programu hii wameajiriwa na kampuni mbalimbali, bila shaka nanyi mtaajiriwa pia hapa GGM au kwingineko. Lengo letu ni kuhakikisha sekta ya madini nchini inapata wafanyakazi wenye uzoefu," alisema Dk. Mvungi.

Mhandisi Ruth Mugurusi ambaye ameajiriwa katika kitengo cha ulipuaji cha GGML, alishukuru kupata fursa hiyo akiwa katika mchakato wa kuhitimu mafunzo yake.

"Mimi ni mtanzania, ninaishukuru sana GGML kwa kunipatia fursa hii. Baada tu ya kuhitimu masomo yangu ya chuo kikuu, nilituma maombi na kuanza mafunzo haya. Ninamshukuru Mungu nikiwa katika kipindi cha mafunzo haya, zilitangazwa nafasi na mimi na wenzangu tukatuma maombi na kufaulu usaili na leo hii hatimaye tumeajiriwa na GGML.

"Ninawashauri wahitimu wengine wa mafunzo haya, waendelee kutuma maombi yao kila nafasi zinapotangazwa kwa kuwa GGML ni kampuni inayotoa fursa kwa watu wote wakiwamo wanawake," alisema.

Tangu programu hiyo ianze mwaka 2009 hadi sasa, jumla ya wahitimu 168 wamenufaika. Kati yao, wanawake ni 58 na wanaume ni 110 huku wengi wao wakiajiriwa na GGML katika vitengo vya uchenjuaji dhahabu, uhandisi, ufundi, ulipuaji na uchimbaji madini na baadhi yao wameajiriwa katika kampuni nyingine ndani na nje ya nchi.

# Ujenzi holela chanzo mafuriko kata 13 Dar

**Na Beatrice Shayo**

UJENZI holela wa nyumba katika kata 13 Wilaya ya Kinondoni mkoani Dar es Salaam, umetajwa kusababisha mafuriko huku kata ya Kigogo ikielezwa kuwa kinara wa madhara hayo. Kata hizo ni Kinondoni, Bunju, Mwananyamala, Kunduchi, Tandale, Mzimuni, Magomeni, Makumbusho, Msasani, Mbweni, Mbezi Juu na Kawe.Hayo yalisemwa jana Dar es Salaam na Mratibu wa Maafa Manispaa ya Kinondoni, Pendo Mwaisaka, wakati wa mafunzo ya kuongeza uelewa wa jamii kuhusu maafa yatokanayo na mafuriko yaliyoandaliwa na Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM).

Mwaisaka alisema kati hizo zinaongoza kupata mafuriko yanayosababishwa na kutanuka kwa mito, maporomoko ya udongo na uchimbaji wa mchanga holela unaochangia uharibifu wa mazingira.

"Sababu nyingine inayosababisha mafuriko hayo ni kuziba kwa mifereji ya maji, mabadiliko ya hali ya hewa na mabadiliko ya tabianchi na ujenzi holela wa nyumba unachangia hayo kutokea katika hizo kata 13," alisema.

Alisema wanaendelea kuelimisha jamii kuhakikisha inajenga nyumba kufuata mipango miji na kuwapo kwa mifereji mikubwa ambayo itakuwa inapitisha maji ili kupunguza mafuriko yanayokuwa yanatokea.

Mwakilishi wa IOM, Maurizio Busatti, alisema warsha hiyo ina lengo la kuelimisha jamii namna ya kukabiliana na maafa na itawasaidia kupata uelewa na kujikinga mapema kabla ya kupata madhara.

Alisema lengo lao kubwa ni kupunguza maafa na watashirikiana na serikali katika kuisaidia jamii kupata uelewa wa majanga ya maafa na pia kufikia malengo endelevu.

Naye Mratibu wa Maafa Mkoa wa Dar es Salaam, Gerald Sando, alisema ni muhimu viongozi kusimamia utunzaji wa mazingira ili kuondokana na changamoto ya maafa.

Alisema maafa yamekuwa kero hasa kipindi cha mvua, hivyo mafunzo hayo yatasaidia jamii kujikinga na majanga hayo na kuhakikisha wanajenga nyumba kwa kufuata mipango miji.




Msajili wa mashirika yasiyo ya kiserikali Tanzania, Vickness Mayao (wa pili kushoto) na Msajili wa jumuiya zisizo za kiserilali Zanzibar, Ahmed Abdullah (katikati), wakikabidhi zawadi za fulana kwa washiriki wa maadhimisho ya miaka mitano ya Mtandao wa Ushiriki Tanzania, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DMI yaomba meli ya mafunzo kwa wahitimu

**Na Joseph Mwendapole**

CHUO cha Bahari Dar es Salaam, (DMI), kimeomba serikali ikipatie meli ya mafunzo kwa ajili ya kuwaongezea ujuzi wahitimu wa mafunzo chuoni hapo huku kikilalamikia miundombinu chakavu.

Ombi hilo lilitolewa jana na Kaimu Mkuu wa Chuo hicho, Dk. Tumaini Gurumo, wakati akizungumza kwenye kusanyiko la wahitimu wa chuo hicho ambalo lilifanyika chuoni hapo, Dar es Salaam.

"Uzuri wa meli ya mafunzo ni kwamba inakuwa imetengenezwa maalum kwa ajili ya mafunzo, inakuwa na madarasa na vyumba vya kulala na unaweza kuifanya ya biashara ukaingiza fedha na wakati huo huo ya mafunzo, hivyo uendeshaji wake ukawa rahisi kidogo kwa sababu kumiliki meli si rahisi sana.

"Kwa hiyo tukipata meli ya aina hiyo hata kama itakuwa inasafirisha kontena kutoka Tanzania kwenda nchi zingine, itasaidia kupata nafasi za mafunzo kwa wanafunzi wetu, hivyo kupata mabaharia wengi hapa nchini," alisema.

Dk. Tumaini pia alisema mahitaji ya mabaharia ni makubwa lakini wengi wanaohitimu mafunzo ya nadharia wako mitaani wakisubiri kupata mafunzo ya vitendo ili kukamilika.

Alitaja changamoto inayokabili chuo hicho kuwa ni uchakavu wa miundombinu kwa kuwa kimekuwa kikitumia miundombinu ile ile ya miaka ya 1980 tangu kianzishwe kikiwa na wanafunzi 12 na inaendelea na miundombinu hiyo hiyo kikiwa na wanafunzi 4,049.

"Kwa hadhi ya wataalamu tunaozalisha hapa DMI na kwa maendeleo ambayo dunia imepitia hadi mwaka huu 2022, hatustahili kuendelea kuwa kwenye miundombinu chakavu kama hii," alisema.

Alisema kupitia kusanyiko hilo watajadili changamoto ya muda mrefu sana ya mafunzo ya vitendo kwa wahitimu wa chuo hicho ambayo huwa yanafanyika kwenye meli.

Dk. Tumaini aliishukuru serikali kwa kuendelea kuipa vifaa vya kufundishia na wahitimu kufanya mafunzo ya vitendo ambavyo hata hivyo bado havijakidhi mahitaji ya sasa ya wahitimu walipo.

"Mtambo wa kufundisha wanafunzi kuendesha meli Stimulators ni muhimu kwa wahitimu kwani ndio unamwonyesha mhitimu kila kilichoko kwenye meli lakini mwisho wa siku lazima mhitimu aingie kwenye meli lakini inashindikana kwasababu hapa nchini hakuna meli za kutosha," alisema.

Pia alisema kama kungekuwa na meli nyingi za hapa nchini ingekuwa rahisi kuweka viwango kwa kila meli kuchukua kiasi cha wahitimu watano kwa ajili ya mafunzo ya vitendo lakini fursa hiyo haipo.

"Tunategemea meli za nchi zingine zichukue wahitimu wetu kwa ajili ya mafunzo ya vitendo huwa siyo rahisi sana kwa sababu hizo meli zinakuwa na nafasi chache sana.

Na ili mhitimu wa ubaharia aive vizuri lazima apate mafunzo ya kwenye meli.

"Tunahitaji watu wa kutusemea huko kwenye vikao kwamba Tanzania imeingia makubaliano na baadhi ya nchi sasa yatekelezwe kwa haraka ili vijana wetu wapate fursa nyingi za kufanya mafunzo ya vitendo," alisema.

Wakati huo huo, chuo hicho kimepongezwa kwa kutoa shahada za uzamili katika usafiri wa maji hali ambayo itasaidia kupata wataalamu wengi wa sekta ya usafiri wa majini.

Pongezi hizo zilitolewa na Meja Jenerali mstaafu Said Shaaban, ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar (ZMA) wakati akizungumza kwenye kusanyiko hilo.

Alisema tangu kuanzishwa kwake chuo hicho kimefanikiwa kutoa wahitimu wengi wanaofanya kazi ndani na nje ya nchi katika sekta ya usafiri wa majini.

"Mahitaji ya wataalamu wa bahari bado ni makubwa sana hapa nchini ndiyo maana naona mchango wa DMI ni mkubwa sana katika kupata watu watakaofanyakazi kwenye usafiri wa majini ndani na nje ya nchi," alisema.

## Mafuru awakumbusha wanamipango nafasi yao kwa maendeleo ya taifa

**Na Waandishi Wetu**

NAIBU Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Lawrence Mafuru, amewataka wataalamu wa mipango kuisaidia serikali kuweka mikakati na mipango mbalimbali ya maendeleo inayolenga kuiwezesha nchi kuwa na kiwango cha juu cha ukuaji wa uchumi.

Mafuru alisema hayo jana alipokuwa akifunga kongamano la mwaka la wana mipango lililofanyika jijini Dar es Salaam.

Alisema wanamipango katika taifa lolote duniani, ndio huamua taifa liweje, hivyo aliwataka kuhakikisha mipango wanayoiandaa inakuwa na manufaa kwa kizazi cha sasa na kijacho ili kuitendea haki kada ya mipango nchini.

"Dhima ya mwaka huu ya kongamano hili inaonyesha umuhimu wa kada ya wanamipango kwa mustakabali wa kizazi cha sasa na kijacho na pia inatukumbusha kuwa wanamipango katika taifa lolote lile ulimwenguni ndio huamua taifa liweje.Kwa hiyo mna wajibu wa kuhakikisha mipango mnayoipanga ina manufaa kwa kizazi cha sasa na kijacho na kwa kufanya hivyo tutakuwa tukiitendea haki kada hii na Taifa litawakumbuka," alisema.

Mafuru aliwataka wanamipango kuhakikisha masuala mbalimbali yaliyojadiliwa kwa siku tatu katika kongamano hilo na maazimio yaliyofikiwa, yanatumika kikamilifu katika maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 kutokana na utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 kukaribia mwisho.

Aliongeza kuwa serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango itahakikisha maandalizi ya Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2050 yanakuwa shirikishi ili kupata dira itakayosaidia kukuza uchumi na kuleta maendeleo ya nchi kwa haraka.

Pia aliwashukuru washiriki wa kongamano hilo kwa kujadili kwa weledi mkubwa masuala mbalimbali yakiwamo ya umasikini, mipango yamaendeleona uhimilivu wa deni la taifa, elimu, maarifa na ujuzi kwa ajili ya kuchochea ushindani, kuajiri na ubunifu na mienendo na mabadiliko ya idadi ya watu na athari zake katika maendeleo ya Tanzania kwa siku zijazo.

Katika hatua nyingine, Mafuru aliwataka washiriki wa kongamano hilo kutambua hatima bora kwa taifa kwa miaka 25 ijayo kuwa iko mikononi mwa wanamipango na kuwataka kuwa mabalozi kwa wananchi pamoja na kutoa ushirikiano wa kutosha kwa sekretarieti na timu ya uandishi pindi watakapoanza kupata maoni na ushauri kwenye maandalizi ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050.

# ASA yakabidhi tani 80 mbegu za ruzuku alizeti

**Na Thobias Mwanakatwe,** MANYONI

WAKALA wa Mbegu za Kilimo Tanzania (ASA), imekabidhi tani 80 mbegu za ruzuku za alizeti kwa wakulima wa Wilaya ya Manyoni zitakazotumika msimu huu wa kilimo.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni, Fadhili Chimsala jana alisema, mbegu hizo zenye ubora wa hali ya juu baada ya kuzipokea zimehifadhiwa katika ghala la halmashauri na zitasambazwa katika kila kata ili kuwafikia wakulima. "Kwa niaba ya Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni, wakulima na wananchi kwa ujumla tunaishukuru serikali kwa kuendelea kuwathamini wakulima na kuhakikisha wanapata pembejeo za kilimo kwa wakati na kwa gharama nafuu," alisema. Naye Ofisa Kilimo Wilaya ya Manyoni, Zakayo Ijojo, alisema mbegu hizo aina ya Record CI ni mbegu bora na imethibitishwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbegu Tanzania.

Alisema kwa kuwa mbegu hizo ni za ruzuku, wakulima watauziwa kwa bei nafuu ya Sh. 5,000 kwa kilo moja ikilinganishwa na sokoni ambako wanauziwa Sh. 10,000 kwa kilo.

Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, Rahabu Mwagisa, alisema katika kiasi hicho cha mbegu kilichopokelewa, Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni imepata tani 50 na Halmashauri ya Itigi imepata tani 30.

Alisema maofisa ughani wahakikishe mbegu hizo zinawafikia walengwa na kuwataka wakulima waendelee kutumia wataalamu wa kilimo kwenye maeneo yao ili wawape ushauri wa kilimo bora.



Mkurugenzi Mtendaji wa Songas, Anael Samuel (kulia), akikabidhi funguo za madarasa mawili na ofisi za walimu kwa Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Manispaa ya Ubungo, Lawi Benard, katika hafla ya kukabidhi msaada wa madarasa, vyoo na madawati yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 66 katika Shule ya Msingi Ubungo Kisiwani, Dar es Salaam jana. Msaada huo ni sehemu ya mpango wa kampuni hiyo katika kuboresha sekta ya elimu katika jamii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Walimu, wanafunzi Zanzibar watembelea vivutio Ruvuma

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

WALIMU 24 na wanafunzi sita kutoka Sekondari ya Mwanakwerekwe C Zanzibar, wapo mkoani Ruvuma kwa ziara ya siku 10 ya mafunzo na kutembelea vivutio vya utalii.

Mkuu wa Wilaya ya Songea, Pololet Mgema amesema ziara hiyo iliyoanza Desemba 8 hadi Desemba 16 mwaka huu, walimu na wanafunzi watashiriki usafi katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Ruvuma, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 61 ya Uhuru wa Tanganyika.

"Desemba 9, walimu na wanafunzi watashiriki mdahalo wa kuadhimisha miaka 61 ya Uhuru wa Tanganyika kwenye ukumbi wa Songea klabu," alisema.

Alisema kuanzia Desemba 10 hadi 13 wataanza kutembelea vivutio vya utalii vilivyopo mjini Songea, vikiwamo mlima Matogoro ili kuangalia chanzo cha Mto Ruvuma, Makumbusho ya Taifa ya Majimaji, Hifadhi ya asili ya Luhira, Makumbusho ya Rashid Kawawa na mapango ya Nduna Songea Mbano katika Mlima Chandamali.

Kwa mujibu wa ratiba ya ziara hiyo, Desemba 14 watatembelea Lugari Zoo iliyopo mjini Mbinga na vivutio mbalimbali vilivyopo katika Ziwa Nyasa, Wilaya ya Nyasa.

Alisema Desemba 15, watatembelea na kujifunza masuala mbalimbali kwenye Taasisi zilizopo katika Manispaa ya Songea na Desemba 16, watahitimisha ziara yao kwa kukutana na Jumuiya ya wakufunzi na wafanyakazi wa Chuo cha Ualimu Songea.

# Washiriki kufanya usafi kuadhimisha miaka 61 ya Uhuru

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, Butamo Ndalahwa na watumishi wa halmashauri hiyo wameshiriki kufanya usafi katika kituo cha afya Mlandizi na kutoa misaada kwenye vituo vya kulelea watoto.

Shughuli hizo ni kati ya vitu vilivyofanywa na halmashauri hiyo katika maadhimisho ya miaka 61 ya Uhuru anbayo kilele ni Desemba 9.

Akizungumza baada ya kufanya usafi na kugawa misaada kwa wanawake wajawazito waliokuwa wanapata huduma katika Kituo cha Afya Mlandizi, Ndalahwa alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa maboresho yanayoendelea kufanyika kwenye sekta ya afya.

Alisema kuwapo kwa dawa na watoa huduma kwenye kituo hicho kumesaidia kwa kipindi cha mwaka mzima kutokuwa na taarifa za vifo kwa mama na mtoto huku huduma nyingine zikiwa zimeboreka.

"Katika maadhimisho haya tuliamua kufika katika kituo hiki cha afya na kutembelea vituo vinavyolea watoto wanaotoka kwenye mazingira hatarishi tuwasikilize vikwazo wanavyokumbana navyo serikali ione namna ya kusaidia kuvitatua," alisema.

Mganga mfawidhi Kituo cha afya Mlandizi, Dk. Sebastian Misoji, alimshukuru Mkurugenzi wa halmashauri kwa ufuatiliaji na kushiriki kutatua vikwazo jambo lililosababisha kituo hicho kutoa huduma bora.

Mkurugenzi wa kituo cha kulelea watoto cha Upendo, Erick Ouma, alimshukuru Mkurugenzi kwa kukumbuka kituo hicho na kuwapatia msaada.

Ouma alisema kwasasa kituo hicho kina watoto 19 na wapo wanaosoma vyuo, sekondari na shule za msingi.

Vituo vilivyopatiwa misaada hiyo ni pamoja na Vijaliwa vingi, Upendo na Masjid Noor, ambavyo vipo mjini Mlandizi vikiwalea watoto wanaotoka katika mazingira hatarishi na yatima.



## Shule saba za sekondari zaonyesha umahiri katika ubunifu

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SHULE saba za sekondari za Mkoa wa Arusha, zimeanza kuonyesha umahiri wao wa kisayansi katika masuala ya ubunifu ili kuchochea uibuaji wa vipaji ambavyo vitakuja na utatuzi wa matatizo mbalimbali yanayoikabili jamii.

Mkuu wa Chuo cha Ufundi Arusha (ATC), Dk. Mussa Chacha, alisema ili kutimiza ndoto zao ni lazima wafikiri namna bora ya kuanza kutangaza kwa jamii ubunifu wanaoufanya kwa kuwa unaweza kuleta tija na kuibua ajira kwa vijana.

Aliyasema hayo jana jijini Arusha, wakati wa mashindano ya bunifu mbalimbali yaliyofadhiliwa na Taasisi ya Future Stem Business Leaders.

"Nawashauri vyema sasa wanafunzi mkatumia bunifu zenu na kuzionyesha kwa jamii, hatimaye vipaji vyenu viibuliwe na kwenda kushiriki katika maonyesho makubwa ya ubunifu na uatamizi,"alisema.

Aliwapongeza wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Arusha, kwa kubuni kifaa cha kuchomea plastiki kwa njia sadifu, bila kutoa moshi nje, ambao ni hatari katika maisha na ikolojia ya viumbe.

"Tunaposema bunifu lazima tujue wanafunzi wetu wanavipaji gani na viendelezwe maana kuna wengine wanaakili ya jambo fulani likiendelezwa ajira zitapatikana kupitia bunifu zao na pia vitaweza kulindwa kwa manufaa yao baadaye,"alisema.

Meneja Miradi wa Taasisi ya Future Stem Business Leaders, Josephine Sepeku, akizungumzia vipaji hivyo, alisema taasisi hiyo inaandaa mashindano ya bunifu mbalimbali na kutoa zawadi kwa washindi, kisha kuwaunganisha na taasisi au kampuni za bunifu ili kuatamia bunifu zao tamizi, kwa ajili ya matokeo chanya ya baadaye kwa maslahi ya taifa.

Alisema taasisi hiyo itaendelea kushirikiana na serikali pamoja na shule mbalimbali za sekondari ili kuibua vipaji vya wanafunzi shuleni, pamoja na kuwasaidia kuwaonyesha njia za kupita katika kuhamasisha bunifu zao na kulindwa kwa ajili ya kuleta mafanikio ikiwemo kutatua matatuzo kwa jamii na wakulima.

Baadhi ya wanafunzi walioshinda na kushika nafasi ya kwanza, baada ya kuonyesha bunifu zao, Krishna Merere na Annabrenda Mushi kutoka Shule ya Sekondari ya Wasichana Arusha, kwa nyakati tofauti walisema kifaa walichotumia ni maalum kwa ajili ya uchomaji taka bila kuleta madhara.

# Kaya 395 Longido zinazotishiwa na njaa zapewa msaada

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

TATIZO la mfumuko wa bei ya mahindi sokoni linalozitesa familia masikini katika Wilaya ya Longido, mkoani Arusha, limelisukuma Shirika la Utafiti, Maendeleo na Huduma kwa Jamii (CORDS), kupeleka misaada ya kibinadamu kwa kaya 395 zinazotishiwa na njaa.

Kwa mujibu wa Ofisa Miradi wa CORDS, Martha Katau, familia zilizonufaika na tani 7.1 za msaada huo wa chakula zinatoka katika vijiji viwili vya Wilaya ya Longido.

"Tumeguswa na kuja kutoa msada huu wa mahindi ya chakula, baada ya kubaini kaya nyingi zinakabiliwa na njaa, hivyo tukaona tusaidie kaya hizo. Hii ni kwa sababu tumekuwa na miradi kadhaa hapa Longido, ikiwamo ile ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, "alisema.

Alisema katika mgao huo, Kijiji cha Ildonyo Kaya 165 zimepatiwa tani 2.6 na Kijiji cha Orpurkel Kaya 230 zimepatiwa tani 4.5 ili kusaidia kukabiliana na upungufu wa chakula.

Aidha, Kaimu Ofisa Kilimo wa Wilaya ya Longido, Mariam Fivawo, alisema ukame umesababisha uhaba wa chakula katika maeneo mengi ya wilaya hiyo ambayo asilimia 95 ya wananchi ni wafugaji.

Hata hivyo aliwataka wananchi wenye mifugo kujitahidi kuuza baadhi ya mifugo yao ili waweze kununua chakula cha bei nafuu ambacho tayari kimepelekwa na serikali katika wilaya hiyo.

Mmoja wa wanufaika wa msaada huo, Witness Alais alisema msaada huo wa mahindi utasaidia kukabiliana na njaa, kwani licha ya kukosa chakula lakini pia hata maziwa ya mifugo hawana kutokana na mifugo mingi kufa kwa ukame na iliyobaki haiwezi kuzalisha maziwa kwa wingi.

"Tunashukuru Shirika la CORDS kwa kutupa msaada huu ambao utasaidia, hasa kina mama na watoto ambao wanashida kubwa zaidi ya chakula"alisema.

Shirika hilo pia wiki iliyopita lilitoa msaada wa mahindi tani 12 kwa kaya 553 katika vijiji vya Idonyonaado na Emuruwa katika Kata ya Mfereji Wilaya ya Monduli, Mkoa Arusha.




Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Madini, Msafiri Mbibo (kushoto), akifungua warsha ya madiwani, asasi za kiraia, viongozi wa Halmashauri na wachimbaji madini, kuhusu matumizi ya takwimu zinazotolewa na Taasisi ya uhamasishaji, uwazi na uwajibikaji katika rasilimali za madini, mafuta na gesi asilia (TEITI), katika Mji mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Naibu Waziri awapa somo wawekezaji matumizi teknolojia

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

NAIBU Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kighahe, amewapa somo wawekezaji wanaoshindana katika sekta ya viwanda, ndege na kampuni za utalii kutumia teknolojia rafiki ili kupunguza utoaji wa hewa ukaa, inayochangia mabadiliko hasi ya tabianchi.

Kighahe aliwafunda wawekezaji hao jana alipokwenda kufungua kongamano la ushindani duniani linaloendelea Jijini Arusha.

"Niwadokeze tu kwamba kama kampuni hizi zitazingatia matumizi sahihi ya matumizi ya hewa ukaa, ni dhahiri kuwa yatasaidia kupunguza hewa ukaa inayochangia mabadiliko ya tabianchi.

"Nia ya wafanyabiashara wote ni kupata faida, kwa hiyo ni lazima kuhakikisha ushindani wa haki unazingatiwa, ikiwamo kuhakikisha mamlaka ya ushindani zinazuia ukiritimba katika biashara ikiwamo nguvu ya soko kuwameza washindani katika biashara."

Pia kudhibiti muingiliano wa biashara katika unaolenga kuwaweza washindani katika baadhi ya biashara na kuongeza kuwa ongezeko la mabadiliko ya tabia nchi unahatarisha usalama na uhatarishi wa theluji katika Mlima Kilimanjaro.


"Wawekezaji katika sekta ya viwanda, ndege na kampuni ya utalii kutumia teknolojia rafiki katika kudhibiti mazingira ikiwamo wanyama katika sekta ya utalii katika upunguzaji wa ikolojia ya wanyama ikiwamo ukataji ovyo wa miti na mkaa "

Kutokana na umuhimu huo, alitoa rai kwa wadau mbalimbali kupanda miti ili kudhibiti uongezeko la hewa ukaa hivyo ni lazima miti ipandwe katika kulinda ikolojia ya wanyama sanjari na uoto asili

"Ili kuendelea kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi ni vyema tukapanda miti kwa wingi na kila mmoja kumhamasisha mwenzake kitokukata miti ovyo ili kuweza kudhibiti ongezeko la hewa ya ukaa"alisema

Kabla ya ufunguzi huo Mwenyekiti wa Tume ya Ushindani Tanzania (FCC), Dk.Aggrey Mlimuka, alisema kongamano hilo ni muhimu katika kuhakikisha kunakuwa na uendelevu na ushindani katika kuhakikisha utalii unakua kwa kasi sanjari na ulinzi wa mazingira

Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Richard Ruyango, aliwasihi wadau mbalimbali katika sekta ya mazingira kuhakikisha mazingira yanalindwa ili kuzuia matatizo ya mabadiliko ya tabia nchi na ikolojia.





## Waajiri waagizwa kuajiri wataalamu wenye sifa

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi, amewaagiza waajiri wote nchini, kuajiri wataalamu wa ununuzi na ugavi wenye sifa ili kuepukana na mzigo wa lawama kwa baadhi yao miradi inapokwama.

Alisema hayo jana katika kongamano la 13 la wataalamu wa ununuzi na ugavi lililofanyika jijini hapo.

Alisema ili kuepukana na jambo hilo, ni vyema waajiri wakahakikisha wanaweka watu wenye sifa za kusimamia idara za ununuzi na ugavi.

"Panapotokea mwajiriwa kakosa sifa wasisite kuwapeleka shule ili kuwawezesha kujiendeleza na sisi tutajitahidi kuzifanyia kazi lengo likiwa ni kupata watu wenye sifa katika sekta hii," alisema Ndejembi.

Aliitaka bodi ya wataalamu wa ununuzi na ugavi kuendelea kuchukua hatua kwa kuzingatia sheria, utaratibu na kanuni zilizoko kwa wataalamu watakaokiuka miiko ya taaluma hiyo ili kuhakikisha wataalamu hao, wanafanya kazi kwa weledi na ujuzi, kwa kuwa wana mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa nchi.

"Ili kuleta tija kwenye utekelezaji wa miradi serikali, lazima ijielekeze kufanya ununuzi wa kimkakati kwa kuzingatia ukubwa wa ununuzi na uwiano wa bidhaa na huduma zinazotumika serikalini, ni imani yangu kwenu kupitia mada na majadiliano mbalimbali yatakayowasilishwa kuhusu ununuzi wa kimkakati zitawajengea uwezo na ufanisi katika katika kutekeleza miradi," alisema.

Alisema serikali ina matumaini makubwa na wataalamu wao kufikia malengo ya mipango ya maendeleo ya taifa ya miaka mitano na anategemea maazimio ya kongamano hilo yatapelekea kupunguza matatizo yanayotokea katika ununuzi na ugavi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB), Godfrey Mbanyi, alisema mwaka 2022 wamesajili wataalamu 1995 na kuongeza idadi ya 15,309.

"Bodi iko katika hatua za awali za kuchukua hatua za kinidhamu na imekusudia kuwaita wataalamu 63, ili waweze kutoa maelezo na hatua mbalimbali zichukuliwe, lakini tumetoa karipio kwa wataalamu 78, ambao wamebainika kufanya kazi chini ya weledi na maelekezo ya kitaaluma," alisema Mbanyi.

Alisema lengo la kongamano hilo ni kuwaleta na kuwakutanisha pamoja wataalamu hao ili kujadili fursa na matatizo yaliyoko, kwa ajili ya kupeleka taaluma hiyo katika kiwango kinachohitajika.

Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Jacob Kibona, alisema bodi yake imepewa jukumu la kisheria la kusimamia wataalamu wa ununuzi na ugavi, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha Tanzania inakuwa na wataalamu wa kutosha wenye sifa stahiki na kufuatilia utendaji wao.

Kaulimbiu ya kongamano hilo ni "Fursa na changamoto katika kutekeleza ukuaji endelevu wa uchumi na maendeleo ya jamii".

# Watoa elimu ya madhara ukatili kwa wanafunzi Manyara

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

BAADA ya Mkoa wa Manyara kushika nafasi ya pili kitaifa kwa matukio ya ukatili wa kijinsia, wadau wanaoongoza mapambano dhidi ya vita hiyo, Shirika la CSP limeanza kuwafungua macho wanafunzi wa shule za msingi na sekondari mkoani Manyara kuhusu madhara ya ukatili. Uamuzi huo unalenga kupunguza kiwango cha matukio hayo, ambayo yameiweka Manyara katika nafasi za juu za mikoa tishio nchini ikiwa na rekodi ya matukio 6,000 kwa mwaka uliopita, sawa na asilimia 58.

Akizungumza jana katika Wilaya ya Babati, wakati wa mwendelezo wa maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia nchini, Mwanasheria wa Shirika la CSP Eliakim Paulo, alisema hadi sasa wamezifikia shule tatu za msingi za Darajani, Oysterbay na Babati.

"Shirika la Civil Social Protection Foundation, tumeona kwamba watoto ni kundi maalum, hivyo hawawezi kujitegemea au kujilinda wao wenyewe, kwa hiyo tukafikia uamuzi tuwape elimu ili wajitambue na kuepuka hayo," amesema Paulo.

Kutokana na uamuzi huo, mwanasheria huyo alisema matukio ya ukeketaji, ubakaji na ulawiti yanawaathiri watoto, hivyo wanatoa elimu hiyo kwa wanafunzi hao ili kuhakikisha matukio hayo yanapungua au kumalizika.

Alisema wataendelea kutoa elimu ya kupinga matukio ya ukatili wa kijinsia kwenye shule nyingine ili wanafunzi hao wazidi kujitambua na kuepuka kufanyiwa ukatili.

Paulo alisema watatoa elimu hiyo kwa jamii hususani kwa wanawake na watoto katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo ili kuhakikisha matukio ya ukatili wa kijinsia yanakomeshwa.

"Pamoja na shule za msingi, pia tutatoa elimu hii kwenye mikusanyiko ya watu ikiwamo hospitalini, minadani na nyumba za ibada," alisema Paulo.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Mji wa Babati, Farida Sekiete, akizungumza na wanufaika wa mafunzo hayo aliwataka watoto hao wasikubali mtu yeyote ashike sehemu zao za siri.



Katibu Tawala wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Upendo Wella (aliyesuka nywele), akishiriki kuondoa takataka zilizotupwa katika dampo lililoanzishwa na baadhi ya wakazi wa Kijiji cha Shirinjoro na wafanyabiashara wa Soko la Samaki la Mailisita, nje ya ofisi za serikali jana, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 61 ya Uhuru wa Tanganyika. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Mradi uboreshaji huduma mahakama watengewa bil.14/-

**Na Mwandishi Wetu,** LUSHOTO

JAJI Mkuu Prof. Ibrahim Juma, amesema awamu ya pili ya mradi wa uboreshaji huduma wa mwaka 2021/2025, unaofadhiliwa na Benki ya Dunia (WB), umetengewa Dola za Marekani milioni sita (Sh.bilioni 14).

Mradi huo ni maalum kwa ajili ya kuongeza ujuzi na maarifa kwa watumishi wa mahakama nchini.

Alisema fedha hizo pia zitatumika kuimarisha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA).

Prof. Juma, aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na wahitimu wa astashahada na stashahada ya sheria katika mahafali ya 22 ya IJA yaliyofanyika Wilaya ya Lushoto, mkoani Tanga.

Alisema lengo ni kuhakikisha kuwa chuo hicho kinachotoa elimu bora na mafunzo kwa wanafunzi wake na kwa watumishi wa mahakama nchini, kwa njia ya TEHAMA.

"Kutengwa kwa kiasi hicho kikubwa cha fedha katika mradi huu wa pili ni ushahidi kuwa, Chuo kinatakiwa kuhama kutoka 'analogue' hadi kidijitali katika utoaji wa mafunzo.

"Fedha zilizotengwa siyo za semina na makongamano, ni za maboresho ambayo yatatoa matokeo, yatakayopimika na yatakayotathiminiwa na serikali na maofisa wa Benki ya Dunia, hivyo ni muhimu kuchangamkia nafasi hii," alisisitiza Jaji Mkuu.

Vilevile, Prof. Juma, alisema Chuo cha Uongozi wa Mahakama, kinatakiwa kitengeneze Jukwaa la Ki-elektroniki 'e-learning platform' litakalotumia akili-bandia (Artificial Intelligence) kwa ajili ya kufundishia, na wanafunzi kupata mafunzo kwa njia ya mtandao.

Hivyo alisisitiza jukwaa hilo linatakiwa liwe la kisasa na lenye ubora, na liweze kutumika kutoa elimu na mafunzo sio tu kwa wanafunzi wa stashahada na astashahada ya sheria, bali pia litumike kutoa masomo na mafunzo elekezi na endelevu kwa majaji, wasajili, naibu wasajili, watendaji, mahakimu na watumishi wa kada zote.

"Ni mategemeo yetu kuwa, jukwaa hilo litasheheni taarifa na mambo yote muhimu ambayo wanafunzi, wahadhiri na watumiaji wengine watajisomea na kujiendeleza. Chuo hiki hakitakuwa kisiwa, kitapata wanafunzi dunia nzima na kuwawezesha watumishi walio kazini kuendelea na kazi huku wakisoma," alieleza Jaji Mkuu.

Alisema jukwaa la ki-elektroniki litakalotengenezwa na Chuo cha Uongozi wa Mahakama kwa ajili ya kutoa mafunzo (e-learning platform), litasaidia kuokoa muda kwakuwa litatumika kutoa mafunzo katika majengo jumuishi yaliyojengwa na yatakayojengwa na mahakama na ambayo yatatumika pia kama vituo vya mafunzo kwa njia ya teknolojia kwa watumishi na wadau bila kusafiri hadi IJA-Lushoto.

Jaji Mkuu, Prof. Juma, alisisitiza kuwa Watanzania wa leo wanaishi katika dunia inayosukumwa na teknolojia yenye nguvu kubwa ya mapinduzi ya nne ya viwanda, hivyo, wahitimu wote wenye elimu ya ngazi au daraja lolote, ni lazima wahakikishe kuwa elimu waliyopata kutoka Chuo cha Uongozi wa Mahakama haitoshi na ni lazima waiboreshe kila siku ili ilingane na mahitaji ya ushindani mkubwa katika Karne ya 21.

Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA), ambaye pia ni Jaji wa Mahakama ya Rufani, Dk. Gerald Ndika, alisema chuo hicho kimepata mafanikio makubwa, ikiwa ni pamoja na kukamilisha utayarishaji wa mwongozo wa ufundishaji wa ajili ya watunza kumbukumbu wa mahakama kuhusu uendeshaji wa mashauri ya watoto.




MRISHO MAKWAYA NA NYUMBA YAKE ...

# Ngome 'kivita' TANU ilikoasisiwa kwa siri, mahali Nyerere alikopata salamu na kuanza safari ya UNO

• Makamanda wake; Kassanga Tumbo, Tewa, Maswanya...

**Na Neema Hussein, Mpanda**




Mzee Selemani Makwaya; shuhuda wa uhuru na nyendo za baba yake na Rais Julius Nyerere, akipatiwa shati la uzalendo la mkoa Katavi na uongozi wa serikali. **PICHA: NEEMA HUSSEIN**

LEO hii ni mzee tena hasa kwa umri, mwenye heshima na jina kubwa kwa maana ya kitaifa, akibeba maana ya uhuru wa nchi Tanganyika kwa hoja na vielelezo.

Huyo ni Mzee Selemani Makwaya, ambaye tarehe za kuwania uhuru alikuwa bwana mdogo, ila baba yake

Mzee Mrisho Makwaya, ndiye alikuwa ameiva katika harakati hizo, akiwa swahiba wa nahodha wa nyendo za kuwania uhuru nchini, Hayati Mwalimu Julius Nyerere.

Mzee Selemani anadokeza kuwa na bahati ya kuambiwa mengi kutoka kwa baba yake aliyefariki mwaka 2016 , mbia wa kabla na baada ya kupatikana uhuru wa Tanganyika, akiwa mshiriki hai.

Anasimulia: "Baba yangu alitueleza licha ya kutueleza nilishawahi kwenda naye Ikulu, aliitwa na Nyerere akaniambia 'mwanangu twende Mwalimu kaniita Dar es Salaam kuna kikao hivyo twende pamoja'..."

Hapo anataja nafasi ya Mpanda, kwamba ingawa wengi hawapafahamu historia pana, ila pamebeba mzizi wa historia ya nchi, kwani palikuwa maeneo makubwa ya kimkakati ya kusaka uhuru na ndiko zilikoanzia harakati.

Mzee Selemani anakumbusha kwamba, Mwalimu Nyerere akiwa Mpanda ndio alipata simu ya kuhitajiwa Umoja wa Mataifa, alikoitwa kwenda kurasimisha mchakato wa uhuru, akisema baada ya hapo akaanza safari akipitia nchi jirani Zambia, jambo analosema analikumbuka vyema.

"Jengo hili tulilosimamia hapa leo linaelezea harakati mbalimbali za chama cha TANU enzi za Mwalimu Nyerere wakati wakifanya harakati za kupigania uhuru wa Tanzania," anasimulia Mzee Selemani, akiwa na ufafanuzi, ndiko alikofikia Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, katika nyendo za uhuru, jengo ambalo leo linaingia katika historia ya nchi.

**KWANINI MPANDA?**

Selemani Makwaya, mtoto wa Marehemu Mzee Mrisho Makwaya, anasema baba yake alikuwa rafiki wa Mwalimu Nyerere, kiunganishi cha urafiki wao kikiwa ni ukaribu katika kupambana kutafuta uhuru Tanganyika.

Anasimulia baba yake walifahamiana na Nyerere, kupitia kwa mjomba wake aliyekuwa Posta Masta (Mkuu wa Posta) Tabora, Nyerere akifundisha. Simulizi yake inaendelea: "Sasa baba yangu katika harakati za kutafuta maisha alijikuta amefika Mpanda. Akiwa Tabora, alikuwa fundi viatu na alikua sonara anauza urembo kama vile hereni na pete.

"Basi aliendelea na biashara hiyo kwa kufuata maeneo ya migodini, akiona huku hali imekuwa mbaya anahamia sehemu nyingine kuliko na mgodi akajikuta amefika Mpanda, hapa Mpanda kulikuwa na mgodi mkubwa sana wa dhahabu, ulikuwa ukimilikiwa na makaburu.

"Sasa baba baada ya kufika huku aliendelea na kazi yake ya kushona viatu, ndipo hao makaburu wakamuona wakataka awatengenezee viatu manamba (watumishi) wa hapo mgodini, basi walimchukua wakampeleka humo mgodini wakampa hiyo tenda ya viatu," anasimulia.

Anaendelea:"Urafiki wao Mrisho Migila Postamasta na Nyerere, wakaanzisha klabu, kumbe ndio chama chenyewe ambacho ni TANU. Sasa wakafungua na grosariy hapo wakawa wanauza na bia, Nyerere akiwa ni Katibu.

"Basi harakati za Nyerere zikaendelea kupamba moto huko Tabora katika kukutana kwao, Mwalimu Nyerere akaanza kumwambia huyo Postamasta 'bwana sasa hii nchi ya Tanganyika vipi huko Shinyanga wapo makaburu, Mpanda?' wapo makaburu (akajibiwa), hizo ndio sehemu za kupeleka chama maana ndio ngome kubwa makaburu wanachukua mali na kuondoka nazo."

Anasema, wakakubaliana kwamba, ndiko maeneo panapaswa kuwekezwa harakati zao za kudai uhuru, hasa penye mikusanyiko ya wayui kama machimboni.

"Hata ile grosary waliyofungua pale Tabora ilikuwa ni njia tu ya kuwapata watu na kuwaeleza lengo la Chama cha TANU, ikiwa ni pamoja na kuwapa kadi za chama, ila walikuwa wakifanya kwa siri mno ili hao Waingereza wasijue.

"Sasa mjomba wangu huyo Postamasta akamwambia Mwalimu Nyerere, Mpanda kuna shemeji yangu (Mrisho Makwaya) anaweza kutusaidia kwa hilo, tukapeleka watu kwa siri ndipo Nyerere akateua watu watano kuja Mpanda.

"Haya ni maneno sasa aliyokua akiyasema baba yangu ( Marehemu), maana tulimuuliza 'wewe na Nyerere kuna nini mbona kila akija Mpanda, lazima utafutwe?" Ndio kutupa hiyo stori, sasa basi alisema alipokea watu watano ambao ni Tewa Said Tewa, kuna mmoja ali-

INATOKA UK.15



## CHARLES MASALAKULANGWA;

# Mkongwe aliyeanza shule akiwa na miaka 15, asimulia uzoefu wa ukoloni, hadi uhuru

**Na Anthony Gervas, Mwanza.**

"NILICHELEWA kuanza shule, sababu nilikuwa nachunga ng'ombe nyumbani zaidi ya 100. Nilizaliwa mwaka 1943, fikiria nilianza kusoma darasa la kwanza 1958, ukipiga hesabu nilikuwa na miaka 15," anajitambulisha Mzee Charles Masalakulangwa, mkazi wa Mtaa wa Bugarika C, jijini hapa.

Hapo anakumbuka maisha zama za ukoloni akiwa kijana akiwa shuleni. Anafafanua: "Wakija wakaguzi wa elimu shuleni,mimi na rafiki yangu tunakwenda kujificha kwenye shamba la mbaazi la shule tusifukuzwe shule, kwa sababu umri wa kusoma ulikuwa umezidi. Wakiondoka ndiyo na sisi tunaenda darasani."

Mzaliwa huyo wa kitongoji cha Lutala, kijijini Dasina wakati huo wilayani Maswa, mkoa wa Shinyanga, leo hii kiko wilayani Itilima mkoani Simiyu, anaeleza simulizi za ujana wake unaoanzia zama ukoloni, utawala wa machifu na watemi akichunga ng'ombe kabla hajaanza shule, maishani akihofia sana wanyama wakali porini kama simba, akiishi kwenye nyumba zilizojengwa kwa miti, kuezekwa na nyasi.



Mzee Charles Masalakulangwa, akiwa nyumbani kwake,katika ofisi yake ya maktaba ya vitabu mbalimbali. **PICHA: ANTHONY GERVAS.**

Anasema vitanda vyao vilitengenezwa kienyeji kwa miti na matandiko ya ngozi za wanyama kama vile ng'ombe, mbuzi na kondoo. Anafafanua:"Tuliwasha moto kwa kupekecha Ulindi na Wimbombo,tulilala usiku ndani pamoja na wanyama, mbuzi, ndama na kondoo, tulijenga nyumba zile katikati tulijenga duara ya miti mfano wa zizi, tuliepuka wasiliwe na simba au fisi."

Anaeleza walichunga ng'ombe kutwa nzima bila ya kunywa maji kutokana na ukame wa kiangazi, hivyo walilazimika kuwanywesha siku ya pili, kutokana na umbali wa kuyafikia maji Mto Simiyu.

Pia, anataja kilimo walilima mtama na uwele uliotumika kwa chakula na biashara na kuna wakati wa njaa kali, walibadilishana mtama na kupewa ng'ombe. Pia, anasema kila ng'ombe alilima kipande chake cha shamba la mtama nyumbani.

Anasimulia pesa zilikuwa adimu,hapakuwapo mashine za kusaga unga, bali walitumia mawe. Anataja mwaka 1954 kilianzishwa Chama Cha Tanganyika African National Union (TANU) wakati Zanzibar, kulikuwapo Afro Shirazi Party (ASP), zahanati au vituo vya afya vijijini havikuwepo, watu walijitibu zaidi kwa dawa za miti shamba.

Anakumbuka kuna siku ng'ombe wao alitumbukia shimoni malishoni na hakujua, lakini baada ya kufika nyumbani baba mzazi alikagua akamkosa, hata akaangukia kucharazwa bakora, wakaenda kumtafuta hadi usiku wa manane wakampata shimoni kisha kumrejesha nyumbani.

Mwaka 1958 akiwa na miaka 15, akajiunga darasa la kwanza katika

INAENDELEA UK.18

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**WAKALA WA UFUNDI NA UMEME TANZANIA (TEMESA)**

**MIAKA 61 YA UHURU WA TANGANYIKA**







Tuulinde, Tuuheshimu, Tuuthamini na Tuudumishe Uhuru Wetu.

17184301



Bodi ya Ushauri, Menejimenti na watumishi wa Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania **(TEMESA)** wanaungana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan** pamoja na Wananchi wote katika kusherekea miaka 61 ya uhuru wa Tanganyika. **TEMESA** tutaendelea kuuenzi uhuru kwa vitendo kwa kufanya kazi kwa bidii na kutoa huduma bora kwa fursa za maendeleo.

***Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA),***

Mhe **Dkt. Samia Suluhu Hassan**
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

**TEMESA HOUSE, 2 Mtaa wa TEMESA, 41104 Tambukareli, 1075, Dodoma**

Namba ya Bure: 0800110379, Barua Pepe; info@temesa.go.tz, Tovuti: www.temesa.go.tz

**temesatanzania**



## MRISHO MAKWAYA NA NYUMBA YAKE ...

# Ngome 'kivita' TANU ilikoasisiwa kwa siri, mahali Nyerere alikopata salamu na kuanza safari ya UNO

INATOKA UK.13

kuwa anaitwa Mzee Kandoro jina jingine sikumbuki, ila alikuwa ni Baba yake aliyekua Mkuu wa Mkoa, Abbasi Kandoro.

"Mwingine alikuwa marehemu Kasanga Tumbo, mwingine ni marehemu Said Maswanya, aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani wa Tanganyika. Kipindi hicho usafiri wa barabara haukuwa mzuri, hivyo walitumia treni ya Uvinza walivyoshuka, wakachukua magari wakaja mpaka hapa.

"Waliambiwa na Nyerere 'mkifika mtafuteni mtu mmoja anaitwa Mrisho Makwaya, hapo Mpanda.' Basi baba aliwapokea walifika wakasema sisi bwana tumetumwa na Mwalimu Nyerere kama wanachama wa Chama cha TANU, ilikuwa 1951 kwenda 1952.

"Shughuli hizi tumekuja kufanya za siri, maana tunaweza kukamatwa endapo tukigundulika na kufungwa kabisa, sababu ngome ya makaburu iko huku (Mpanda). Kwa, hiyo, tunaomba utusaidie, walimwambia baba. Basi baba yangu akatoa nyumba yake wakafika hao watu na wakaanza kuuza kadi za chama (TANU) kwa siri.

"Mzee wangu alichukua kadi namba moja na mama yangu mzazi alichukua kadi namba mbili. Walipata wanachama wengi, ila wengine walikua wakiwapinga na kusema 'hii itakuja kutuletea shida, wakitugundua makaburu watatuua' wakasema haina shida liwalo na liwe," anasimulia historia.

### KUZALIWA TANU

"Basi kufikia mwaka 1954, Mwalimu Nyerere akawapigia simu hizi simu za kizamani, akawambia jamani sasa Chama kimekuwa na nguvu, msijifiche tena fanyeni mkutano wa hadhara," anasimulia Mzee Selemani na kuendelea:

"Basi siku wanafanya mkutano wa hadhara, ndio walipanda hiyo miti ya misufi (eneo la Mnarani Mpanda), ili iwe kielekezo Mwalimu Nyerere alikuja wakapiga na picha ya pamoja na Mzee (Marehemu Mrisho Makwaya) alikuwepo.

Anasema nyumba ya baba yake Mzee Mrisho Makwaya, iliyotumika kuwaficha



Marehemu Mzee Mrisho Makwaya, mwanaharakati wa uhuru na Mwalimu Julius Nyerere, alipokuwa na mkewe, katika zama za uhai wao.

watu watano waliotumwa na Nyerere, iliendelea kutumika kuwa ofisi za chama na baba yake ndio akawa Mwenyekiti wa kwanza wa TANU Mpanda.

"Mzee(Mrisho Makwaya) alisema hivi, mwaka 1959 Mwalimu Nyerere alikuja kwa siri akafikia palepale kwenye ile nyumba ya Mzee (marehemu Makwaya), alikaa kama siku tatu, alikuwa akitumia usafiri wa treni hadi Uvinza, halafu anakuja na yale magari ya kizamani.

### SAFARI YA UNO

"Kwa hiyo, Nyerere akiwa hapa Mpanda kwenye nyumba ya Mzee akiwa amesimama mlangoni, alipokea ujumbe kwenye simu wa kwenda Marekani," anasimulia Mzee Selemaani na kuendelea:

"Basi alitoka akaitangaza pale ile meseji, sasa Mpanda hapakuwa na ndege inayokwenda nje wala uwanja wa ndege ilibidi Mwalimu Nyerere, akapandie ndege Zambia, sehemu moja inaitwa Mbala. Mwalimu alipokwenda kuchukua madaraka sasa kuwa Waziri Mkuu. lazima atengeneze serikali.

"Mbunge wa kwanza wa Tanganyika kwa wilaya ya Mpanda, alikua marehemu Kasanga Tumbo. Ofisi yake ya bunge alikuwa chumba kile pale Ofisi ya Bunge (jengo la Mzee Mrisho, Mpanda), alikuwa ni hapa maana kulikuwa hakuna maeneo yote yametawaliwa mwaka 1959 kwenda 1960 hadi kupata uhuru."

Mzee Selemani anasimulia namna Mwalimu Nyerere akiwa Waziri Mkuu, alitangaza mipango ya kuunda maendeleo ya Tanganyika kwa miaka mitatu katika kipindi cha mpito kuelekea uhuru, akisema wakati huo, mwenyeji wake wa Mpanda, Mzee Mrisho aliendelea kuwa Mwenyekiti wa TANU.

Anasimulia namna Waziri Mkuu, alivyosafiri kukagua hatua za maendeleo sehemu mbalimbali, akitumia magari na ndege. Mzee Selemani ana simulizi za ziada: "Alikuwa akifika hapa mtu wa kwanza ni Mzee wangu (Mzee Mrisho) atampokea, watasalimiana."

Mzee Selemani anakumbuka hata mwaka 1963 Mzee alipoenda mkutanoni jijini Dar es Saalam, hata kutokea dhoruba ya kiusalama, baba yake ni miongoni mwa waliokuwa eneo la tukio.

"Sasa wale wajumbe waliobaki walipigwa sana akiwemo mzee wangu alipigwa sana, alikaa Dar es Salaam miezi mitatu kwa matibabu, hapo ndio Mzee aliona aache shughuli za kichama (TANU) kwa yale maumivu aliyopata.

"Ila Nyerere aliendelea kumkumbuka kila walipokuwa wakiazimisha shughuli za kichama, watu walianza kumshawishi Mzee ili amuone Nyerere ampe madaraka kama wengine.

"Mzee aliendа kumuona Kawawa, Kawawa akampeleka kwa Pius Msekwa akampa kadi ya kuonana na Nyerere, ila Mzee aliwaza sana akikumbuka zile shughuli za kichama za malumbano ya kugombea vyeo vilimkatisha tamaa," anakumbusha historia.

Hadi sasa anasema, historia ya mji Mpanda, hali kadhalika ya uhuru wa nchi, imedumu kuoanishwa na maisha na makazi ya Mrisho Makwaya, akibaki nembo ya mji wa Mpanda katika kuipatia uhuru wa Tanganyika na simulizi ya eneo la Mnarani.



Nyumba ya Marehemu Mzee Mrisho Makwaya, ambako kulikuwa kambi ya TANU na safari ya Julius Nyerere kwenda UNO, ilikoanzia. **PICHA ZOTE: NEEMA HUSSEIN.**

GCLA GOVERNMENT CHEMIST LABORATORY AUTHORITY

**MAMLAKA YA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI (GCLA)**

**MAADHISHO YA MIAKA 61 YA UHURU**




Dr. Hussein Ali Mwinyi
Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

Mhe. Samia Suluhu Hassan
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Watumishi wa **MAMLAKA YA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI (GCLA)** tunaungana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan na Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Dr. Hussein Ali Mwinyi na Watanzania wote katika kusherehekea Maadhimisho ya Miaka 61 ya Uhuru wa Tanzania.

**1961 - 2022**

*Mamlaka itaendelea Kuenzi mema yote ya Uhuru kwa kuimarisha huduma za uchunguzi wa kimaabara na kuendelea kusimamia Sheria za Mamlaka Katika kuunga mkono dhamira ya Serikali ya awamu ya sita ya kuijenga Tanzania katika Nyanja zote za kimaendeleo ya sayansi na teknolojia.*

*Muungano Wetu ni Tunu Yetu*
*Tuulinde, Tuutunze na Tuuheshimu*

**9 DESEMBA**

217185902

Gcla.Tanzania gcla1895 gcla_official

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## WIZARA YA MAJI
## WAKALA WA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI

RUWASA
Rural Water Supply and Sanitation Agency

"Kuanzishwa kwa RUWASA kumerekebisha usimamizi wa miradi na kuongeza kasi ya utekelezaji wake, tumeweza kuongeza nidhamu ya kazi na ufanisi wa kazi". Hayo yalisemwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Machi, 2022 wakati wa kilele cha wiki ya maji Mlimani City Jijini Dar es Salaam.

RUWASA ambayo ni kifupi maneno ya Kiingereza Rural Water Supply and Sanitation Agency ikiwa na maana ya Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, ni taasisi changa ya umma iliyoundwa na Serikali kupitia Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini Na. 5 ya Mwaka 2019 na kuanza kazi rasmi tarehe 1 Julai 2019.

Majukumu ya RUWASA ni kusanifu na kujenga miradi ya maji, kusimamia skimu za usambazaji maji na kutoa huduma ya maji safi na salama kwa wananachi waishio vijijini kupitia taasisi zinazojulikana kama CBWSOs, yaani Community Based Water Supply Organizations au kwa Kiswahili Vyombo vya Utoaji wa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii. Pia, RUWASA ina jukumu la kuunda, kusajili, kuzijengea uwezo na kudhibiti CBWSOs.

Kaulimbiu yetu maarufu ni "MAJI BOMBANI". Kaulimbiu hii tuliibuni kwa lengo la kuhamasisha na kujenga dhana mpya ya uwajibikaji miongoni mwa watendaji wa Sekta ya Maji hususan RUWASA kwamba kipimo cha mafanikio yetu ni MAJI KUTOKA BOMBANI na siyo vinginevyo.

**Malengo na Mipango ya RUWASA**
RUWASA inatekeleza shughuli zake kwa kuongozwa na Mpangomkakati wa miaka mitano, yaani 2020/2021 hadi 2024/2025. Mpangomkakati unalenga pamoja na mambo mengine, kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi waishio vijijini hadi kufikia kiwango kisichopungua asilimia 85 na hivyo kutimiza lengo la Ilani ya Chama Tawala (Chama cha Mapinduzi) ya Mwaka 2020 - 2025.

**Hali ya Huduma ya Maji Ilivyokuwa Kabla ya Kuundwa kwa RUWASA**

Wakati wa kuanzishwa kwake,



Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akigusa maji mara baada ya Uzinduzi wa mradi wa maji wa Kakonko – Kiziguzigu uliopo Kakonko Mkoani Kigoma.

RUWASA ilirithi jumla ya skimu za maji 1,379 zilizokuwa zimekamilika na kulikuwa na miradi 632 ya ujenzi wa skimu za usambazaji wa maji katika maeneo mbalimbali nchini. Kati ya skimu hizo zilizokuwa zimekamilika, 177 zilikuwa hazitoi huduma ya maji kwa wananchi kutokana na changamoto mbalimbali ikiwemo changamoto ya kukauka kwa vyanzo vya maji. Wakati huo, yaani mwezi Julai 2019 upatikanaji wa huduma ya maji vijijini ulikuwa ni wastani wa asilimia 64.8.

Pamoja na kiwango hicho cha upatikanaji wa maji, kwa ujumla, hali ya huduma ya maji vijijini haikuwa ya kuridhisha. Ujenzi wa miradi ulikuwa ukichukua muda mrefu. Hata miradi iliyokuwa ikikamilika na kuzinduliwa, ilidumu muda mfupi na kusababisha wananchi wa vijijini kuendelea na adha ya upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama. Aidha, miradi ilikuwa ikijengwa kwa gharama kubwa ikilinganishwa na uhalisia wa soko.

Huduma ya Maji Katika Kijiji cha Msomera, Handeni Tanga
Sambamba na utekelezaji wa mpango wa bajeti 2021/2022, kuliibuka pia uhitaji wa mradi wa maji kwa wananchi wa Kijiji cha Msomera Wilayani Handeni Mkoa wa Tanga ambacho wananchi kutoka Ngorongoro wanahamia kwa hiari.

RUWASA inatekeleza ujenzi wa mradi wa maji katika Kijiji hicho, ambapo mpango wa utekelezaji unafanywa kwa awamu kulingana na ujenzi wa nyumba zinazojengwa kwa ajili ya watu wanaohamia. Awamu ya kwanza na ya pili zimekamilika.

Kukamilika kwa awamu hizo kumewezesha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi wapatao 17,000 pamoja na mifugo yao na kupelekea idadi ya vituo vya maji kuongezeka kutoka 12 hadi kufikia vituo vya kuchotea maji 30 kwa matumizi ya binadamu na vituo 3 vya kunyweshea maji mifugo.

Aidha, katika kuboresho huduma ya maji katika Kijiji cha Msomera, Serikali kupitia RUWASA inaendelea na ujenzi wa bwawa la maji kwa gharama ya Shilingi bilioni 1.99 ambapo kwa sasa umefikia zaidi ya asilimia 50. Ujenzi wa bwawa hilo utakapokamilika, utasaidia kuboresha huduma ya maji kwa wananchi na mifugo yao pia.

Kwa sasa, kati ya vijiji vyote 12,319 nchini, ni vijiji 8,769 vinavyofikiwa na huduma ya uhakika ya majisafi na salama. Kwa mujibu wa tathmini iliyofanyika mwezi Aprili 2022, upatikanaji wa huduma ya maji vijijini ulikuwa umefikia kiwango cha asilimia 74.5 ikiwa ni ongezeko la asilimia 9.7 ikilinganishwa na wastani wa 64.8 mwaka 2019. Kwa mpango na kasi ya utekelezaji wa miradi, RUWASA inatarajia kuvuka lengo la asilimia 85 ifikapo mwaka 2025, kama ilivyoelekezwa na Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

**Mpango wa Utekelezaji wa Miradi kwa Mwaka wa Fedha 2022/23**
Katika mwaka huu wa fedha, yaani 2022/23, RUWASA imepanga kutekeleza jumla ya miradi 1,029, ambapo kati ya miradi hiyo 381 ni mipya na miradi 648 ni ile ambayo utekelezaji wake unaendelea kutoka mwaka wa fedha uliyopita. Kiasi cha shilingi 387,736,591,242 kimeidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo. Kukamilika kwa miradi hiyo, kutawezesha upatikanaji wa huduma ya maji vijijini kuongezeka kwa wastani wa asilimia 6 hivyo ifikapo Julai 2023 wastani wa upatikanaji wa huduma ya maji vijijini itakuwa 80.04%.

**Utekelezaji wa Miradi ya Maji kupitia programu ya Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi Dhidi ya UVIKO – 19**

RUWASA inaendelea na utekelezaji wa miradi ya maji kupitia fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya Ugonjwa wa UVIKO - 19. Kupitia Mpango huo, RUWASA inatekeleza miradi 172 katika maeneo mbalimbali ya vijijiji.

Utekelezaji wa miradi hiyo unagharimu Shilingi 78, 528,753,850. Vilevile katika Mkoa wa Songwe (eneo la miji) RUWASA inatekeleza miradi miwili (2) ya maji ya Uhuru - Tunduma (Mji wa Tunduma) na Mwansyana (Mji wa Vwawa) kwa gharama ya Shilingi 1,209,394,234.24 hii kupelekea RUWASA kutekeleza jumla ya Miradi 174 kwa gharama ya Shilingi 79,738,148,084.24.



Mkurugenzi Mkuu wa RUWASA Mhandisi Clement KIVEGALO (kulia) na Mkurugenzi wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Wizara ya Maji CPA. Joyce Msiru (kushoto) wakifungua koki ya maji wakati walipotembelea mradi wa maji wa Kimala ulipo Wilayani Kilolo Mkoa wa Iringa.



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI
WAKALA WA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI

RUWASA
Rural Water Supply and Sanitation Agency



Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akimtua ndoo ya maji kichwani mkazi wa Tanganyika mara baada ya uzinduzi wa mradi wa maji wa Sibwesa Wilayani Tanganyika Mkoa wa Katavi. Mradi wa maji wa Sibwesa umetekelezwa kwa fedha za Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO 19 na sasa unahudumia wakazi zaidi ya 7,000.

Ili kuendana na muda unaotakiwa kukamilisha utekelezaji wa miradi hii, ilionekana ni vyema utekelezaji ukafanyika wa aina mbili ambazo kwanza ni kufanya ununuzi wa Pampu na Bomba kwa pamoja kutoka kwa Wakala wa watengenezaji wa pampu na viwanda vya uzalishaji wa bomba na Pili kutumia wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maji (civil works). Miradi minne (4) tu inatekelezwa kwa kutumia utaratibu wa wataalam wa ndani (Force Account).

Hadi kufikia tarehe 30 Novemba, 2022 utekelezaji wa miradi hiyo umefikia hatua mbalimbali. Utekelezaji wa miradi hiyo kwa ujumla katika Mikoa yote 25 umefikia asilimia 94.38 ambapo miradi 70 imekamilika kwa asilimia 100 na miradi 104 ipo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji.

Miradi 154 kati ya 174 imeanza kutoa huduma ya maji kwa wananchi na miradi 20 bado haijaanza kutoa huduma kutokana na changamoto mbalimbali ambazo zinaendelea kupatiwa ufumbuzi ikiwemo kuchelewa kwa upatikanaji wa msamaha wa kodi, maunganisho ya umeme, na upatikanaji wa mita za umeme na transformer kubwa (100kVA) kutoka TANESCO.

Vituo 1714 vya kuchotea maji vilipangwa kujengwa ambapo hadi sasa vituo 1685 vimejengwa na vituo 1299 vinatoa huduma kwa wananchi na wateja wapatao 1361 wameunganishiwa maji majumbani.

**Udhibiti wa Gharama za Ujenzi wa Miradi ya Maji**
Kama inavyofahamika, hapo awali ujenzi wa miradi ya maji ulikuwa ukifanyika kwa gharama kubwa ikilinganishwa na uhalisia. Kwa kutambua hilo, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 RUWASA ikiwa katika mchakato wa kuajiri wakandarasi ilifanya majadiliano ya kina ya mikataba (Contract Negotiation) na wakandarasi kwa miradi 86, ambapo kupitia majadiliano hayo, RUWASA iliokoa fedha kiasi cha Sh. 57,405,177,725.22. Kabla ya majadiliano, gharama kwa miradi yote 86 ilikuwa ni Sh. 367,310,874,913.66. na baada ya majadiliano, gharama ilipungua hadi kufikia Sh. 309,905,697,188.44

**Mwelekeo Mpya Katika Utoaji wa Huduma ya Maji Vijijini**
Mojawapo ya changamoto kubwa iliyokuwepo kabla ya kuundwa kwa RUWASA ni huduma ya maji kutokuwa endelevu. Katika kuhakikisha skimu za maji zilizojengwa katika maeneo ya vijijini zinaendelea kutoa huduma ya maji kwa viwango vilivyokusudiwa, RUWASA tumechukua mwelekeo mpya kwa kufanya mambo yafuatayo:-

**Kuhakikisha kuwa CBWSOs Zinakuwa na Wataalam na Kuwajengea Uwezo**
Hadi sasa, RUWASA imefanikiwa kuunda CBWSOs 2,509, ambazo zimeajiri wataalamu wapatao 5,296. Kati ya hao, Mafundi ni 1,837, Wasaidizi wa Hesabu 1,529 na Wasaidizi wa Ofisi 1,930. Kuwepo kwa wataalam hao kumewezesha shughuli za kiufundi kufanywa kwa weledi zaidi ikilinganishwa na hapo awali, na hii imesaidia kuongeza uhakika wa huduma.

Wataalam hao watajengewa uwezo kwa kuwapatia mafunzo maalum (tailor-made training) na hivi karibuni RUWASA itakutana na Uongozi wa VETA Makao Makuu kuona namna ya kuingia makubaliano ya kudumu ya utoaji wa mafunzo maalum kwa watumishi wa CBWSOs.

Aidha, sambamba na ujenzi wa mradi wa maji, RUWASA imekuwa pia ikijiingiza kwenye gharama za mradi wa ujenzi wa ofisi ya CBWSOs, ununuzi wa vitendea kazi muhimu, malipo ya mishahara ya miezi 6 mpaka 12 kutegemeana na ukubwa wa skimu husika.

**Kuandaa Miongozo ya Uendeshaji wa Huduma ya Maji Vijijini**
RUWASA imefanikiwa kuandaa jumla ya miongozo 5 inayohusiana na uendeshaji wa huduma ya maji vijijini. Miongozo hiyo, ni Mwongozo wa Uunganishwaji wa CBWSOs (Guidelines for Clustering of CBWSOs), Mwongozo wa Ukokotoaji wa Bei za Maji (Guideline of Tariff Setting), Mwongozo wa Uendeshaji na Matengenezo ya Miradi (Operation and Maintenance Manual) na Muongozo wa Kujengea Uwezo (Training Manual). Katika mwaka huu wa fedha wa 2022/23, RUWASA itaanza kutoa mafunzo kwa wadau mbalimbali ili waelewe dhana ya CBWSO ikiwa ni pamoja na viongozi wa Serikali wa Mikoa na Wilaya. Kazi hii itafanywa na RUWASA kwa kushirikiana na Wizara ya Maji pamoja na Ofisi ya Rais TAMISEMI.

**Eneo la Ufundi**
RUWASA imepanga kuanzisha Timu za Utoaji wa Msaada wa Kiufundi katika ngazi ya Mkoa, ambazo zitakuwa na wataalam wa Kada zote muhimu kwa ajili ya kuhudumia CBWSOs. Vilevile, kila Mkoa utakuwa na Bohari ya Vipuli muhimu kwa ajili ya ukarabati wa miradi mbalimbali iliyopo ndani ya Mkoa.

Aidha, katika kuhakisha kuwa gharama za uendeshaji wa miradi zinapungua na huduma inakuwa endelevu, RUWASA inashirikiana na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na REA kubadilisha mifumo ya nishati ya uendeshati wa mitambo ya maji kutoka kwenye mfumo wa dizeli kwenda Mfumo wa Umemejua (solar power) na umeme wa TANESCO. Hadi sasa, jumla ya skimu 19 kati ya 74 za mikoa miwili ya Singida na Dodoma tayari zimebadilishwa kwa kufungwa umemejua. Kazi hii itaendelea kwa awamu kwa nchi nzima.

**Eneo la Usimamizi wa Fedha**
Katika kuboresha makusanyo ya maji, RUWASA imeingia makubaliano na Chuo Kikuu cha Arusha na Mbeya ya kubuni Dira za Malipo Kabla ya Matumizi (pre-paid meters), ambazo zitafungwa katika skimu za maji vijijini. Malipo ya maji yataunganishwa na Mfumo wa malipo wa Serikali uitwao GePG.

Katika Kudhibiti matumizi ya fedha, RUWASA imefungua Akaunti kila mkoa, ambazo zitapokea fedha za malipo ya mauzo ya maji. Fedha zilizokusanywa zitakuwa zikitumwa kwenda CBWSOs husika kwa awamu kutegemeana na mpango wa matumizi ulioidhinishwa.

**Bei Ukomo za Huduma ya Maji Vijijini**
Mwishoni mwa mwezi Juni, 2022, RUWASA ilitangaza bei ukomo za maji ambazo zimelenga kutatua changamoto uwepo wa bei kubwa ya maji, kwa mfano kabla ya kutangazwa kwa bei ukomo, ndoo moja ya maji ya lita 20 ilikuwa inauzwa kwa Sh. 100 kwa Skimu zinazotumia Dizeli. Baada ya bei ukomo kutangazwa, bei ya ndoo moja ya lita 20 ilishuka kutoka Sh. 100 hadi kufika Sh. 50. Vilevile, RUWASA itaendelea kufanya mapitio na maboresho ya ukomo wa bei za maji kila mwaka ili kuhakikisha bei za maji zinaendena na uhalisia wa gharama za uendeshaji kwa kipindi husika.

**"RUWASA – MAJI BOMBANI"**



Tangi la maji la mradi wa Nyamlenge Iringa uliyotekelezwa kwa fedha za Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya ugonjwa wa UVIKO 19 unahudumia zaidi wa wakazi 1675.

## CHARLES MASALAKULANGWA;

# Mkongwe aliyeanza shule akiwa na miaka 15, asimulia uzoefu ukoloni, hadi uhuru

**INATOKA UK. 14**

Shule ya Msingi Gambasingu kijijini kwao, wakifundishwa Kiswahili anachokiita 'cha kulazimishwa' na walimu wao waliokuwa wawili tu, akiwataja majina; Isack Ngasa, aliyefundisha Kiswahili na Joas Nkangaga wa hesabu.

Hapo anasifu zama hizo hazikuwapo lugha chafu shuleni na kwa anayebainika anapewa adhabu ya kuvaa kitu mithili ya 'black board'.

Ni wakati huo anasimulia mtu akihitimu darasa la nne anarudi nyumbani kuchunga ng'ombe, kulima, kuoa, au kama ni binti anaolewa wakishindwa mtihani wa kuingia darasa la tano katika shule ya Lalago Middle School iliyokuwa kijiji cha Lalago Maswa.

Anasema, kuna siku mchana akiwa darasa la sita, alikutwa na Mwalimu Mkuu shuleni akila chakula wali maharage huku kijiko ameweka chini, alimwamuru kumwaga chini chakula, jambo alililifanya shingo upande, akiumia sana nafsi yake, maana njaa ilimuuma sana.

Mwaka 1965 akahitimu darasa la nane shuleni Lalago, wakafaulu wanafunzi sita kati ya 45 kujiunga na Shinyanga Sekondari na baadaye mwaka 1967, akahamishiwa Shule ya Sekondari Ushirika wa Kahawa mkoani Kilimanjaro.

Anasimulia wanafunzi wengi walitoka kabila la wachaga na wasukuma jumla yao 45, mlo mkuu ukiwa samaki aina sangara na sato waliovuliwa kutoka Bwawa la Mungu.

**NUSURA AFUKUZWE SHULE**

Akiwa shuleni Kilimanjaro, anasimulia akanusurika kufukuzwa masomo na akakataa kulima kipande chake cha shamba walichokuwa wakipewa kila mmoja kulima kahawa.

Mwanafunzi kiongozi wa bweni alimtukana na kumfyonza, kijana huyo anasema ni baada ya kuchelewa kwenda shamba kulima kipande chake, hata akajisikia kafanyiwa hivyo, akagoma kulima.

Anasimulia usiku kiongozi wa bweni alitangaza bwenini kuwa amempa adhabu kusafisha choo cha bweni wiki nzima, kutokana na kugoma kulima sehemu yake ya shamba.

"Niliposikia usiku akitangaza (kiranja) kwamba mimi amenipa adhabu ya kusafisha choo cha bweni. Na mimi nikatangaza pale pale bwenini kuwa, wanafunzi (wenzake) wakiniona nakwenda chooni siyo kusafisha, bali kujisaidia," anasimulia.

Hapo ndipo wanafunzi wote wakaangua kicheko bwenini, kiongozi wa bweni akaenda kushitaki kwa mkuu wa shule na baada ya hapo, akaitwa na kuambiwa alale achapwe viboko na mkuu wa shule, akakataa akiomba kujua kosa lake kisha ajieleze.

Anasema, mwalimu mkuu aliamua kumwita karani wa shule na kumpa maagizo kumuandikia 'waranti' (waraka wa safari) kurudi nyumbani, lakini mkuu wa shule baadaye alikuwa ametoka kwake 'kujinyoosha' akiwa amesahau jukumu lake.

Mwanafunzi Masalakulangwa alipolala usiku, wazo likamjia kumfuata mkuu huyo asubuhi nyumbani kwake, alipofika akamwambia "jana ulisahau kusaini waranti yangu, nimekuja kukwambia, pia kuomba msamaha."

Hata hivyo, mkuu huyo wa shule akawa na hasira akamfukuza, ndipo Masalakulangwa akamtamkia anaondoka akishajua lengo lake hataki wanafunzi wasukuma mpaka atawamaliza wote.

"Kauli hizo zilimuuma sana mkuu wa shule, akanitazama akishikatama huku naondoka, akaniita akaniambia basi nenda darasani, ndiyo ikawa nusura yangu kufukuzwa," anasema.

Anasimulia baada ya mwaka 1970 alipomaliza kidato cha nne, alifanya mtihani wa kuhitimu na akachaguliwa kuwa Mkaguzi wa Pamba, baadaye akasomea fani hiyo.

Ilkuwaje? Muda mfupi mwaka 1972 akasikia matangazo kanisani likiwa ni cha kiwanda cha uchapishaji kumteua kwenda kusomea taaluma ya uchapishaji miaka mitatu, kati ya 1972 hadi 1974 na alipohitimu akaendelea na masomo nchini Marekani miaka minne, kati ya mwaka 1974 hadi 1978.

**BAADA UHURU**

Baada ya kupatikana Uhuru wa Tanganyika mwaka 1961, anamsifu Rais Julius Nyerere kufanya kazi kubwa ya kujenga utaifa nchini, lugha ya Kiswahili ikikuzwa, kufutwa udini na ukabila, huku kukikuzwa umoja kwa namna nyingi.

Masalakulangwa anakumbusha kuwapo chama cha upinzani chini ya Zuberi Mtemvu, kabla ya kuingia mfumo wa chama kimoja mwaka 1964, pia anaukumbuka urafiki Rais Nyerere na Rais John F. Kenedy wa Marekani.

Mzee huyo anashuhudia misaada iliyomiminika nchini na kuanzia miaka ya 1964/1965, Tanzania ikawa rafiki mkubwa na China, nchini kukiwapo siasa za Ujamaa na Kujitegemea na sera kimataifa 'kutofungamana na upande wowote.'

Anarejea mwaka huo 1964 Tanganyika na Zanzibar ziliungana kuunda Tanzania, Nyerere akiwa Rais na Makamu wake Abeid Karume.

Pia anashuhudia baada ya hapo kukafanyika Azimio la Arusha mwaka 1967, mali binafsi kama majengo, mashamba, benki na viwanda kugeuzwa kuwa vya umma.

Anataja mageuzi ya vijiji vya ujamaa vingi alivyoshudia vilitajirika, akitoa mfano kijiji cha Nyangili wilayani Busega, Simiyu,wakati huo ilikuwa Magu, mkoani Mwanza kuwa na miradi ya maduka makubwa na kumiliki mabasi.

Hata hivyo, anasema baada ya miaka mingi vijiji vingi vilianza kuyumba na kufilisika mali, hata wakazi kuangukia maisha magumu.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI
SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA (TASAC)
Imethibitishwa:ISO 9001: 2015

Maadhimisho ya Miaka 61 ya Uhuru
TUKO HURU
Tuulinde, Tuuheshimu, Tuuthamini na Tuudumishe Uhuru Wetu.
1961 - 2022



Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), Tunaungana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan na Watanzania wote katika kuadhimisha **Miaka 61 ya Uhuru wa Tanzania Bara.**

217186602

Jengo la PSSSF Tower, Sakafu ya 7 na 8, Kiwanja Na. 20/21, Mtaa wa Garden/ Ohio
S.L.P 989, Dar es Salaam- Tanzania, Simu: +255 222 127 314, Nukushi: +255 222 127 313
Barua pepe: dg@tasac.go.tz, info@tasac.go.tz, Tovuti: www.tasac.go.tz




## MIAKA 10 YA e-GA:

# Serikali Mtandao inavyotekelezwa kwa vitendo

Kutokana na mabadiliko makubwa ya sayansi na teknolojia yanayotokea duniani, ni ukweli usiopingika kwamba kama serikali na Taasisimbalimbali duniani hazitakwenda sambamba na mabadiliko hayo zitabaki nyuma kwenye maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Mabadiliko hayo ndio yameibua msemo maarufu wa "dunia ni kijiji" hii ni kutokana na ukweli kwamba kwa matumizi ya teknolojia mtu anaweza kupata taarifa kwa haraka na kwa urahisi kupitia mtandao wa intaneti. Vivyo hivyo, serikali na Taasisimbalimbali duniani kote zinatumia mtandoa wa intaneti kuendesha shughuli zake kupitia mifumo maalumu iliyojitengenezea.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Taasisizake haijabaki nyuma katika matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku.

Kupitia Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), serikali imeweza kutengeneza mifumo mbalimbali ya kiutendaji na ya utoaji wa huduma kwa jamii ambayo si kwamba imeongeza tu ufanisi katika utendaji wa Serikali, pia imeongeza ufanisi na kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi, wageni na wafanyabiashara.

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Mhandisi. Benedict Ndomba ameeleza kuwa e-GA imetekeleza shughuli mbalimbali tangu kuanzishwa kwake miaka 10 iliyopita, ambazo zimeleta ufanisi mkubwa kwa Serikali na Taasisizake.

"Katika kipindi cha miaka 10, Mamlaka imeweza kutekeleza jukumu lake la msingi la kuratibu, kusimamia na kukuza jitihada za Serikali Mtandao pamoja na kuhimiza utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao kwa Taasisiza Umma", amefafanua Ndomba.

Mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka 10 ni pamoja na kusimamia kikamilifu usalama wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA na kuwezesha kubaini na kukabiliana na matishio ya kiusalama mtandaoni, sambamba na kufanya ukaguzi na tathmini za usalama wa mifumo kwa Taasisimbalimbali za Umma na kusimamia uzingatiaji wa sheria na kanuni, pamoja na viwango na miongozo ya Serikali Mtandao iliyoandaliwa ipatayo 52. Miongozo hiyo inapatikana kupitia tovuti ya e-GA ambayo ni **www.ega.go.tz**

Aidha, Mamlaka pia imeweza kupokea, kupitia na kutoa ushauri kuhusu utekelezaji wa miradi mbalimbali ya TEHAMA kutoka kwa Taasisiza Umma zipatazo 223, na mafunzo ya uzingatiaji wake yapatayo 263 kwa Taasisimbalimbali za Umma.

Mhandisi. Ndomba ameyataja mafanikio mengine yaliyopatikana katika kipindi cha miaka 10 ni pamoja na kujenga na kusimamia uendeshaji wa vituo vya Serikali vya kuhifadhi mifumo na taarifa, ambavyo hadi sasa



**Mkurugenzi mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) Mhandisi Benedict B. Ndomba akielezea jinsi Serikali ilivyorahisisha upatikanaji wa huduma kupitia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)**

vinatumiwa na Taasisi121 kuhifadhi mifumo na taarifa zao kwa usalama wa uhakika, na ujenzi na usimamizi wa mtandao wa mawasiliano wa Serikali ambapo hadi sasa Taasisi 299 zimeunganishwa na kuwezeshwa kuwasiliana chini ya uratibu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao.

Aidha, Mamlaka kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali za Umma, imesanifu, kujenga na kusimamia uendeshaji na matumizi ya mifumo tumizi 34, mifumo shirikishi 13 na mifumo ya kisekta 20. Mifumo kama vile: Mfumo wa malipo ya serikali (GePG), Mfumo wa Barua pepe kwa Serikali na Taasisizake (GMS), mfumo wa Ankara za Maji (MAJIIS), mfumo wa taarifa za watumishi na mishahara (New HCMIS), nk.

Kutokana na maendeleo ya teknolojia na ongezeko la matumizi ya simu za kiganjani, mamlaka pia imesanifu, kujenga na kusimamia uendeshaji wa mfumo wa serikali wa kutolea huduma kwa njia ya simu za mkononi (Government Mobile Platform), ambapo hadi sasa Taasisimbalimbali za Umma zinautumia na kuwezesha mifumo ya TEHAMA 236 kutoa huduma kupitia simu za mkononi kwa kutumia arafa na USSD menyu *152*00#, mfano ni malipo ya LUKU, GePG na Ankara za Maji, malipo ya ardhi, nk.

"Ni muhimu ikumbukwe kwamba, hatua hizo zinaenda sambamba na utoaji wa ushauri wa kitaalamu na msaada wa kiufundi katika utekelezaji wa Serikali mtandao ambapo huduma hiyo inatolewa na maafisa wa e-GA kwa kushirikiana na maafisa wa Taasisiza serikali", amesema Ndomba.

Aidha, ili kufanya huduma za serikali mtandao ziwe endelevu na kuendana na kasi ya ukuaji wa teknolojia, Mamlaka inafanya shughuli za Ubunifu, Utafiti na Mafunzo katika kityuo chake cha Dodoma. Aidha, jitihada zinaendelea ili kupanua huduma za kituo hicho.

Kupitia kituo hicho, Mamlaka imeshirikiana na Taasisiza elimu ya juu na zile za ubunifu ambapo tafiti zipatazo 13 kwa ajili ya kutambua vipaji na ubunifu kutoka kwa vijana wanaosoma au waliomaliza elimu ya juu zimefanyika na wanafunzi 125 wameshiriki hadi sasa.

Katika jitihada za kutatua changamoto, ambazo Taasisiza Umma wanakumbana nazo katika utekelezaji wa serikali mtandao, Ndomba amesema kwamba, Mamlaka imetoa msaada wa kitaalamu kwa Taasisiza Umma 602 zinazotumia huduma za serikali mtandao kupitia dawati la msaada.


"Pamoja na mafanikio ambayo yamepatikana mpaka sasa, Mamlaka imepanga kuendelea kutekeleza shughuli za usimamizi wa usalama wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA, kuchukuwa hatua za kupunguza wingi na urudufu wa mifumo na kuiwezesha kuwasiliana na kubadilishana taarifa, kubuni njia mpya za serikali mtandao hasa kupitia simu za mkononi, pamoja na kuendelea kuhimiza uzingatiaji wa sheria, kanuni, viwango na miongozo ya serikali mtandao katika Taasisiza Umma".

Ili kuwezesha mifumo kubadilishana taarifa, Mamlaka imejenga mfumo wa Government Enterprise Service Bus (GovESB) mfumo huu unawezesha mifumo mbalimbali kubadilisha taarifa, ambapo TaasisiZaidi ya 40 zimeanza kubadilishana taarifa kupitia mfumo huu, amesema Ndomba.

Pia, Ndomba amebainisha kwamba Mamlaka inalenga kuhakikisha kuwa inasimamia uongezaji wa mawanda ya miundombinu ya Mtandao wa Mawasiliano Serikalini ili kuweza kuunganisha Taasisizilizo katika Mikoa yote na Wilaya zote kupitia fedha za mradi wa Tanzania ya Kidijitali (Digital Tanzania Project – DTP) na kuongeza uwezo wa vituo vya kuhifadhi mifumo na taarifa ili viweze kutumiwa na Taasisizote za Serikali ili kuongeza tija na ufanisi na kuhakikisha usalama wa taarifa za Serikali.

Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) ni Taasisiya Umma iliyoanzishwa kwa Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya mwaka 2019. Ni Taasisiyenye mamlaka ya kuratibu, kusimamia na kukuza jitihada za Serikali Mtandao pamoja na kuhimiza utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao kwa Taasisiza Umma.

Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya mwaka 2019 imeainisha majukumu na mamlaka yanayoiongoza Mamlaka ya Serikali Mtandao katika utekelezaji wa Serikali Mtandao nchini Tanzania. Sheria ya Serikali Mtandao inapatikana kupitia tovuti ya Mamlaka **www.ega.go.tz**




**Mfumo Mkuu wa Ubadilishanaji Taarifa (Government Enterprise Service Bus ) GovESB**



# Mzee Butiku aja na hoja kurejea mbinu za Nyerere

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

NI miaka 23 ya kumbukumbu ya kifo cha Mwalimu Julius Nyerere ambaye ni muasisi wa taifa la Tanzania.

Hivi karibuni kumekuwapo kelele nyingi za ukosefu wa maadili na malezi ni ishara tosha kuwa taifa linapaswa kujitafakari katika kumuenzi Mwalimu Nyerere.

Aliyekuwa Msaidizi binafsi wa Mwalimu Nyerere wa masuala ya Utafiti na sasa, Mkurugenzi wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere, Mzee Joseph Butiku, akizungumza kwenye mjadala wa kitaifa wa wazee jijini Dodoma mwanzoni mwa mwezi huu, anasema ni wakati wa kuwa na jukwaa la maadili la utaifa ambalo wazee wanapaswa kuliunda.

“Taasisi ya Mwalimu Nyerere tunakusudia kuunda kwa kuwa wazee ndio msingi wa jukwaa hili, ili kuelea vijana, tutakuja kwenu(wazee) tupate maoni yetu kwa ajili ya jukwaa la uzalendo, tusipokuwa na tabia ya kutekeleza ni kazi bure.”

“Kama huna serikali makini ni bure, kama una wazee waoga ni bure, kama una wazee wanasimanga simanga serikali ni bure, jukwaa hili litasaidia kuongoza taifa vizuri kuwa watu Watanzania,”anasema.

Anasema vijana wanatakiwa kuwa kama Mwalimu Nyerere katika kuheshimu wazee wao na kusimamia utu na haki sawa kwa wote.

“Shida yetu wote ni tabia, wazee simamieni tabia bila kuogopa, sasa hili kundi la wazee uzee ndio watu, misingi inasimamiwa na wazee, tunataka wazee wanaosimamia misingi, tumeshindwa kusimamia misingi,”anasema.

Anadems: “Tumeshindwa kulea, tumemsikia mama Samia(Rais Samia Suluhu Hassan) anasema njooni tushirikiane tulee, tunashindwa tunakabidhi polisi wanakurupushana na ‘Panya Road’, piga hao nyie mnashukuru, hivi ni binadamu gani wanatengeneza bunduki kuua watoto wao, wameshindwa nini?”.

“Wale watoto msiwalaumu ni sisi, mtoto umleavyo ndivyo akuavyo, nani kawalea hao? katika mfumo wetu wa Afrika, tunasema huyu binti wa nani ana tabia mbaya, huyu kijana wa nani hastahili kuwa hivyo, wote tunajua amekosea kwasababu ule mfumo wa maadili tunaufahamu wote tumefundishwa.

“Wale wanaoiba ni watoto wa nani kwa hiyo kazi nyingine yetu sasa ni kulea vijana bila kubabaisha, bila unyonge, Rais ni mtu, urais anatoa kwetu sisi wazee, wazee kwanza ndio watetezi wa misingi,” anasema.



Mzee Joseph Butiku. **PICHA: MAKTABA.**

Anahimiza malezi kwa watoto na kwamba taasisi inaona kuna umuhimu wa kuundwa jukwaa hilo.

“Wazee, vijana na watoto tuunde jukwaa la uzalendo litakalolinda misingi yetu, na sisi wazee tusimamie kulea watoto, tujue tufundishe nini wakati gani na vijana wetu watatusikiliza na madaraka tutawapa hatutataka kuwanyang’anya sisi ni washauri,” anasema.

Anasema katika kuchagua viongozi wazee, wana kauli kubwa katika jamii huko wanaoitwa viongozi wa jamii.

“Mimi nataka kuwa Rais wa nani? Sina nguvu hizo, wazee wanataka kukaa kwenye mabaraza? Mbaki wazee, nchi ikishindwa ni nyinyi sio kwenda kutafuta vyeo vingine cheo cha maana ni cheo cha mzee simamie, muulize Rais, Waziri kwaini hili haliendi vizuri.”

“Kwa sababu tumechagua watu bungeni yupo mwanasheria wa serikali anasimamia katiba yetu kama kuna mapungufu kusahihisha ni rahisi na sio ubishi wa wazungu huko waliibiana mali wakajenga uhasama wa kudumu na leo ndivyo walivyo wanyang’anyi na wezi,” anasema.

Anasema wazee wakiwa waoga kusaidia vijana wasinyang’anywe watakuwa wamekwisha.

“Jukwaa la uzalendo msingi wake uchumi, mama anasema kilimo, viwanda, umeme, hayo ndio ya msingi, sisi tunasema katiba ipo, tukiacha wizi na kufundisha kunyang’anyana.

“Kama chuo kikuu kitatoa vijana hawana tafsiri ya maisha ya leo kama walivyokuwa nayo kina Nyerere basi hatuna taifa, kama chuo hakitafundisha utu na watu na kujitegemea watafundisha watu waporaji walioelewa misingi ya wazee wao litakuwa taifa bora,” anasema.

Anafafanua kuwa dunia haiwezi kufundishwa kwa silaha bali kwa moyo wa upendo na kwamba amani,usalama, maadili na tabia kwa watanzania hilo ndilo taifa.

“Leo mahitaji yameongezeka Mwalimu Nyerere na wenzake walisimamia utu sawa, haki sawa kwa wote na ilikuwa misingi ya wazee wao, katiba haijaandika ukiwa kiongozi ule rushwa au kunyang’anya mali za wenzako, wewe useme wazee wamepitwa na wakati hii ni tabia mbaya,”anasema.

Butiku anasisitiza kazi ya wazee ni kusimamia misingi ya utu bila kubabaika.

**VIJANA WAFUNDISHWE KAZI**

“Ujamaa wa Mwalimu Nyerere ni kujihudumia mahitaji yetu, kuna kelele nyingi hakuna hela, Mungu ametupa akili tufanye kazi na kazi yetu ya msingi tangu mababu na mababu ni kulima kuwa na chakula.”

“Kwa kuwa tumestaraabika, tulime kisasa na mazao yetu yaendelee katika viwanda na tuzalishe mahitaji yetu tutumie na mengine tuuze tupate fedha na tuwafundishe vijana wetu kazi, ”anasema.





# Matukio 336 ya ubakaji yaripotiwa miezi 10

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MATUKIO 336 ya ubakaji yameripotiwa mkoani Mbeya, katika kipindi cha kuanzia Januari mpaka Oktoba mwaka huu.

Takwimu hizo zilitolewa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alipotoa taarifa ya maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia nchini ambayo huadhimishwa kila mwaka kuanzia Novemba 25 mpaka Desemba 10.

Homera alisema idadi hiyo inaongoza kwa matukio ya ukatili wa kijinsia ndani ya mkoa huo ambako yamejitokeza zaidi ya matukio 550 yaliripotiwa katika kipindi hicho yakihusisha ukatili wa aina mbalimbali.

Alisema matukio mengine ya ukatili wa kijinsia yaliyojitokeza ni kama vile, vipigo kwa kina mama, ukatili wa kiuchumi na ukatili wa kisaikolojia.

Alifafanua kuwa kati ya matukio hayo, makosa ya kulawiti ni 54 shambulio la kudhuru mwili 35, shambulio la aibu 32 na kutelekeza familia 29.

"Tayari kesi 189 zilifikishwa mahakamani ambapo kesi 11 watuhumiwa walifungwa jela maisha, kesi tisa walifungwa miaka 30 na kesi 25 walihukumiwa vifungo mbalimbali huku kesi 136 zikiendelea na upelelezi na kesi 75 zimefungwa polisi kwa kukosa ushahidi," alisema Homera. Hivyo aliwataka wadau wote nchini kuhakikisha ukatili wa kijinsia hasa ubakaji unatokomezwa kwa kuhakikisha ushahidi unakamilika unapopelekwa mahakamani.

Subira Mwankusye (21) mkazi wa Jiji la Mbeya kutokana na hali ya uchumi kuwa mbaya nililazimika kuingia kwenye mahusiano ya kimapenzi ili kupata fedha za kujikimu.

Alisema alimpata mtoto wake ambaye alikuwa tayari kumhudumia lakini alikuwa muathirika wa maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi ambapo hapo baadae alibaini baada ya yeye kuanza kuumwa.

Alisema kitendo hicho alikichukulia kuwa miongoni mwa ukatili wa kijinsia kwani huyo mwanaume alimlaghai kwa fedha na kumharibia ndoto za maisha yake.













## Wanafunzi wenye ulemavu waomba wazazi kuadhibiwa

**Na Peter Mkwavila,** MPWAPWA

WANAFUNZI wenye ulemavu wa Shule ya Sekondari Mpwapwa wameiomba serikali kuwachukulia hatua kali za kisheria wazazi na walezi wanaowanyima watoto wao haki ya msingi ya kuwaandikisha shule.

Walitoa ombi hilo juzi wakati wakizungumza na waandishi wa habari.

Mmoja wa wanafunzi hao Meshack Ngiluduu, alisema serikali inatakiwa kuwachukulia hatua kali za kisheria wazazi na walezi hao wanaowakwamisha watoto hao kielimu na kuwasababishia umasikini kwenye maisha ya kila siku.

Ngiluduu, ambaye ni mwanafunzi wa kidato cha tano mwenye ulemavu wa kutoona, alisema kuwa bado kuna baadhi ya wazazi na walezi hawajandokana na dhana potofu iliyojengeka miongoni mwao kuwa kumsomesha na kumwendeleza kielimu mtoto ni kupoteza muda,mali na fedha.

Alisema kuwa bado kuna wazazi na walezi wanaoishi na watoto ambao ni walemavu hawako tayari kuwasomesha na kuwaendeleza kielimu kwa madai ya kutoona faida yoyote watakayoipata kwenye familia husika.

Aidha alisema watoto hao pamoja na ulemavu walionao wana haki sawa ya kupata elimu kama ilivyo kwa watoto wengine, ukizingatia kuwa walio wengi wamekuwa wakifanya vizuri darasani kushinda hata ambao wako vizuri kimaumbile.

"Kwa niaba ya wanafunzi wezangu ambao tuna ulemavu wa aina mbalimbali tuliopo madarasani na wale ambao wanahitaji kusoma lakini wamenyimwa fursa ya kupata elimu, tunaiomba serikali iwachukulie hatua wazazi wasiotaka kuwasomesha na kuwaendeleza kielimu watoto wao,"Ngiluduu alisisitiza.

Mratibu wa Mradi wa Elimu Jumuishi kutoka Kanisa la Free Pentecostal Church of Tanzania (FPCT), Janne Mgidange alisema kuwa elimu bado inahitajika kwa jamii inayoishi na watoto hao.

Alisema kuwa baadhi ya wazazi na walezi ambao wana watoto wenye ulemavu wanamawazo kuwa kumsomesha na kumwendeleza mtoto kielimu wanapoteza mali zao.

Mgidange alisema kutokana na dhana serikali kwa kushirikiana na taasisi, mashika, wameendelea kutoa elimu ambayo wazazi na walezi wenye watoto hao wataweza kubadilisha mtizamo huo na hatimaye wakawapeleka shule.

Hata hivyo aliwataka wazazi na walezi wenye watoto wanaosoma kuwajibika katika malezi na mahitaji ili waweze kufanya vizuri kimasomo itakayowasababishia kupata alama nzuri zaidi.

# Naibu Waziri akerwa kusuasua ujenzi zahanati

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange ameeleza kutoridhishwa na ujenzi wa Zahanati ya Manchali B iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma.

Hivyo, amewaagiza watendaji kujitathimini na kuchukua hatua.

Alitoa maagizo hayo juzi alipofanya zaiara ya kukagua ujenzi wa zahanati hiyo katika Halmashauri ya Chamwino Kijiji cha Manchali B.

Akiwa katika zahanati hiyo aliwataka watendaji wa halmashauri hiyo kuwa na utaratibu wa kujifanyia tathmini ya utendaji kazi kwani ni muda mrefu wamekaa na fedha za kuendeleza ujenzi bila sababu za msingi.

"Hili ni tatizo kubwa kama tunaweza kukaa na Sh.milioni 50 ya zahanati kwa zaidi ya miezi 12 bila kukamilisha, nafikiri tunahitaji kujitathmini na kuchukua hatua, wananchi wanasubiri, Rais Samia Suluhu Hassan ameleta fedha sisi kazi yetu ni kutekeleza na kuhakikisha miradi imekamilika na wananchi wanaanza kupata huduma" alisema Dk. Dugange.

Hivyo alimtaka Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Dk. Semistatus Mashimba, kumweleza wamejipangaje ili itakapofika Desemba 12, mwaka huu zahanati nne zilizopatiwa fedha ziwe zimekamilika ili kuanza kutoa huduma ya afya kama inavyotarajiwa.

Hata hivyo Dk.Mashimba alisema maelekezo yote wameyapokea na kwamba watayafanyia kazi ili zahanati hizo zianze kutoa huduma kwa wananchi katika muda uliopangwa.

Mganga Mkuu wa Mkoa, Dk. Best Magoma alisema katika mwaka wa fedha 2021/22022 Mkoa wa Dodoma ulipatiwa Sh. bilioni 1.3 kwa ajili ya uendelezaji zahanati.

Alisema matarajio ni kuona ifikapo Desemba 30 mwaka huu miradi yote iwe imekamilika lakini pia katika mwaka 2022/2023 Mkoa wa Dodoma umepata Sh. milioni 550 kwa ajili ya zahanati 11 na Halmashauri ya Chamwino wamepatiwa zahanati mbili zitakazojengwa.

Awali Ofisa Afya wa Wilaya ya Chamwino, Peter Athuman, akisoma taarifa ya Zahanati ya Kijiji cha Manchali B inayojengwa kwa gharama ya Sh.milioni 93.5 alisema ujenzi wa jengo hilo unahusisha nguvu za wananchi.

Alisema Sh. Milioni 3.5 zimehusisha ukusanyaji wa mawe, mchanga na kokoto, mapato ya ndani ya halmashauri Sh.milioni 10 na sh.milioni 50 fedha kutoka serikalini

Diwani wa Kata ya Manchali, Nelson Mtundu, aliishukuru serikali kwa kuwapatia fedha za ujenzi wa zahanati pia aliomba kuwajengea kituo cha afya ili kusogeza huduma kwa kuwa kata yake inavyo vijiji vitano ambavyo havina kituo cha afya.



Mkuu wa Kitengo cha Huduma ya Jamii Ubalozi wa Uingereza, Getrude Mapunda (wa pili kushoto) na Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Stanslaus Choaji (wa tatu kushoto), wakikata utepe kuzindua ofisi za mradi wa Shule Bora mkoani humo juzi. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Jeshi la Magereza kuchukua taarifa za wafungwa kidijitali

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Magereza lipo katika mchakato wa kuanzisha mfumo wa kielektroniki wa uchukuaji wa taarifa za wafungwa na mahabusu ili kuimarisha utendaji na kuondoa malalamiko kwa wananchi.

Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza, Mzee Nyamka, alieleza hayo jana wakati akifungua mafunzo ya kuwajengea uwezo maofisa magereza, askari na watumishi raia kuhusu Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Alisema kuwa, Jeshi hilo litakuja na mfumo wa uchukuaji wa taarifa za wafungwa na mahabusu na hiyo ni kutaka kupunguza msongamano wa mahabusu ikiwamo kuepusha malalamiko.

"Tulijaribu kuwa na mfumo huu awali lakini haukuendelea kwa vile tulikuwa bado hatujajipanga vizuri lakini sasa mfumo huo utakapokamilika utasaidia sana kuboresha utendaji," alisema Nyamka

Alisema katika mwaka wa fedha 2022/2023, serikali imelitengea Jeshi la Magereza Sh. bilioni tano kwa ajili ya kufunga vifaa vya vya upekuzi pamoja na kamera za ulinzi (CCTV).

Álisema kuwa baada ya mfumo huo kufungwa vilio vya wabunge vitapungua kutokana na kulalamikia mfumo huo uwepo.

"Mara nyingi vilio vya wabunge vilikuwa ni Jeshi la Magereza kuja na mfumo wa kisasa ili kuondokana na mfumo wa upekuzi tulio nao,"alisema Nyamka.

Alisema Jeshi la Magereza hilo lipo mstari wa mbele kuendana na kasi ya mabadiliko ya TEHAMA.

Álisema kuwa kitengo cha TEHAMA makao makuu ya Jeshi kimekuwa mstari wa mbele kuhakikisha kinatoa huduma kwa vitengo vingine ili kufanikisha shughuli za kila siku kwa kuzingatia sheria ya nchi.

Nyamka alisema katika mwaka huu wa fedha mfumo wa matumizi ya ofisi mtandao yataanza, mfumo huo utapunguza gharama za matumizi ya karatasi na kutoa huduma kwa haraka na ufanisi.

"Kila mtumishi kupatiwa barua pepe ya serikali na kuacha kutumia barua pepe binafsi na zoezi hilo limeanza kwa wanasheria wote wa Jeshi la Magereza na awamu itakayofuata ni watumishi wote wa Jeshi hilo," alisema.

Nyamka alisema pia Jeshi la Magereza litakuwa na kanzi data ya pamoja iliyounganishwa na mfumo wa utumishi hilo litarahisisha kupata taarifa za watumishi kwa haraka na kwa usahihi.

"Mafunzo haya yanasaidia kujenga uelewa, bajeti iliyopo haitoshelezi, tutakapopata fedha zaidi watakaopata mafunzo wataongezeka," alisema.

Nyamka alisema ufinyu wa bajeti umesababisha kutoweza kufikia malengo ila juhudi zipo na zinaonekana. Alisema kuwa magereza mengi nchini hayana vitendea kazi vya kisasa vinavyoendana na teknolojia ya sasa.





# Wataka ushirikishwaji wanahabari utungaji sheria

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WADAU kutoka asasi za kiraia na za Serikali wamesema kuwa kuna haja ya ushirikishwaji kwa waandishi wa habari katika michakato ya utungaji ama uboreshwaji wa sheria mbalimbali.

Walisema hayo jana katika Ofisi za Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Tunguu Zanzibar katika kikao cha kuzipitia na kutoa maoni yao kwa baadhi ya sheria ikiwamo Sheria ya Tume ya Uchaguzi, Sheria ya Habari na Sheria ya Takwimu Zanzibar.

Juma Khamis kutoka Jumuiya ya Waandishi wa Habari za Maendeleo Zanzibar, alisema kuna baadhi ya sheria zinazoleta mkanganyiko katika utekelezaji wake huku baadhi zikionekana kuminya uhuru wa habari.

"Ili kuepuka haya ni vyema sisi waandishi wa habari tukashirikishwa kikamilifu tangu hatua za awali kwenye uundwaji wa sheria ili kutoa maoni yetu pale tunapoona hapatakua sawa hususani katika utendaji wetu wa kazi"alisema.

Mwandishi wa Habari Mwandamizi Zanzibar, Salim Said Salim, alisema kuna baadhi ya sheria ni za ajabu na kutolea mfano kipengele cha Sheria ya Uchaguzi kinachomkataza mwandishi wa habari kutojumuisha matokeo ya uchaguzi yaliyobandikwa ukutani katika vituo vya kupigia kura, matokeo ambayo tayari yamewekwa kwa ajili ya umma na maofisa wenyewe wa tume hiyo.

Alisema kipengele hicho cha sheria kinakiuka uhuru wa habari na kuwanyima taarifa wananchi na kueleza kuwa kuna haja ya kufanyiwa marekebisho ya haraka ili waandishi wa habari kufanya kazi zao kwa mujibu wa sheria.

"Kwa kuwa maofisa wenyewe wa tume ya uchaguzi ndiyo waliojumlisha na kubandika matokeo ya kura kwenye vituo huku karatasi hizo zikiwa tayari zimetiwa saini za wahusika kwanini mwandishi wa habari azuiwe keshiria kufanya kazi yake ya kutoa taarifa hizo za idadi ya kura husika kutoka kwenye vituo"alisema.

Akichangia katika mkutano huo mwandishi wa habari kutoka Shirika la Magazeti ya Serikali Tanzania (TSN), Issa Yussuf, alisema kuna haja ya wanaohusika uandaaji na urekebishaji wa sheria kuratibu mpango mzima wa awali wa kukusanya maoni ya wananchi kabla ya kufikisha miswaada katika Baraza la Wawakilishi.

Mratib wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), Shifaa Said Hassan, alisema kuwapo kwa sheria bora katika nchi zitasaidia kuleta usawa na demokrasia.

Mtatibu huyo alisisitiza umuhimu wa kufuata na kutekeleza kwa vitendo mikataba ya kikanda na kimataifa ambayo nchi imeridhia ni jambo la msingi na linalopaswa kutiliwa mkazo zaidi.

Mkutano huo uliandaliwa na TAMWA Zanzibar kwa kushirikiana na Internews Tanzania uliokua na lengo la kupitia baadhi ya Sheria Zanzibar na kutoa maoni yao juu ya yale wanayoona yanahitaji kufanyiwa marekebisho.



Wadau kutoka taasisi mbalimbali za Serikali na kiraia, wakionyesha kuunga mkono kwa pamoja maazimio ya mkutano wa kikao cha kuzipitia na kutoa maoni yao kwa baadhi ya sheria ikiwemo Sheria ya Tume ya Uchaguzi, Sheria ya Habari na Sheria ya Takwimu, katika mkutano ulioandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Matukio ya ulawiti, ubakaji Zanzibar yashika kasi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

IDADI ya matukio ya udhalilishaji hasa ya ulawiti na ubakaji yanaongezeka kila mwezi visiwani Zanzibar, licha ya juhudi kubwa zinazochukuliwa za kupambana na vitendo hivyo nchini.

Hayo yalisemwa jana Mjini Unguja na Ofisa Takwimu kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali katika kitengo cha makosa ya jinai na jinsia, Ramla Hassan Pandu wakati akiwasilisha ripoti ya matukio hayo ya miezi kumi ya mwaka 2022.

Alisema kwa mujibu wa takwimu hizo zinaonesha kuwa Wilaya ya Magharibi B Unguja, inaongoza kwa kuwa na matukio 207 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia ambapo kesi 89 za ubakaji na 31 za kulawiti watoto wadogo waliokuwa na umri wa miaka 12 hadi mwaka mmoja.

Alisema hali ya matukio ya vitendo hivyo, inasikitikisha na waathirika wakuu ni watu wenye ulemavu pamoja na watoto wadogo ambao ndiyo tegemeo kubwa la baadae, hivyo jitihada zaidi zinahitajika katika kupambana na matukio hayo.

Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Jamii kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wazee na Watoto, Mohamed Jabir Makame akiwasilisha mada ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia alisema Serikali ya Zanzibar inasimamia utekelezaji wa mpango kazi wa kitaifa wa kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa mwaka 2014 hadi 2022.

Aidha alitaja sababu zinazopelekea kuwapo kwa matendo hayo ikiwamo kuvunjika kwa ndoa, tamaa na matumizi mabaya ya simu hasa kwa vijana na watoto.

## Watu wenye ulemavu walia kutoingizwa katika mpango

**Na Mwandishi Wetu**

WATU wenye ulemavu wametoa kilio chao kuhusu kutoingizwa katika masuala ya watu wenye ulemavu katika Mpango wa Serikali ya kitaifa wa Kumaliza vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto (NPA) wa mwaka 2017-2022.

Walieleza kilio hicho jana Mjini Zanzibar katika mkutano maalumu wa kuelezea mpango huo kwa watu wenye ulemavu.

Yumna Mmmangak utoka Jumuiya ya Wanawake Wenye Ulemavu, alisema mpango huo haukuyafikia mahitaji ya watu wenyeulemavu kutokana na kutoingizwa masuala yanayowahusu na badala yake kuingizwa zaidi masuala ya wanawake na watoto.

Alisema katika mpango huo takwimu za matukio ya udhalilishaji haziwasemei watu wenye ulemavu na badala yake zinawasemea wanawake na watoto tu, pamoja na kutozingatia utekelezaji wa ahadi za nchi kwa watu wenye ulemavu.


Fatma Chesa kutoka Jumuiya ya Wasiona, alisema ni vyema mpango huo uandaliwe upya na kuomba kuainishwa kwa takwimu za watu wenye ulemavu na kusisitiza nyenzo zitumike katika kuonesha mahitaji.

Aidha alishauri kuongezwa kwa bajrti kwa ajili ya mahitaji ya watu wenye ulemavu pamoja na kuangaliwa kwa ukaribu zaidi takwimu za ajira ambazo haziendani na hali halisi ya mahitaji ya watu wenye ulemavu.

Akiwasilisha mada ya hali ya watu wenye ulemavu katika mpango wa NPA, Mhadhiri kutoka Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Dk. Masoud Hemed Nassor, alisema mpango huo umeweka mkazo maalumu wa kumaliza vitendo vya ukatili na udhalilishaji dhidi ya wanawake na watoto.

Alisema kuwa lengo ni kuwaelezea watu wenye ulemavu mpango huo ili kuufahamu kwa undani pamoja na kutoa maoni yao wanapohisi uhitaji wa watu hao unapaswa kuingizwa katika mpango huo.

Aidha alisema mkutano huo umetoa nafasi kuona mafanikio na matatizo katika mpango huo na kutoa kipaumbele cha nini kifanyike katika kuwasaidia watu wenye ulemavu katika mpango huo.





# Wanafunzi wajisaidia vichakani kisa uhaba wa vyoo

**Na Shaban Njia,** SHINYANGA

WANAFUNZI wa Shule ya Msingi Lyamidati katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, wapo hatarini kupata magonjwa ya mlipuko ikiwamo kipindupindu, kuhara damu na kuumwa tumbo kutokana na kujisaidia nyuma ya vyoo na vichakani kwa ukosefu wa matundu ya vyoo.

Shule hiyo yenye wanafunzi 954 ina matundu ya vyoo nane ambayo hayatoshelezi kwa kuwa mahitaji ni matundu 48 hatua ambayo inafanya watoto hao kujisaidia vichakani.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Makoye John, akizungumza na Nipashe ofisini kwake alisema wanafunzi wenye umri mkubwa wanaongoza kujisaidia vichakani.

Alisema wakati wa kipindi cha mapumziko wanafunzi wengi hukimbilia chooni kujisaidia, lakini kutokana na uchache wa matundu ya vyoo inawalazimu kujisaidia kwa awamu na wakati mwingine wale wenye umri mkubwa wanakimbilia kujisaidia nyuma ya vyoo na vichakani.

Alisema wameshafanya vikao mbalimbali kupitia Serikali ya Kijiji na Ofisi ya Mtendaji wa Kata kuangalia namna ya kutatua shida hiyo na kwamba mwaka ujao wataanza na matundu nane kati ya 48 yanayohitajika kwa sababu wananchi wanategemea kupata fedha baada ya kuvuna mavuno yao.

Mwalimu wa Taaluma wa shule hiyo, Hamisi Dotto alisema hali ya kitaaluma kwa wanafunzi ni nzuri na wanafunzi 100 waliohitimu elimu ya msingi mwaka huu watafanya vyema na kujiunga na elimu ya sekondari.

Alisema kipindi cha mvua za masika kuna utoro kwa sababu ya wazazi kuwazuia watoto wao wasiende shule ili wakawasidie katika shughuli za shambani.

Akijibu hoja hiyo, Ofisa Elimu Msingi wa Halmashauri hiyo, Christina Bukoli alikiri shule nyingi za msingi ikiwamo Lyamidati zina na uhaba wa matundu ya vyoo na mwaka huu wa fedha wametenga Sh. milioni 150 kwa ajili ya kutatua tatizo hilo.

Aidha alisema mwaka jana shule hiyo ilipokea Sh. milioni 40 na kuanzisha ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa ambavyo havikukamilika na mwaka huu wa fedha watapokea Sh. milioni 12.5 kwa ajili ya ukamilishaji ili wanafunzi wapate sehemu nzuri ya kusomea.

Bukoli alisema kuna mradi unaitwa Busti unaotekelezwa na serikali wa uboreshaji wa miundombinu ya elimu na kwamba utakapowafikia utasaidia kutatua tatizo hilo.



Ofisa Maendeleo ya Jamii wa kata ya Bulyanhulu, Anna Mwakalinga, akitoa elimu ya kupambana na vitendo vya ukatili kwa wanafunzi wa shule ya msingi ya Bugarama, wilayani Msalala, mkoani Shinyanga jana, wakati wa kampeni ya kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia inayoendeshwa na Mgodi wa Barrick Bulyanhulu, katika kuadhimisha Siku 16 za kupinga vitendo hivyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shirika latoa msaada baiskeli 500 kwa wanafunzi wa kike

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

SHIRIKA la Plan International limetoa msaada wa baiskeli 500 kwa wanafunzi wa kike wanaotembea umbali mrefu kwenda shuleni.

Mkurugenzi wa mradi wa kusaidia watoto wa kike balehe wanaosoma sekondari kuwawezesha kuhitimu masomo yao, Nicodemas Gachu alisema mradi huo unatekelezwa katika mikoa ya Kigoma na Geita kwa ufadhili wa serikali ya Canada na Shirika la Plan International kwa kipindi cha miaka mitano.

Alisema katika Mkoa wa Geita wanafunzi wa kike wanaotembea umbali mrefu watapata baiskeli 300 na Kigoma baiskeli 200.

Mkurugenzi wa miradi wa Shirika la Plan Intenational, Peter Mwakabwale alikabidhi baiskeli hizo kwa wanafunzi hao mbele ya Mkuu wa Wilaya ya Geita, Wilison Shimo aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Geita kwenye uzinduzi wa mradi huo.

Alisema kuwa mbali na shirika hilo kutekeleza mradi huo lakini pia inatekeleza mradi wa elimu na ulinzi wa mtoto, upinga ukatili na uhifadhi wa mazingira.

"Mradi huu utawawezesha wanafunzi wa kike kuhitimu elimu ya msingi na sekondari na kuwaepusha na vishawishi na mimba za utotoni," alisema.

Mwanafunzi wa Shule ya Sekondari, Bung'wangoko mkoani Geita, Aneth Komanya alishukuru shirika hilo kwa msaada huo na kuahidi kusoma kwa bidii na kufikia malengo yake.

# TAKUKURU yaokoa mil.470/- za madini ya ujenzi

**Na Vitus Audax,** MWANZA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Mwanza imefanikiwa kudhibiti mianya ya upotevu wa Sh.milioni 470 katika ukusanyaji wa mapato ya madini ya ujenzi ndani ya halmashauri tatu za Kwimba, Misungwi na Sengerema.

Imeelezwa kuwa katika halmashauri hizo hakukuwa na mapato yaliyokusanywa kupitia ushuru wa madini hayo ndani ya maeneo ya machimbo na kwenye vizuizi, hivyo kusababisha upotevu wa mapato na kulisababishia hasara taifa.

Hayo yalibainishwa jana jijini Mwanza na Mkuu wa TAKUKURU mkoani humo, James Ruge wakati akitoa taarifa ya ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo yenye thamani ya Sh. bilioni 16.2 katika robo ya mwaka kati ya Julai hadi Septemba mwaka huu.

Ruge alisema katika halmashauri hizo walibaini kuwapo kwa machimbo holela ya madini ya ujenzi yasiyofuata utaratibu hivyo kuikosesha serikali mapato kupitia rasilimali hizo.

Alisema mamlaka hiyo imefanikiwa kudhibiti upotevu huo ikiwa ni pamoja na utolewaji wa vibali na leseni za uchimbaji wa madini hayo pamoja na kusaidia halmashauri hizo kutenga maeneo rasmi kwa ajili ya uchimbaji wa madini hayo na kudhibiti uchimbaji holele.

Alisema hatua hiyo imeisaidia serikali kukusanya Sh.milioni 477.1 katika kipindi cha robo mwaka ya Julai hadi Septemba huku baadhi ya wakandarasi waliokuwa wakikwepa kulipa ushuru nao wakianza kulipa ushuru huo.

Katika hatua nyingine Ruge alisema TAKUKURU imefanikiwa kupokea taarifa 126 za kiuchunguzi na kati ya taarifa hizo 106 zinahusu vitendo vya rushwa na 20 ni masuala mengine.

Alisema wamefanikiwa kufungua mashtaka 57 kwa watumishi wa umma waliobainika kujihusisha na vitendo vya rushwa na kati ya kesi hizo serikali imefanikiwa kushinda tisa kati ya 11 zilizoamuliwa.

Katika hatua nyingine Ruge alisema taasisi hiyo itaendelea kushirikiana na wananchi katika kuzuia na kupambana na vitendo vya rushwa mkoani humo.

## UN: M23 iliwauwa raia 131

Ujumbe wa Umoja wa Mataifa nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (MONUSCO) unasema waasi wa M23 waliwauwa raia 131 mashariki mwa nchi hiyo mnamo Novemba 29 na 30 mwaka huu.

Kulingana na matokeo ya uchunguzi wa awali, waliouwawa walikuwa sehemu ya mauaji yaliyokuwa yanafanywa kwa ajili ya kulipiza kisasi kwa raia. MONUSCO iliongeza kwamba wanaume 102, wanawake 17 na watoto 12 waliuwawa kwa risasi za moto au silaha zingine.

Umoja wa Mataifa ulisema watu wanane walijeruhiwa kwa risasi na 60 wengine kutekwa nyara huku karibu wanawake 22 na wasichana watano wakiwa walibakwa. Mamlaka mjini Kinshasa zilikuwa zimesema watu 300 takriban wote wakiwa ni raia walifariki dunia katika mashambulizi ya M23 katika kijiji cha Kishishe katika mkoa wa mashariki wa Kivu Kaskazini.

M23 ilikuwa imekataa kuhusika na mauaji hayo.

**Umoja wa Mataifa ulisema watu wanane walijeruhiwa kwa risasi na 60 wengine kutekwa nyara huku karibu wanawake 22 na wasichana watano wakiwa walibakwa.**

# Russia yajiandaa vita muda mrefu

**WASHINGTON,** MAREKANI

TAASISI ya Marekani ya Utafiti wa Vita (ISW) imechambua hotuba ya Rais Vladimir Putin, aliyoitoa katika mkutano wa Baraza la Haki za Kibinadamu kwa kueleza Russia inajiandaa na vita vya muda mrefu.

Katika hotuba yake, Rais Putin alisema kwamba operesheni maalum ya kijeshi ni mchakato mrefu na inapaswa kupatikana kwa maeneo mapya.

"Putin alijifananisha na Tsar Peter I wa Russia, kwa kueleza Russia sasa inadhibiti Bahari ya Azov, ambayo Peter alipigania," wamesema wataalamu wa Marekani.

"Kutajwa kwa historia ya kifalme ya Russia kunaweka wazi malengo ya sasa ya Putin nchini Ukraine kama ya kibeberu na bado ni ya kiwango cha juu," uliongeza muhtasari huo.

Ulisema Putin anatayarisha hadhira ya ndani ya nchi yake kwa vita virefu, vya kuchosha ambavyo vinahitajika ili kuyateka maeneo mapya ya Kiukreni.

Aidha, wataalam wa Marekani wanatilia maanani matumizi ya kwanza ya ndege zisizo na rubani za Shahed zilizotengenezwa na Iran nchini Ukraine katika kipindi cha wiki tatu zilizopita.

Jeshi la Ukraine lilisema kuwa jeshi la Russia lilizitumia tena Jumatano usiku kwa mashambulio katika miji kadhaa, pamoja na mikoa ya Dnieper, Kyiv, Poltava, Zhytomyr na Zaporozhye.

"Vikosi vya Urusi vina uwezekano wa kubadilisha ndege zisizo na rubani kwa matumizi katika msimu wa baridi na kuna uwezekano wa kuzitumia zaidi katika wiki zijazo kushambulia miundombinu muhimu ya Ukraine," wataalam hao wa ISW waliandika.

Wakati huo huo, Kansela wa Ujerumani, Olaf Scholz, amesema hatari ya silaha za nyuklia kutumika katika mzozo wa Ukraine imepungua.

"Russia imeacha kutishia kutumia silaha za nyuklia ili kukabiliana na jumuiya ya kimataifa kuashiria mstari mwekundu," alisema Scholz.

Siku ya Jumatano, Vladimir Putin wa Russia alipendekeza ingetumia tu silaha za nyuklia kulipiza kisasi.

Lakini Marekani ilishutumu maoni hayo kama mazungumzo yasiyo na msingi.

Katika mahojiano yaliyofanyika jana, Scholz alisema kuwa ziara yake ya hivi majuzi nchini China imechangia kukomesha tishio la kuongezeka kwa nyuklia.

Alisema kuwa yeye na Rais wa China Xi Jinping walikuwa wanakubaliana kwamba silaha za nyuklia zisitumike na kwamba nchi za G20 zimesisitiza msimamo huo.

Kauli ya Kansela wa Ujerumani imekuja siku moja baada ya Rais Putin kusema kwamba hatari ya vita vya nyuklia inaongezeka itakuwa ni makosa kuificha.

**BBC**



Aliyekuwa Makamu wa Rais wa Peru, Dina Boluarte, akiwasalimia wabunge baada ya kuapa bungeni kuwa rais mpya wa nchi hiyo.**PICHA:REUTERS**

# Rais mpya wa Peru, Dina Boluarte aapishwa

**LIMA,** PERU

BUNGE la Peru limemwapisha Rais mpya Dina Boluarte baada ya kushuhudiwa mabadiliko ya kisiasa kufuatia Rais aliyekuwepo madarakani Pedro Castillo kukamatwa siku ya Jumatano.

Rais huyo wa mrengo wa kushoto Pedro Castillo, aliondolewa madarakani na wabunge na kisha alikamatwa baada ya kujaribu kulivuruga bunge katika hatua ambayo imekosolewa kuwa kama jaribio la mapinduzi.

Wakipuuzia tangazo lake wabunge wa Peru waliendelea na mipango ya awali ya kupiga kura ya kumwondoa madarakani kwa kura 101 zilizounga mkono na kura 6 zilipinga.

Matokeo hayo yalipokelewa kwa vifijo ndani ya bunge na kisha kumwita makamu wa rais Dina Boluarte kuchukua hatamu.

Dina mwenye umri wa miaka 60 amekuwa mwanamke wa kwanza kushika wadhifa wa urais nchini Peru na ataliongza taifa hilo hadi mwaka 2026.

Mara baada ya kuapishwa rais huyo mwanamke ambaye mwaka mmoja uliopita hakuwa anajulikana sana katika ulingo wa siasa za Peru, ametoa wito wa mwafaka wa kisiasa baada ya miezi kadhaa ya kukosekana utulivu ambao umeshuhudia majaribio mawili ya kumwondoa rais mamlakani.

"Ninachukua madaraka kama rais wa kikatiba wa Jamhuri, nikifahamu wajibu mkubwa unaoniangukia. Na wito wangu wa kwanza, kwani isingeweza kufanyika vinginevyo ni kutoa wito wa umoja mpana zaidi kwa Waperu wote." alisema

Mtafaruku wa kisaisa ulianza jana baada ya Castillo kutangaza kupitia hotuba yake aliyoitoa kwa njia ya Televisheni kwamba analivunja bunge linalodhibitiwa na upinzani, akipiga marufuku utaratibu na kwamba atatawala kwa amri kwa karibu miezi tisa.

Hata hivyo tangazo hilo halikuwazuia wabunge waliokusanyika mapema kuliko ilivyokuwa imepangwa awali kwa ajili ya kupiga kura ya kumwondoa madarakani.

Castillo alilazimika kuondoka Ikulu ya rais akiwa na dhamira ya kuomba hifadhi katika ubalozi wa Mexico kabla ya kukamatwa kwa mujibu wa ripoti ya polisi.

Duru katika ofisi ya mwanasheria mkuu wa serikali zilisema kwamba rais huyo anachunguzwa kwa tuhuma ya uasi.

Mwanasiasa huyo amepelekwa katika kituo cha polisi mashariki mwa Lima ambako rais wa zamani wa taifa hilo Alberto Fujimori ambaye pia aliondolewa madarakani na bunge anatumikia kifungo kwa makosa ya ubadhirifu wa fedha.

Mamia ya waandamanaji wanaomuunga mkono na kumpinga Castillo walikusanyika mbele ya majengo ya bunge jana Jumatano.

Kuelekea kura ya kumwondoa madarakani, Marekani ilimtaka Castillo kufuta uamuzi wake na kusema kwamba baada ya kura hiyo haimtambui tena kama rais.

Serikali za mataifa ya America Kusini zilielezea wasiwasi mkubwa na kutoa wito wa kuheshimu demokrasia.

**DW**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA KIHONDA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na......66/2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: KELYIN MICHAEL NJITAGO WA ARUSHA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA: DAFROSA DAMAS MTENA**

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 12 Mwezi 12 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

Imetolewa leo tarehe 07 mwezi 12 mwaka 2022

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO KIHONDA
MOROGORO
.................................
**HAKIMU**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**RAMADHANI AHMAD PANDE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 955 DUV – SUBARU IMPREZA.** Chassis namba **GH7004480.** Engine namba **EJ20D243728.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/URA/RB/475525/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**BERNADETHA PHILIPO NGONYI** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 349 BYE – TVS / STAR.** Chassis namba **MD625AF41JIB05194.** Engine namba **DF4BJIX04966.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/URA/RB/475313/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**WU ZHOU INVESTMENT CO.LTD** tunatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya ... yenye namba za usajili **MC 782 DBR** Yenye chases namba **LLCLGL300MA503168** Injini namba **LC163FMLUQ302223** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi Taarifa ya polisi RB. Namba **IRI/IRI/RB/475363/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya TANGA**

**Kituo cha MJINI TANGA Mkoa TANGA**

**Usimamizi wa mirathi na 242|2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU ANNA MESHACK MBWAMBO**

**KATIKA SAHURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIOLETWA NA EZEKIEL ELITUMAINI MJEMA**

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama zamwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa
Hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 14 Mwezi 12 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehem anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika

Imetotewa leo tarehe 07 Mwezi 12 mwaka 2022

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO KIHONDA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na......67/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: HAMPHREY WA MOROGORO**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA: KULWA KEDMAN MAMBOLEO**

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 16 Mwezi 12 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

Imetolewa leo tarehe 07 mwezi 12 mwaka 2022

**HAKIMU MFAWIDHI**

- Futa isiyohusika.

Imetolewa leo tarehe ....07.... Mwezi ....12.... Mwaka ....2022

**IN THE COURT OF APPEAL OF TANZANIA**
**AT SUMBAWANGA**
**CIVIL APPEAL NO................................OF 2022**
**BETWEEN**
**BUSAD IBRAHIM**
**(Adminitratrix of the estate of the late Issa Mohamed Doon)................................APPELLANT**
**VERSUS**

1.TREASURY GENERAL..................1ST RESPONDENT
2.VIOVENA & CO.LTD.....................2ND RESPONDENT
3.GODWIN E.NZINYANGWA..........3RD RESPONDENT
4.WEMA H.LUMULIKO..................4TH RESPONDENT
5.GRACE H.LUMULIKO..................5TH RESPONDENT
6.REHEMA PANYA........................6TH RESPONDENTAND
7.HON.ATTORNEY GENERAL..........NECESSARY PARTY

**RECORD OF APPEAL and WRITTEN SUBMISSION**
**RE:SERVICE OF THE RECORD OF APPEAL AND WRITTEN SUBMISSION**
**TO THE: 2ND,3RD,4TH,5TH and 6TH RESPONDENTS**

This is to notify and serve you the RECORD OF APPEAL and WRITTEN SUBMISSION in respect of the above Appeal.The record of appeal and Written Submission are found via the Email of the High Court of Tanzania at Sumbawanga,and the office of Mwakolo and Company Advocates.You are accordingly served.

Email:**hcsumbawanga@judiciary.go.tz**

**Dated at Mbeya this 05th day of November,2022.**

..........................................
**SIMON T.M. MWAKOLO**
**( ADVOCATE FOR THE APPELLANT )**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MOROGORO**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**
**KITUO CHA KINGOLWIRA**

**Usimamizi wa Mirathi Na......8/2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: RAJABU MWENYEMVUA KALABI**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA: ABDALLAH R. RAJABU**

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 20 Mwezi 12 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

Imetolewa leo tarehe 02 mwezi 12 mwaka 2022

## KUPOTEA KWA LESENI YA MAKAZI

**BALO YAJILE MWAKATALA anatangaza kupotea kwa Leseni ya makazi yenye majina BALO YAJILE MWAKATALA . Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: DAR/URA/RB/475471/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya DODOMA**
**Kituo cha MAKOLE Mkoa DODOMA**
**Usimamizi wa mirathi Na. 100/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU CHAMLEE MYALIZE wa NDACHI**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA... KHADIJA MOHAMED KOVA**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 12 Mwezi 12 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo Tarehe 24 Mwezi 11 Mwaka 2022

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HARMONIZE

## AOMBA RADHI KUHUSU BANGI



NYOTA wa Bongofleva, Rajab Kahali maarufu Harmonize ameomba radhi kutokana na wimbo wake na mwimbaji wa dancehall wa Jamaica, Konshens 'Weed Language', siku moja tu baada ya kupokea onyo kali kutoka kwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Tanzania (DCEA).

Jumatano, Kamishna Mkuu wa DCEA, Gerald Kusaya alionya kuwa hatua kali zitachukuliwa dhidi ya wanamuziki wanaotunga nyimbo za kuhamasisha matumizi ya dawa za kulevya.

"Kuna wasanii wanahamasisha matumizi ya dawa za kulevya ikiwamo bangi. Kama kuna wasaniii wanaodhani badala ya kutunga nyimbo za kuhamasisha jamii, wanatunga za kuhamasisha matumizi ya dawa za kulevya, sheria yetu inasema hao tutawachukulia hatua," alisema Kusaya.

Onyo hilo linaonekana kuzua hofu kwa Harmonize ambaye juzi asubuhi aliomba radhi hadharani kupitia taarifa iliyoandikwa.

Mwimbaji huyo mahiri, kupitia lebo yake ya Konde Music Worldwide alisisitiza wimbo wake 'Weed Language' ulikuwa na lengo la kuupanua na kuukuza muziki wa Tanzania duniani kote lakini ulitafsiriwa isivyofaa.

"Kutokana na kadhia iliyosababishwa na maudhui ya wimbo huo tunaomba radhi na tunaahidi kuuondoa wimbo huo kwenye mitandaoyote ya kijamii," taarifa kutoka kwa usimamizi wa Konde Music Worldwide ilisomeka.

"Pia tunaahidi kuboresha nyimbo zetu ili ziendane na utamaduni wetu pamoja na miongozo ya mamlaka ya serikali."

## D'BANJI ASHIKILIWA KWA UFISADI NIGERIA



TUME ya Huru ya Ufisadi na Makosa Mengine ya Nigeria (ICPC) imethibitisha kwa BBC inamshikilia mwanamuziki, Daniel Oyebanjo, maarufu kama D'Banj.

Taarifa ya ICPC ilisema inamshikilia mwimbaji huyo kwa uchunguzi wa ulaghai unaohusishwa na mpango wa N-Power, mabilioni ya fedha ya kuwezesha vijana wa Nigeria.

N-Power ni mpango ambao Rais, Muhammadu Buhari, alianzisha Juni 8, mwaka 2016, kushughulikia masuala ya ukosefu wa ajira kwa vijana na uwezeshaji, na kusaidia kuongeza maendeleo ya kijamii.

Katika taarifa iliyotolewa na Kamishna wa ICPC, Azuka Ogugua, ilieleza chanzo cha kuzuiliwa kwa D'banj.

"Takriban watu 10 wanashikiliwa na ICPC katika miezi michache iliyopita kuhusiana na ulaghai wa N-Power, na wamepewa dhamana ya kiutawala baada ya kuzuiliwa kwao. Yupo mwanamuziki, Oladipo Daniel Oyebanjo.

"Oyebanjo (D'banj) alijisalimisha na kuzuiliwa katika makao makuu ya ICPC Desemba 6, mwaka huu na kwa sasa anasaidia wapelelezi kubaini mazingira ya madai ya ulaghai ya walalamishi.

## NYOTA NDOGO ATEMA NYONGO



MWANAMUZIKI mkongwe wa Mombasa, Abdalla maarufu Nyota Ndogo amewasuta wanamitandao ambao wamekuwa wakimwonyesha chuki na kumsema sura yake sio nzuri.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Nyota Ndogo ameeleza kuchukizwa kwake na watu ambao wamekuwa wakikosoa sura yake na kuhoji jinsi alivyoweza kupata mume mzungu mwenye fedha.

"Siku moja mtu aliniuliza wewe Nyota ulivyo na sura mbaya na vile una fedha ingekua mimi ningefanya sajari, hapo ndio binadamu tumefikisha. Tumesahau mpaka aliyetuumba. Hii sura bado hamujaizoea tu? Basi haiendi popote ulipo," aliandika msanii huyo.

Aliwashauri kutumia akili zao vizuri huku akiwabainishia sura sio kila kitu kinachohitajika katika mafanikio maishani.

"Wengine mnaketi tu mkisema Nyota ana sura mbaya. Mnauliza aliwezaje kupata mzungu? Anakaa kienyeji!.. tumia akili ndugu yangu, akili hailetwi na sura. Wengine hata darasa la nane hatukufika, lakini Alhamdulillahi twashukuru Mwenyezi Mungu alitupatia akili.

"Tumesota tukiwa wadogo lakini hatukukata tamaa hadi tukaanza kuwajengea maisha ya baadaye watoto wetu," aliongeza.

Mwanamuziki huyo aliweka wazi hakuwahi kufuata fedha kwa mume wake mzungu, Henning Neilsen.

Alisema hapo awali aliwahi kuwa kwenye ndoa na mtu asiyejaliwa fedha nyingi huku akieleza kuwa kila wakati anapojitosa kwenye ndoa huwa anafuata mapenzi.

"Kule kwa wale maskini pia tulikuwa tunafuata mapenzi. Jameni wengine wetu tuna mapenzi ya kweli sio fedha. Ametokea wakati huu nimeangukia mapenzi kwa mtu mwenye fedha.

# AZAM, MALIMAO DIMBANI MICHUANO KOMBE LA FA

**Na Adam Fungamwango**

AZAM FC inatarajia kuikaribisha Malimao kutoka Katavi katika mechi ya raundi ya pili ya mashindano ya Kombe la FA itakayochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Timu zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara zinaanzia raundi ya pili baada ya mechi za awali kuzihusisha klabu za Championship, First League na mabingwa wa mikoa.

Bingwa wa michuano hiyo inayoendeshwa kwa mtindo wa mtoano ataiwakilisha Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

**Kaimu Ofisa Habari wa Azam FC, Hasheem Ibwe, aliliambia gazeti hili maandalizi kuelekea mechi hiyo yamekamilika na wanaahidi kikosi chao kitatoa burudani kwa mashabiki wao.**

Ibwe alisema hakutakuwa na kiingilio chochote kwa mashabiki watakaofika kushuhudia mtanange huo kama ilivyokuwa kawaida kwao watapocheza mechi za Ligi Kuu.

Mechi nyingine za michuano hiyo zitakazochezwa leo ni kati ya wenyeji Nduguti wataikaribisha Gwambina FC, African Lyon itakuwa kwenye Uwanja wa Uhuru kucheza dhidi ya Mbuni FC, Polisi Katavi itakuwa kwenye Uwanja wa Azimio, Mpanda ikiwasubiri Mbeya Road.

Green Warriors itacheza dhidi ya Stand United kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Dar es Salaam na Stand FC ya Mtwara itakuwa ugenini kwenye Uwanja wa Sokoine Mbeya kuivaa Mbeya City.

Simba itaanza kampeni ya kuwania taji hilo kwa kuwaalika Eagle FC wakati Yanga itawashubiri Kurugenzi ya mkoani Tabora.

Yanga ndio mabingwa watetezi wa mashindano hayo ambapo katika mechi ya fainali waliifunga Coastal Union ya jijini, Tanga.



Bendi ya Jeshi la Wananchi (JWTZ), ikitumbuiza katika mahafali ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima yaliyofanyika Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Mapinduzi Cup mambo yameiva*

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

JUMLA ya timu 12 zinatarajiwa kushiriki katika mashindano ya Kombe la Mapunduzi yatakayofanyika kuanzia Januari Mosi hadi 13, mwakani.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kombe la Mapinduzi, Khamis Abdallah Saidi, alizitaja timu zitakazoshiriki kutoka Tanzania Bara ni pamoja na Simba, Yanga, Azam FC, Singida Big Stars na Namungo FC.

Saidi alizitaja timu nyingine kutoka Zanzibar kuwa ni KVZ FC, Malindi SC, Mlandege FC, KMKM, Chipukizi na Jamhuri.

"Maandalizi ya mashindano haya yanakwenda vizuri, tunatarajia ushindani utaendelea, lakini muhimu ni kuimarisha mahusiano na kuzipa maandalizi mazuri timu zinazotarajia kushiriki mashindano ya kimataifa," alisema mwenyekiti huyo.

Alisema mashindano hayo yanatarajiwa kushirikisha timu moja tu kutoka nje ya Tanzania ambayo ni Aigle Noer, mabingwa wa Ligi Kuu Burundi.

Alitaja zawadi ya mshindi wa kwanza katika mashindano hayo ni Sh. milioni 30 na mshindi wa pili ataondoka na Sh. milioni 20.

## Yanga Princess yakubali ilizidiwa

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kufanikiwa kuifunga Yanga Princess bao 1-0 katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam juzi, benchi la ufundi la Fountain Gate Princess limesema hiyo ni dalili njema kwa timu yao msimu huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Fountain Gate Princess, Alex Alumirah, alisema lengo lake ni kutwaa ubingwa wa ligi hiyo msimu huu na ushindi huo utawaongezea umakini kuelekea mechi zinazofuata.

"Ukitaka kuwa bingwa lazima uzifunge Simba na Yanga, kwa matokeo tuliyoyapata yameonyesha wachezaji wangu wana uwezo wa kuifunga timu yoyote kubwa," alisema Alumirah.

Kocha huyo aliwapongeza wachezaji wake kwa kiwango kizuri walichokionyesha katika mchezo huo wa ugenini.

Alisema wachezaji wake walifuata maelekezo aliyowapa kabla ya kuingia uwanjani huku akiongeza nidhamu ya ukabaji waliyoifanya ilisaidia kupata ushindi huo.

"Niliwaambia wachezaji wangu wahakikishe wanamfunga mpinzani wetu dakika za mwanzo, nikijua tukimfunga muda huo atapoteza nguvu na kweli wamefanya kama nilivyotaka," kocha huyo alisema.

Aliongeza hata hivyo timu yake haikucheza vizuri katika kipindi cha pili na anakwenda kuyafanyia kazi makosa aliyoyaona ili yasijitokeze tena kwenye michezo mingine.

Kocha Mkuu wa Yanga Princess, Edna Lema, alisema ameukubali 'muziki' ulioonyeshwa na wachezaji wa Fountain Gate Princess.

"Ninaipongeza Fountain Gate Princess kwa ushindi walioupata, nitafanyia kazi mapungufu yote ili yasijitokeze katika mchezo wetu ujao, kipindi cha pili timu yangu ilicheza vizuri isipokuwa hatukupata nafasi ya kurudisha goli, ligi ndio imeanza naamini tutafanya vizuri kwenye mchezo ujao," Edna alisema.



Edna Lema

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### AMRABAT ANUKIA ENGLAND

KLABU za Tottenham Hotspurs na Liverpool zinawania kumsajili kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Morocco, Sofyan Amrabat, mwenye umri wa miaka 26, kutoka Fiorentina katika dirisha la uhamisho litakapofunguliwa Januari. (***90min***)

### MILAN WAMTAKA MARTINELLI

AC Milan inatarajiwa kushindana na Barcelona katika mbio za kumsajili kiungo wa kati wa Arsenal na Brazil, Gabriel Martinelli, mwenye umri wa miaka 21, iwapo wataamua kumuuza winga wa Ureno, Rafael Leao (23) kwenye dirisha la Januari. (***Calciomercato***)

### ARSENAL YAMKACHA MUDRYK

ARSENAL huenda ikalazimika kuahirisha mpango wao wa kumnunua winga wa Shakhtar Donetsk na Timu ya Taifa ya Ukraine, Mykhailo Mudryk, mwenye umri wa miaka 21, baada ya kuumia kwa mshambuliaji wa Brazil, Gabriel Jesus. (***Sun***)

### RABIOT AITAMANI EPL

KIUNGO wa kati wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Adrien Rabiot, mwenye umri wa miaka 27 amesema angependa kucheza Ligi Kuu England (EPL). Mkataba wa mchezaji huyo anayelengwa na Manchester United pamoja na klabu ya Juventus unamalizika mwaka wa 2023. (***Express***)

### GAKPO AITAJA UNITED

WINGA wa PSV na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Cody Gakpo, mwenye umri wa miaka 23, amesema "atafikiria" kuhusu kujiunga na Manchester United, lakini hajawasiliana na klabu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu England. (***NRC***)

### MUSIALA KUULA BAYERN

KLABU ya Bayern Munich inatazamia kumpa mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Jamal Musiala, mwenye umri wa miaka 19 mkataba mpya. (***Bild***)

### ZAHA ANUKIA MARSEILLE

KLABU y Marseille inataka kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ivory Coast, Wilfried Zaha, mwenye umri wa miaka 30 kutoka Crystal Palace baada ya mkataba wake utakapokamilika hapo mwakani. (***90min***)

### NEWCASTLE BAJETI NDOGO

KOCHA, Eddie Howe, amesema kanuni za udhibiti wa matumizi ya ununuzi wa wachezaji kwa haki sawa huenda ukapunguza bajeti ya Newcastle katika dirisha la uhamisho la Januari. (***Mail***)

### ROMA YAMFUATA DEPAY

AS Roma ipo katika hatua za mwisho za mazungumzo na wakala wa mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Uholanzi, Memphis Depay, mwenye umri wa miaka 28, kuhusu kuhama kutoka Barcelona na kujiunga na klabu hiyo ya Italia.(***Sport***)

### JOAO ANUKIA ATLETICO

ATLETICO Madrid iko tayari kusikiliza ofa kwa mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ureno, Joao Felix, mwenye umri wa miaka 23, ambaye anataka kuondoka katika klabu hiyo. (***TVE, via Mail***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# GAPKO: MAN UNITED WAKIJA, NITAWAFIKIRIA

## ●●● Afunguka klabu hiyo ilionyesha nia ya kuhitaji huduma yake tangu...

**DOHA,** Qatar

NYOTA wa Timu ya Taifa ya Uholanzi anayekipiga katika klabu ya PSV Eindhoven, Coady Gapko, ameweka wazi ataifikiria Manchester United kama itamfuata.

Nyota huyo ambaye amekuwa na msimu mzuri sana kuanzia katika klabu yake mpaka sasa akiwa na Uholanzi, amekua nguzo muhimu kwenye kikosi cha kocha, Louis Van Gaal, kutokana na ubora ambao amekua akiuonyesha.

**Gapko amefunga mabao matatu katika michuano ya Kombe la Dunia inayoende lea nchini hapa na kuzifan ya timu mbalimbali kuanza kumfuatilia kwa karibu.**

Mchezaji huyo alipoulizwa kuhusu kujiunga na Manchester United ambayo inahusishwa naye kwa karibu alisema, "Sijaskia kuhusu Manchester United bado.

"Kama watakuja, nitafikiria na Mungu akisaidia. Nilifikiri kuhusu Manchester United msimu uliomalizika, lakini kama haikutokea sijui tena kuhusu jambo hilo."

Gapko ni mchezaji aliyekuwa anafuatiliwa kwa karibu na United katika dirisha la usajili lililopita, lakini dili iliharibika mwishoni kabisa.

Lakini mashetani wekundu hao wanaonekana kurudi kwa kasi na kuhitaji saini ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi.







# RABIOT: UFARANSA HAIMTEGEMEI MBAPPE




**DOHA, Qatar**

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Ufaransa na Klabu ya Juventus inayoshiriki Ligi Kuu ya Italia, Adrien Rabiot, amesema Ufaransa haimtegemei mshambuliaji, Kylian Mbappe.

Mbappe hadi sasa yupo kileleni katika orodha ya wafungaji bora wa michuano ya Kombe la Dunia mwaka huu baada ya kufunga mabao matano na kutoa pasi mbili za magoli.

Mbappe amejipambanua kama mchezaji muhimu wa Ufaransa.

Na Rabiot anakiri Mbappe ni silaha yao kubwa kwenye kikosi, lakini anaamini timu hiyo haimtegemei yeye tu kupata matokeo, kwa sababu kuna wachezaji wengine wenye uwezo wa kufanya mabadiliko muda wowote.

Rabiot anaeleza wanamhesabu Mbappe kama wachezaji wengine kwenye kikosi na cha msingi ni kuomba kila mchezaji kwenye timu yao awe fiti kuelekea mchezo wao wa robo fainali dhidi ya England ambao utachezwa kesho.

Hivyo mchezo huo unatarajiwa kuwa mkali na wenye ushindani mkubwa.

# Walker apania England vs Ufaransa

**DOHA, Qatar**

MLINZI wa Manchester City, Kyle Walker, hatampa, Kylian Mbappe nafasi yoyote wakati England itakapomenyana na Ufaransa katika mechi ya robo fainali ya Kombe la Dunia itakayochezwa kesho.

England ya Gareth Southgate iliiondoa Senegal katika hatua ya 16 bora, lakini wanakabiliwa na mtihani mgumu zaidi dhidi ya mabingwa hao watetezi.

Walker anafahamu vyema kuhusu tishio la nyota wa PSG, Mbappe na amesisitiza lazima waichukulie Ufaransa kama timu na si watu binafsi.

Mchezaji huyo wa City, mwenye umri wa miaka 32, amesema: "Mbappe ni mchezaji mzuri katika kiwango kizuri kwa hiyo haitakuwa kazi rahisi, lakini kama mtaalamu unataka kucheza dhidi ya wachezaji bora na ni mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani ninaelewa tunachohitaji kufanya ili kumzuia."

Walker amesema amekutana na baadhi ya wachezaji bora duniani, lakini lazima achukulie kama mchezo mwingine na lazima ampe heshima, lakini sio sana huku akisisitiza utakuwa mchezo mgumu kwao.

"Tunamfahamu ni mchezaji mzuri na ndio maana anazingatia maswali yote. Lakini tusimsahau Olivier Giroud, ambaye amefunga mabao mengi, Ousmane Dembele na Antoine Griezmann.

"Kwangu mimi, maswali yote yasiwe kuhusu yeye (Mbappe). Nashukuru ni mwanasoka mzuri lakini kuna wengine pia."



HABARI MICHEZO

554,107/-

# MAYELE, MGUNDA WANG'ARA TUZO ZA LIGI KUU NOVEMBA

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa Yanga, Fiston Mayele, amechaguliwa kuwa Mchezaji Bora wa Ligi Kuu Tanzania Bara Novemba sambamba na Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, imeelezwa.

Taarifa iliyotolewa Idara ya Habari na Mawasiliano ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), imesema wanamichezo hao wamechaguliwa na Kamati ya Tuzo za Shirikisho la Soka Nchini (TFF), iliyokutana Desemba 6,mwaka huu.

Nyota huyo kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), alionyesha kiwango kizuri katika mwezi huo, alifanikiwa kufunga mabao saba, ikiwamo 'hat-trick' kwenye mechi dhidi ya Singida Big Stars.

Pia alihusika katika upatikanaji wa bao moja kwenye mechi tano tu alizocheza kwa kuwashinda, Moses Phiri wa Simba na Mrundi Saido Ntibazonkiza wa Geita Gold FC.

Katika mechi hizo Yanga iliichapa Kagera Sugar bao 1-0, Singida Big Stars mabao 4-1, ikailaza Dodoma Jiji na Mbeya City magoli 2-0 kila moja, kabla ya kupoteza kwa Ihefu mabao 2-1.

Kamati ilisema Mgunda alishinda tuzo hiyo dhidi ya Hans van Pluijm wa Singida Big Stars na Mecky Maxime wa Kagera Sugar.

Kwa mwezi huo, Simba iliifunga Ihefu bao 1-0, ikalaza Ruvu Shooting mabao 4-0, Polisi Tanzania mabao 3-1, na kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Singida Big Stars na Mbeya City pia.

"Kamati ya Tuzo haikuuhusisha timu ya Azam FC kutokana na kutokuwa na kocha mkuu kwenye mwezi huo," ilisema sehemu ya taarifa.

Meneja wa Uwanja wa CCM Liti ulioko mkoani Singida, Hassan Simba, alichaguliwa kuwa meneja bora wa viwanja.



## Simba yaitangazia hali ya hatari Eagle

INATOKA UK. 32

ya daktari, ripoti yao itatueleza kama afya yake iko tayari kwa mapambano au vinginevyo, tunahitaji mchango wa kila mchezaji ili tufikie malengo yetu," aliongeza kocha huyo wa zamani wa Coastal Union.

Alieleza anatarajia kuwapumzisha baadhi ya wachezaji waliotumika katika mechi nyingi zilizopita ili kuwapa muda wa kupumzika na watakaporejea wawe imara zaidi.

Simba ilikuwa na wakati mzuri katika mechi nne walizocheza mwezi uliopita ambapo walishinda dhidi ya Ihefu FC, Namungo FC, Ruvu Shooting na Polisi Tanzania.

Kwa matokeo hayo, Kamati ya Tuzo ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), ilimtangaza kocha huyo kuwa mshindi wa tuzo ya Kocha Bora wa Novemba.

## AZAM FC 'VITANI'

INATOKA UK. 32

iliyopelekea Namungo kupokea kichapo cha mabao 2-0 ni ubora, uzuri wa uwanja wao ambao unachezeka vyema.

Kaze alisema uwanja mzuri kama ule na unasaidia wachezaji wanaojua kandanda kuonyesha vyema viwango vyao na ndicho walichokifanya katika mchezo huo wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliochezwa juzi usiku.

"Tulijua kwenye uwanja huu si rahisi kwa timu nyingine kupata matokeo kwa sababu ni wa nyumbani kwa wenyeji wetu, sisi tumeinjoi sana kucheza hapa kuliko Namungo wenyewe, ndiyo maana umeona tumecheza vizuri na kushinda pia.

Nawapongeza wachezaji wangu wametekeleza majukumu yao, tumemiliki mpira na tumepata nafasi kama tano hivi za kufunga mabao, tumefunga mabao mawili, tumepata pointi tatu muhimu," alisema Kaze.

Denis Kitambi, Kocha wa Namungo, alikiri kikosi chake kilifanya makosa ambayo yalisababishwa kuadhibiwa katika mchezo huo.

"Tumefanya makosa na tumeadhibiwa, kipindi cha kwanza mpango wetu haukwenda vizuri, wakati wa mapumziko ulifanyiwa kazi. Niliwaambia wachezaji kipindi cha pili tucheze ili tuwe na hatari zaidi kwenye lango la Yanga na tulitengeneza nafasi ambazo hatukuzitumia," Kitambo alisema.

Mechi hiyo ilikuwa ni ya kukamilisha mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu, Yanga ikiwa kileleni kwa kujikusanyia pointi 38, Namungo ikimaliza ikiwa kwenye nafasi ya tisa kwa pointi zake 18 kibindoni.


SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. 10/12/22 | 18:00 | Blackpool vs Birmingham | 2.68 | 3.28 | 2.58 |
| 2. 10/12/22 | 18:00 | Swansea vs Norwich City | 2.37 | 3.38 | 2.88 |
| 3. 10/12/22 | 18:00 | Lincoln vs Wycombe | 2.83 | 3.28 | 2.46 |
| 4. 10/12/22 | 18:00 | Bristol Rovers vs Port Vale | 2.52 | 3.32 | 2.72 |
| 5. 10/12/22 | 18:00 | Oxford Utd vs Barnsley | 2.34 | 3.29 | 2.99 |
| 6. 10/12/22 | 18:00 | Grimsby vs Tranmere | 2.26 | 3.19 | 3.24 |
| 7. 10/12/22 | 18:00 | Salford City vs Walsall | 2.42 | 3.20 | 2.95 |
| 8. 10/12/22 | 21:00 | Villarreal B vs Tenerife | 2.74 | 2.83 | 2.88 |
| 9. 10/12/22 | 22:00 | England vs France | 3.04 | 3.24 | 2.43 |
| 10. 11/12/22 | 16:00 | Genclerbirligi vs Erzurum BB | 2.53 | 3.48 | 2.58 |
| 11. 11/12/22 | 16:00 | Gillingham vs Bradford City | 3.24 | 3.14 | 2.28 |
| 12. 11/12/22 | 16:00 | QPR vs Burnley | 3.08 | 3.33 | 2.27 |
| 13. 11/12/22 | 16:30 | Calcio Lecco vs Padova | 2.31 | 3.06 | 3.16 |
| 14. 11/12/22 | 16:30 | Feralpisalo vs Novara | 2.26 | 3.05 | 3.40 |
| 15. 11/12/22 | 16:30 | Roda Kerkrade vs Heracles | 2.59 | 3.43 | 2.59 |
| 16. 11/12/22 | 16:30 | De Graafschap vs FC Eindhoven | 2.41 | 3.43 | 2.79 |
| 17. 11/12/22 | 16:30 | Mantova vs Pro Vercelli | 2.60 | 3.05 | 2.90 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 09/12/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 11:45 | 5924 | Brisbane Roar vs Adelaide United | 2.45 | 3.48 | 2.63 |
| 13:00 | 1444 | Kapaz vs Turan Tovuz | 2.53 | 3.07 | 2.63 |
| 14:00 | 2010 | Shijiazhuang vs Wuhan Zall | 2.62 | 3.11 | 2.52 |
| 14:00 | 2128 | Kasetsart University FC vs Suphanburi | 2.82 | 3.31 | 2.26 |
| 14:30 | 1603 | Wuhan Three Towns FC vs Shandong Luneng | 1.96 | 3.26 | 3.55 |
| 14:30 | 2766 | Shenzhen vs Changchun Yatai | 3.98 | 3.35 | 1.82 |
| 14:30 | 5859 | Shanghai Shenhua vs Dalian Aerbing | 2.33 | 3.10 | 3.10 |
| 15:00 | 5774 | Ararat Armenia vs Lernayin Artsakh | 1.20 | 5.25 | 12.63 |
| 15:15 | 5398 | Al Hikma vs AL Ahed | 9.80 | 5.20 | 1.29 |
| 15:40 | 2581 | Al Suwaiq vs Bahla | 2.01 | 3.15 | 3.90 |
| 16:00 | 2183 | Kampala City Council vs Express FC | 1.60 | 3.71 | 4.88 |
| 16:05 | 3793 | Al Nasr Salalah vs Al Seeb | 5.26 | 2.92 | 1.76 |
| 16:15 | 1885 | PO Triglias vs FC Veria | 1.91 | 3.01 | 4.08 |
| 17:00 | 1115 | Irb Ouargla vs ES EL Ghozlane | 2.34 | 2.67 | 3.35 |
| 17:00 | 2671 | MC EL Eulma vs Hamra Annaba | 1.66 | 3.11 | 5.64 |
| 17:00 | 3099 | MO Constantine vs JS Bordj Menaiel | 2.27 | 3.10 | 3.25 |
| 17:00 | 3368 | USM EL Harrach vs Ain M'lila | 1.42 | 3.73 | 7.75 |
| 17:00 | 4387 | USM Annaba vs US Souf | 2.16 | 3.25 | 3.35 |
| 17:00 | 4755 | NRB Teleghma vs CA Batna | 1.56 | 3.41 | 6.04 |
| 17:00 | 5203 | Ib Khemis El Khechna vs US Chaouia | 2.48 | 2.87 | 2.87 |
| 17:00 | 5395 | Hyderabad FC vs East Bengal | 1.50 | 4.10 | 5.27 |
| 17:00 | 5605 | JSM Skikda vs AS Khroub | 6.20 | 4.40 | 1.47 |
| 17:00 | 5628 | Pyunik Yerevan vs Urartu | 2.14 | 2.92 | 3.45 |
| 18:00 | 4126 | Croatia vs Brazil | 8.21 | 4.80 | 1.35 |
| 20:00 | 1535 | Doxa Katokopia vs AEK Larnaca | 4.92 | 3.81 | 1.66 |
| 20:00 | 2506 | Sepsi Osk vs Voluntari | 1.52 | 3.85 | 6.13 |
| 20:00 | 2899 | Samsunspor vs Yeni Malatyaspor | 1.36 | 4.57 | 6.81 |
| 20:00 | 4322 | Pafos FC vs Apoel Nicosia | 2.47 | 3.05 | 2.95 |
| 21:00 | 1547 | Chemnitz vs Hertha II | 1.52 | 4.09 | 5.06 |
| 21:00 | 2852 | ETSV Weiche vs Hannover II | 2.10 | 3.74 | 2.81 |
| 21:00 | 4019 | Astoria Walldorf vs Hoffenheim II | 3.40 | 3.50 | 1.92 |
| 21:30 | 1306 | Saint Brieuc vs Le Mans | 3.11 | 3.31 | 2.16 |
| 21:30 | 1309 | FC Oberneuland vs Brinkumer SV | 1.36 | 5.42 | 5.62 |
| 21:30 | 2370 | Sedan vs Cholet | 2.00 | 3.30 | 3.55 |
| 21:30 | 3135 | Viktoria Griesheim vs FC 1931 Eddersheim | 2.90 | 4.10 | 2.08 |
| 21:30 | 3185 | Bourg Peronnas vs Orleans | 1.99 | 3.31 | 3.55 |
| 21:30 | 3628 | Red Star vs FC Versailles 78 | 1.95 | 3.35 | 3.65 |
| 21:30 | 5193 | Le Puy vs Dunkerque | 3.12 | 3.22 | 2.21 |
| 21:30 | 5900 | Villefranche Sur Saone vs Chateauroux | 2.40 | 3.12 | 2.87 |
| 21:30 | 5984 | Avranches vs Nancy | 3.20 | 3.30 | 2.13 |
| 22:00 | 1674 | Jong KRC Genk vs Club Brugge U21 | 2.08 | 3.75 | 2.96 |
| 22:00 | 2100 | Paris 13 Atletico vs Bastia Borgo | 2.01 | 3.30 | 3.50 |
| 22:00 | 3489 | Eintracht Frankfurt II vs Baunatal | 1.45 | 5.20 | 5.40 |
| 22:00 | 4634 | Netherlands vs Argentina | 3.40 | 3.05 | 2.23 |
| 22:00 | 5065 | Hamburger SV III vs FC Suderelbe | 3.40 | 4.20 | 1.85 |
| 22:45 | 2246 | Coleraine FC vs Crusaders Belfast | 2.87 | 3.41 | 2.18 |
| 22:45 | 2367 | Crawley Town vs Hartlepool | 2.03 | 3.42 | 3.37 |
| 22:45 | 2449 | Arbroath vs Dunfermline | 2.11 | 3.34 | 3.05 |
| 22:45 | 5335 | Alloa Athletic vs Queen of South | 2.08 | 3.46 | 3.02 |
| 23:45 | 4482 | Famalicao vs Tondela | 1.78 | 3.34 | 4.17 |

18+ CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Ijumaa Desemba 9, 2022

Nipashe




UKURASA 29

**Gapko: Man United wakija, nitawafikiria**



Kiungo wa Yanga, Feisal Salum 'Fei Toto' (kulia), akijiandaa kumtoka beki wa Namungo, Emmanuel Asante katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Majaliwa ulioko Ruangwa, mkoani Lindi juzi usiku. Yanga ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

# AZAM FC YAINGIA 'VITANI' NA YANGA

●●●Yadaiwa kuandaa dau nono ili kumnasa Fei Toto, yenyewe yajivunia...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

WAKATI Yanga ikitamba ubora wa Uwanja wa Majaliwa ulioko Ruangwa, Lindi umesaidia kikosi chake kupata ushindi, habari zilizopatikana jijini zinasema Azam FC inajipanga kuvunja akaunti yake kwa ajili ya kuwania saini ya kiungo nyota wa Jangwani, Feisal Salum 'Fei Toto', imefahamika.

Mchakato wa usajili wa Fei Toto ambaye alitua Yanga akitokea Singida Big Stars, ambayo hakuichezea hata mechi moja, unatarajiwa kuanza rasmi baada ya dirisha dogo la usajili litakapofunguliwa wiki ijayo.

Taarifa zinasema Azam FC kutoa ofa nono kwa mchezaji huyo ili kuimarisha kikosi chake ambacho msimu huu kinahitaji kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara na taji la Kombe la FA.

"Azam FC iko tayari kutoa ofa kubwa ambayo itakuwa na thamani mara tatu au tano ya kiasi cha fedha anacholipwa sasa mchezaji huyo na klabu ya Yanga, " kilisema chanzo hicho.

Kiliongeza Azam FC inafahamu Fei Toto amebakiza miezi 10 katika mkataba wake na wao wanahitaji kuununua muda huo uliosalia.

"Matajiri wamefika mbali, wameshafanya mazungumzo na familia yake (Mama mzazi wa Fei Toto), na mama ameridhia mwanae kuhamia Azam, " kiliongeza chanzo hicho.

Hata hivyo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat', alisema hizo ni tetesi kulingana na ubora anaonyesha mchezji huyo ili kujitengenezea njia ya kupata donge nono kutoka kwa waajiri wake wakati mkataba wake ukielekea tamati.

Popat alisema uwezo na kiwango cha nyota huyo ni kizuri lakini kwa sasa kikosi cha Azam FC kiko kamili kupambana ili kutimiza malengo yao.

"Sisi timu yetu inajitosheleza, Feisal ni mchezaji mzuri lakini hatuna mpango naye, hizo tetesi tu na ni njia za wachezaji kutengeneza mipango ya mikataba inapokaribia kuisha, mchezaji yeyote akiwa kwenye kiwango bora haya mambo yanaibuka kwa kutengenezwa na meneja, ndio muda wa kupiga pesa," alisema Popat.

Naye Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, aliliambia gazeti hili sababu kubwa

INAENDELEA UK. 31

## Simba yaitangazia hali ya hatari Eagle

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, amesema atashusha kikosi kamili katika mechi ya mashindano ya Kombe la FA dhidi ya Eagle FC itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Kikosi cha Simba kimerejea mazoezini jana asubuhi kujiandaa na mechi hiyo ya raundi ya pili baada ya kumaliza mapumziko ya siku mbili.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mgunda, alisema katika soka la sasa hakuna timu ndogo, hivyo kikosi chake kitajiandaa vizuri kuikabili wapinzani wao bila ya kuwadharau.

Mgunda alisema anahitaji kuanza kampeni ya kuwania taji hilo linaloshikiliwa na watani zao Yanga kwa kishindo na hilo linawezekana endapo wachezaji wake watakuwa makini wakati wote wa mchezo.

"Tunajiandaa kuanza vizuri mashindano haya, tunahitaji kushinda ili tusonge mbele katika michuano hiyo ya Kombe la Shirikisho, haitakuwa mechi rahisi, na hakuna mechi nyepesi, mechi zote ni ngumu na zina ushindani kulingana na aina ya mpinzani unayekutana naye," Mgunda alisema.

Kocha huyo alisema malengo yao makubwa ni kuhakikisha wanafanya vizuri na kurejesha mataji yote waliyopoteza katika msimu uliopita na hilo kila mchezaji analifahamu.

"Tumerudi kwenye uwanja wa mazoezi ili kujiimarisha, tutacheza mechi hiyo kwa tahadhari kubwa kwa sababu hakuna timu ambayo ni dhaifu, ukifika hatua hii basi wewe ni bora, timu za daraja la chini husumbua timu kubwa, tunalitambua hilo, hatutawadharau," alisema kocha huyo.

Alisema amefurahi kuona nyota wake, Nelson Okwa, amesharejea nchini kutoka kwao Nigeria alipokwenda kwa ajili ya matibabu na ujio wake unamwongezea kufanya chaguo kwenye kupanga kikosi.

"Bado tunasubir ruhusa

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042